**4 NOVEMBA, 2023**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TATU

**Kikao cha Tano – Tarehe 4 Novemba, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. MICHAEL CHIKOKOTO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Kaguzi za Ufanisi kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano.

Ninayo majina hapa ya Waheshimiwa Wabunge wanaotaka kuchangia, tutaanza na Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecil Mwambe na Mheshimiwa Eric Shigongo, ajiandae.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, cha kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa utulivu wa nchi yetu, lakini pia kwa kutupa nafasi ya kujadili masuala yanayohusu nchi yetu kwa uwazi na bila woga. Sasa kazi iliyobaki ni sisi Wabunge kuwasimamia wananchi ambao wametutuma kuja hapa kusema haki na kuwasemea katika mambo yale ambayo ni maovu.

Mheshimiwa Spika, hii *document* ya CAG iko wazi, ni *public document* kwa hiyo kila mtu anaiona. Hata hapa mtu akisema ataonekana kwamba labda huyu akisema hivi amesema vibaya tutakuwa tunajidanganya tu, kwa sababu hii *document* iko wazi na hata mataifa mengine wameshaisoma. Kwa hiyo, ni kazi yetu sisi Wabunge kuwasemea wananchi ambao wametutuma kuja hapa kusema yale ambayo yanawafaa. Maana yake itakuwa ngumu sana kutosema ambapo unaangalia kila kurasa tatu za majedwali, kila majedwali kumi, matano, manne, matano, sita, saba Halmashauri ya Bunda imo.

Mheshimiwa Spika, kila ukizungumza wizi wa vifaa vya tiba Halmashauri ya Bunda imo, kila ukiuliza sijui hela za *POS* hazikuja Halmashauri ya Bunda imo. Wakati fulani inaniwia vigumu sana kusema hii ripoti kila wakati inaangalia Bunda na Bunda ndiyo jimbo langu na Halmashauri ndiyo Halmashauri yangu, mnaohusika mmeiona hiyo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa najiuliza maswali mengi na Bunge lililopita tulisema hivi haya maazimio tunayoweka humu ndani yanaenda wapi, yaani nani anayatekeleze? Sasa nikajiuliza

wewe Spika na Bunge lako katika Katiba Ibara ya 143 umepewa mamlaka, Ibara ya 96(1) imelipa mamlaka Bunge hili kuunda Kamati mbalimbali na tumeweka *PAC,* tumeweka *LAAC* na tumeweka *PIC.*

Mheshimiwa Spika, sasa najiuliza tuunde Kamati nyingine ambayo itakuwa inafuatilia maazimio ya Ripoti ya *CAG*. Najiuliza tarehe 2 Novemba, 2022 tulizungumza juu ya *KADCO* na tukaamua katika azimio kwamba sasa Serikali iende ikachukue uwanja wa *KIA* yaani Kampuni ya *KADCO* itoke uwanja wa *KIA* ikabidhiwe Serikali kwa Mamlaka ya Ndege Tanzania.

Mheshimiwa Spika, azimio tumeweka na mbaya zaidi nimesoma hapa mpaka Baraza la Mawaziri wameweka wamezungumza hili jambo, mpaka leo tunazungumza hamna kitu. Sasa hayo maazimio tunampa nani, yaani hii kelele tunampigia nani kwa mfano, maana yake mimi naona wezi wote tunaowazungumza humu ndani wengi wameteuliwa na Mawaziri, wengi wameteuliwa na Rais na wengi tunao sisi Chama Cha Mapinduzi ambao ndiyo waamuzi.

Mheshimiwa Spika, yaani Rais wa Chama Cha Mapinduzi, Mawaziri wa Chama Cha Mapinduzi, wezi wanaiba, chama kinawataka wawafukuze wezi hawawatoi. Maazimio ya Bunge tunataka, maazimio ya Bunge hili, mwizi na mtetea mwizi wote waende *lock up* wote mazianyati, tumechoka sasa, tunamtetea nani? Kwa mfano, sasa lile azimio limesema, ninajiuliza hiyo *KADCO* ni mtu au ni nani, yaani *KADCO* ni chombo fulani au nini sasa?

Mheshimiwa Spika, kama azimio la Bunge limesema, Mawaziri wamesema na jambo halitekelezeki na siyo kwamba hiyo *KADCO* inaleta faida, imetengeneza hasara karibu ya shilingi bilioni sijui tano. Hivi ni nini sasa tunasema, tunazungumza kufanya nini? Mheshimiwa nafikiri kwamba tuunde Kamati nyingine ambayo itashughulika na jambo hilo ili itusaidie.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nasikia Wabunge wanazungumza wizi wizi, wizi, nimesoma ripoti hii nimegundua

kumbe wizi siyo peke yake tu, yaani hapa tunapokwenda kunadalili ya mauaji ya Watanzania wasio na hatia. Hivi kama vituo vya afya na zahanati 16 na kama hospitali za mkoa na hospitali za rufaa 17 zinakuwa na madawa yaliyoisha muda wake zaidi ya miezi mitatu mpaka miaka kumi ikiwemo Benjamin Mkapa ambapo tunatibia Wabunge.

Mheshimiwa Spika, dawa zimeisha muda wake zenye thamani ya shilingi bilioni 3.5 zimeisha muda wake, sasa hapa tunasema nini, tunazungumza kupata nini? Yaani leo Tanzania ambayo tuna wasomi, tuna mifumo ambayo inaangalia *expire date* iko wapi kwneye dawa, leo tuna dawa, vituo vya afya, zahanati, bohari kuu zimeisha muda wake na zipo. *CAG* anasema miezi mitatu mpaka miaka kumi, zipo.

Mheshimiwa Spika, hiyo ni dalili moja wapo ya kwamba huko tunakokwenda tutaua Watanzania wasio na hatia na wataalam tunao. Mimi nafikiri kwamba nalo hilo tuliangalie maazimio haya tunampa nani? Lazima tukubali sasa kwamba Bunge lijalo kama kuna Ripoti ya *CAG* tupate kwanza maazimio yetu tuliyoyaweka Bunge hili kama yametekelezwa, kama hayakutekelezwa hakuna haja ya kujadili, tunajadili nini sasa. Nafikiri kwamba tuangalie kwamba inakuwaje.

Mheshimiwa Spika, nimeangalia kitu kinaitwa *GPSA,* taasisi mbalimbali zimeagiza magari shilingi bilioni 35 *point,* mpaka ripoti hii inatengenezwa hayajaja, labda sasa sijui kama tutajibiwa au itakuwa muda mwingine. Shilingi bilioni 35 magari yameagizwa hayaji, watu wanadai magari, hayaji, hela zimetolewa. Sasa tunamwambia nani? Tuunde Kamati ya kufuatilia maazimio hayo ili tuweze kuwa na uhakika wa jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kuna mikataba yaani tunaajiri wakandarasi, tunatengeneza mikataba, tuna wanasheria na tuna kila kitu, riba shilingi bilioni 418; yaani tunalipa watu hewa, mtu umemtengenezea mikataba riba shilingi bilioni 418, ukigawa kwa shilingi 500 kituo cha afya ni vituo karibu 387. Tunagawa, yaani unawapa watu bure tu, shilingi bilioni 418. Watoto wanakaa chini,

hali ni mbaya zahanati hazijafikia, tunagawa. Kwa hiyo, nafikiri kwamba tuunde kamati ya ufuatiliaji wa jamnbo hili.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, Wabunge wamesema mambo mengi hapa ukisema ni kumalizia tu, mambo mengi yamezungumzwa humu ndani. Amezungumza mtu mmoja hapa jana Mbunge na Wabunge wengi wamesema hili Bunge letu sasa linatazamwa, lina Spika wa Mabunge ya Dunia. Kwa hiyo, sasa lazima tuangalie na nimekusikia kwenye kauli yako wakati unahitimisha baada ya kupata zilke kura nyingi ukasema kwambva *IPU* fedha zao mali yao itakaa salama. Naomba sasa usalama wa Watanzania wa mali za umma ukae salama kwenye Bunge hili waanzie hapa. Nikuombe waanzie hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Mkurugenzi hivi tukizungumza hapa tunamzungumza Rais, hivi Rais amemteua Mkuu wa Mkoa amemteua Mkurugenzi kwenda kuiba?

**MJUMBE FULANI:** Hapana.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, Rais amemteua Mkurugenzi kwenda kuiba? Tunamsaidia Rais wezi wote walioiba huko dani tuwatoe. Siku moja niliwahi kusema hapa na narudia…*(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere malizia sekunde 30 muda wako umeshaisha.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, niliwahi kusema hapa, nikibahatika kupata Uwaziri au Unaibu Waziri baada ya siku tano mtakuwa mmenifukuza, kwa sababu ziara yoyote nitakayoenda kila nitakaemkuta ameharibu ni *lock up, lock up, lock up,* nikirudi mtasema nimekiuka demokrasia, mtanifukuza kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, maombi ya wachangiaji yako mengi hapa na jambo hili ni zito kwa kweli. Siyo jambo ambalo unaweza kupunguzia watu muda kirahisi, lakini sasa pia lazima twende na uhalisia wa tutaweza kukaa hapa muda gani.

Kwa hiyo, kwa idadi ya majina niliyo nayo hapa mbele ya walioomba kuchangia tukubaliane pamoja na kwamba tutatumia siku nzima leo kukaa hapa ndani, lakini tutaweza kumudu muda vizuri ikiwa kila mmoja wetu atatumia dakika nane badala ya dakika kumi. Kwa hiyo, wachangiaji wataanza kuchangia dakika nane badala ya kumi na kengele zitagonga mbili kama ilivyo ada.

Mheshimiwa Cecil Mwambe atafuatiwa na Mheshimiwa Eric Shigongo, Mheshimiwa Jesca Msambatavangu ajiandae.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi asubuhi hii, lakini nikupongeze kama alivyotangulia kusema ndugu yangu hapa Mheshimiwa Getere kwamba nafasi uliyonayo ni kubwa sana na naamini dunia inafuatilia Bunge letu la Tanzania na nikuombe sana utengeneze historia kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utatutendea haki sana endapo utaelekeza sasa sisi kama Wabunge tukae na kupitia maazimio yote yaliyotolewa na Bunge kwenye Ripoti za *CAG* kwa miaka mitatu nyuma ili wote waliohusika wawajibishwe ndani ya Bunge letu, kwa sababu hiki ndicho wanachokisubiri wananchi huko nje kuona sisi tumefanya nini.

Mheshimiwa Spika, ukifuatilia kwenye mitandao binafsi unapongezwa sana na Wabunge wengi wanaochangia wanapongezwa sana. Ndugu zetu Mawaziri kwa namna fulani wanalaumiwa na wanakuwa *less popular* maeneo mengi hasa zaidi wanapotaka kutoa taarifa za kuwa-*distract* watu kwenye mjadala mzito kama huu unaohusu Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nikuombe pamoja na kwamba kanuni zinaruhusu kufanya hayo mambo Waheshimiwa Mawaziri

mtuache tuishauri Serikali, lakini pia tujaribu kuielekeza kwa sababu naamini Bunge hili linafuatiliwa wapi kwenye matobo kwenye maeneo sisi tunakotokea kwa maana ya lutaka kulisaidia taifa letu. Kwa hiyo, mtuache tufanye kazi yetu ya kuishauri Serikali, lakini na kuwashauri na ninyi ili mkachukue hatua mtakaporudi kwenye ofisi zenu.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wengi wameongea na kama ulivyosema hapo kwamba hata muda wenyewe sasa tunapunguza kwa sababu tunaelekea kwenye kuhitimisha. Nimekuja hapa kwa ajili ya kutoa ushauri.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu wa kwanza kuhusu kubadilisha kanuni ili Ripoti ya *CAG* inapokuja mwezi Machi ikiwezekana Wabunge tukubaliane tuendelee kuijadili kwa kubadilisha kanuni zetu ili tunapokwenda mwezi Julai kwenda kufanya *allocation* za pesa nyingine kwa ajili ya bajeti inayofuata na haya tuwe tumepata majibu yake, kwa maana ya kwamba taarifa hii tuwe tumeijadili. Kwa hiyo, tuone namna ya kubadilisha kanuni kwenye hilo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine Mheshimiwa Simbachawene jana alijibu kwamba sisi Wabunge ni sehemu ya Kamati za Fedha kwenye Halmashauri zetu. Hakuna Mbunge hapa ambaye hafahamu kwamba ratiba zinatofautiana sana. Sisi tuko hapa Bungeni tunajadili masuala haya, lakini na huko kwenye Halmashauri zetu vikao vya Halmashauri vinaendelea, Kamati za Fedha zinakaa, Mabaraza yanakaa. Kwa hiyo, tuone namna ya kubadilisha kanuni ili tuweze kuhudhuria kwenye hivi vikao na tuweze kuzishauri Halmashauri zetu vizuri namna ya matumizi bora ya hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumejadiliwa hapa suala la Mfuko wa Usalama wa Raia *SACCOS* na kwamba taarifa zimekuja kuna upotevu. Mheshimiwa Bulaya jana hapa alisema vizuri tuombe basi kama kweli tuna nia ya kutaka kuwawajibisha hawa watu na Mheshimiwa Naibu Waziri jana alijibu kwamba kuna watu wako mahakamani. Nataka nimkumbushe amemsahau Mheshimiwa Afande Sirro ambaye alikuwa *IGP* wakati haya mengine

yanatokea basi wafanye utaratibu wamrudishe ili naye aunganishwe na hawa watu walioko mahakamani kwa sababu ametwambia kwamba hili jambo liko mahakamani. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, tukaangalie pia na suala la Mfuko huu wa Kufa na Kuzikana lakini tukaangalie na *SACCOS*…

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe kuna tarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nampa taarifa, siyo Sirro peke yake, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili ametajwa kwenye taarifa baada ya taarifa akapata uteuzi wa Naibu Katibu wa Maliasili na Utalii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Cecil Mwambe unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Spika, naipokea hiyo taarifa nadhani namuongezea Mheshimwa Waziri hapa wigo mpana wa kutimiza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, pia kuna suala la Mfuko huu wa *Usalama wa Raia SACCOS,* askari wetu wamekuwa na malalamiko makubwa sana, Mheshimiwa Waziri yuko hapa kwamba kila mara wanakatwa, hawapati taarifa zinazohusiana na makato yao, lakini hata hivyo kunakuwa na marejesho ama faida inayopatikana hawajawahi kushirikishwa.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni mishahara imeogezwa, ukiangalia kiasi cha mshahara kilichoongezwa na makato waliyoongezewa polisi kwenye huu mfuko wao havifanani. Kwa hiyo, niwaombe nao wakajaribu kujadiliana na wakubwa wa polisi kwa sababu askari hawa wadogo wanakatwa pesa hizi, lakini wao wanaamini kwa sababu ya utii wanaotakiwa kuwa nao

mambo mengine wanashindwa kuyapinga, wanayaleta kwetu sisi kama Wabunge tuseme hapa yasikike ili wakubwa waone namna ya ku-*review* kwenye haya mambo.

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine lakini hili pia ni ombi na nimemuona hapa rafiki yangu Bwana Ndejembi kwamba tumesoma hizi taarifa zote, tumesikia madudu mengi yanayofanyika kwenye halmashauri zetu. Mimi niko hapa kuomba ukaguzi maalum kwa ajili ya Halmashauri ya *Masasi DC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mchungahela hapa jana wakati anasema, wakati anamalizia kwenye dakika ya tisa alitoa maelekezo kwamba hata kwenye Halmashauri yetu kuna ubadhirifu. Nataka nikuongezee, maeneo ambayo natamani kabisa mkayakague la kwanza kabisa ni eneo ambalo Mheshimiwa Rais alitoa pesa kwa ajili ya madawati, eneo hili halijafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ujenzi wa sekondari Shule ya Mpeta, ujenzi ule umekuwa unalalamikiwa sana, lakini pia kuna ujenzi wa ghala letu la Halmashauri ya Wilaya ya *Masasi DC,* ujenzi huu umekuwa unalalamikiwa sana. Pia tunayo hospitali yetu Mheshimiwa Rais alitoa pesa nyingi za kwenda kukamilisha Hospitali ya Tarafa ya Chikundi, sasa hivi ni karibu mwaka wa pili, tunaelekea mwaka wa tatu pesa zimekwisha, ujenzi wake haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tunalo jengo letu ya *Masasi DC* ambalo Mheshimiwa Rais alikwenda kulifungua hili jengo mwezi mmoja miezi miwili iliyopita wakatoi wa ziara yake. Wakati Rais anakwenda nataka nikuchekeshe kitu kimoja hapa, palifanyika utaratibu wa kuondoa simenti kwenye Shule ya Sekondari ya Kata ya Chikunja ili kwenda kufanya marekebisho kwenye hili jengo Rais atakapopita aone pale mambo ni safi, naomba mambo yote haya yakakaguliwe na tupate taarifa maalum.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo lingine limejitokeza karibuni pesa za likizo za walimu zaidi ya 120 wa Halmashauri ya Wilaya ya *Masasi DC* nazo zimetumika kwenye matumizi tofauti, walimu

hawa hawajalipwa wameshindwa kwenda likizo. Kwa hiyo, nimeombwa na walimu na ili lenyewe nililete hapa niliseme.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nimesema kwamba mjadala huu umekuwepo hapa kwa siku tatu na sisi tunatokea maeneo hayo, na nakumbuka Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa aje kufanya ziara kwenye Wilaya yetu ya *Masasi DC,* tulitamani haya mambo yote tumuoneshe tumwambie kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu kuna haya mambo yanayotokea kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo bado niikumbushe Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba sasa waratibu hiyo ziara ya kuja Halmashauri ya *Masasi DC,* lakini kabla ya hapo ninyi kama watu wa TAMISEMI nendeni mkaangalie haya maeneo niliyowaambia kwa sababu tuna Mkurugenzi mpya, tunae pale *DC* wetu mpya ambaye ameripoti hivi karibuni, lakini wao wamerithi mambo ambayo wao hawawezi kuyamaliza pale, wameyakuta haya madudu.

Mheshimiwa Spika, pia niishauri Serikali kama inawezekana kila tunapopeleka Mkurugenzi mpya, Mkuu wa Wilaya kwenye maeneo haya ikafanyike kwanza *special audit* ili wakabidhiwe halmashauri ikiwa *clear.*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunapokaa muda mrefu na hizi taarifa kwa mfano Taarifa ya *CAG* tunaijadili leo hapa baada ya *LAAC* kwenda kufanya huko ukaguzi na vitu vingine, kimsingi tumebakisha taarifa mbili, maamuzi ya taarifa zetu tatu za huko nyuma hatujafanyia kazi. Walau sisi tuna historia tulipoingia Bunge la mwaka 2020 lakini tayari haya mambo tulishajadili kati ya 2015 mpaka 2020 tutawaachia kiporo Bunge lijalo kwa sababu tunaacha hivi vitu ambavyo sisi tumeviharibu, tumeshindwa kuviweka sawa sawa tunacha kwa ajili ya Bunge lijalo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo niombe taarifa hizi za *CAG* zikija mwezi Machi tuzijadili kwa sababu kama hapa anatuambia tunapunguza muda wa majadiliano. Taarifa ambayo imekaa miezi sita/saba na sisi leo tunaijadili kwa dakika nane kwa dakika

kumi, kwa dakika 15 tunajadili kwa siku tatu kuna mambo mengi ambayo kimsingi tunahitaji kuyachambua.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nisisitize bado tuombe kubadilisha kanuni ili ikiwezekana taarifa hizi zije mapema tuzijadili kwa ajili ya kusaidia Taifa letu, kwa ajili ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipatia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Abdallah Chikota na Mheshimiwa Jafari Chege, Mheshimiwa Michael Mwakamo ajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mezani kwetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kuwapongeza wenyeviti wa Kamati zetu hizi tatu za *PAC, LAAC* na *PIC* kwa taarifa zao nzuri ambazo wamewasilisha, lakini pia niwapongeze Wajumbe kwa uchambuzi ambao wameufanya kuhusu Ripoti ya *CAG*. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa kutupa taarifa ambazo ni za bayana ya nini kinachoendelea katika Wizara zetu, Serikali za Mitaa na Idara ambazo zinajitegemea, ni ripoti ambayo haina mashaka na uzalendo wa *CAG* tunaufahamu, kwa hiyo hongera sana Ofisi ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda mimi nitajikita sana kwenye Taarifa ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* na niendelee kuipongeza taarifa hii kwamba ni taarifa ambayo imeandaliwa vizuri. Imeonesha madhaifu mengi kwenye makusanyo ya mapato ya ndani, imeonesha udhaifu katika udhibiti wa ndani, imeonesha udhaifu katika mfumo wa usimamizi, lakini imeonesha udhaifu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani ambacho kingekuwa imara kingekuwa kinawasaidia Mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini pia imeonesha udhaifu wa Sekretarieti za Mikoa katika kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, taarifa hii iko vizuri na sipendi kwenda kwenye takwimu kwa sababu ukisoma taarifa yao kila kurasa wametoa maelezo na takwimu za fedha ambazo zimepotea na hasara ambayo Serikali imeipata.

Mheshimiwa Spika, ningejielekeza kwenye nini tukifanye na hasa kwenye ku…, kwa sababu ukiiangalia hii taarifa kuna mambo kama matatu hivi; kwanza kuna suala la sheria zinazoongoza Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuna miongozo yetu, lakini kuna muundo. Mimi nitajikita hapo ili pengine tuweze kurekebisha kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia kwenye sheria zetu ambazo zinaongoza Mamlaka za Serikali za Mitaa zimetungwa muda mrefu sana, ni muda sasa wa kufanya mapitio au tujiulize je, zinafaa kuendelea hadi sasa? Kuna mjumbe mmoja pale kaka yangu Mheshimiwa Mwambe amesema kwamba sisi ni sehemu ya Madiwani na tunahusika na ubadhirifu unaotokea. Ndugu zangu kwa mifumo iliyopo sasa hivi na miongozo iliyopo sasa hivi hata Madiwani wenyewe hawafahamu kinachoendelea kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi nani anamsaidia Diwani kuifahamu Taarifa ya *CAG,* nani anamsaidia Diwani kujua *final account* za halmashauri? Menejimenti inaamua nini ipeleke kwenye Baraza na nini isipeleke, lakini je, hivi kweli inawezekana taarifa za sekta kama kumi hivi Madiwani wakutane siku moja tu kwenye Baraza wazungumzie elimu, wazungumzie afya, wazungumzie maji na wazungumzie nini. Hii mifumo kwa kweli sasa hivi haituwezeshi.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile ukisoma ile Sheria ya Tawala za Mikoa, Katibu Tawala wa Mkoa siyo mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wa halmashauri, yeye ni mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wa *RS*. *RAS* akienda kwenye Halmashauri pale hata kama atapiga kelele Wakuu wa Idara wataulizana kwani huyu mmemjazia mafuta aondoke zake, kwa sababu hawezi kufanya chochote. Atapiga kelele zake atafanya hivi, anaondoka zake. Mamlaka ya nidhamu ya *RAS* ni kwa watumishi wa *RS* tu, lakini wale wa Mamlaka za Serikali za Mitaa siyo wa kwake.

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna suala hili la ugatuaji, tuna Sera yetu ya Ugatuaji ya mwaka 1998; je, hiyo ni *valid* mpaka sasa hivi? Kuna malalamiko yapo kwamba TAMISEMI sasa kumekuwa *congested*.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko yapo sasa hivi kwamba kwa mfano Katibu Mkuu Uvuvi akitaka kuandika barua kupeleka kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa ni mpaka ipitie kwa Katibu Mkuu, TAMISEMI. Ina maana kwamba tuna *Chief Secretary* mwingine sasa mdogo, kwamba hatuwezi kupeleka taarifa huko mpaka zipitie TAMISEMI, lakini je, kuna *coordination* gani kati ya TAMISEMI na hizi Wizara za kisekta?

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu Mheshimiwa Rais amekuja na *4R* hii *R* ya *reform* lazima tufanye *reform* kubwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tufanye *reform* kwenye *Regional Secretariat, RC, RAS* wawe na nguvu kwenye usimamizi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ikibaki hivi hivi tutaendelea kama *business as usual* na ndiyo maana Mawaziri mnapata shida sana, viongozi wetu wa Kitaifa wanapata shida sana, wanapofika mikoani wanashughulikia *isuue* ambazo zingefanywa na ma-*DC* na ma-*RC*. Naomba tufanye mabadiliko ya hizi sheria. Hizi sheria siyo *bible* siyo msahafu, tuzibadilishe sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile naomba sasa kwenye mabadiliko haya tuangalie nafasi za Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa, isiwe mtu akiteuliwa basi ndiyo huyo Mkurugenzi, Wakurugenzi hawa tuwape mikataba sasa na kuwe na *KPI* za kuwapima, akimaliza muda wake kama ha-*perform* basi aondoke, lakini Mkurugenzi akishateuliwa anaona ameula, Akiharibu Kiteto anakuja Nanyamba, akitoka Nanyamba anakwenda Nanyumbu anabadilisha badilisha tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo lazima ifike mahali sasa tena mimi Mheshimiwa Mchengerwa nakutegemea sana. Wewe ulipoingia TAMISEMI tuna matumaini makubwa sana. Ni mtu wa kuthubutu, hebu kafukunyue hivi vitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka za Serikali za Mitaa sheria nyingine zimetungwa wakati wa Baba wa Taifa tuzibadilishe sasa hivi. Mchengerwa unaweza na timu yako, kafanye mabadiliko ili tuwe na *strong RS*. Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala, akifika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa haonekani kuwa ni mtu ambaye anaweza kuchukua hatua, lakini anafika pale anapiga maneno kwamba hizo ni kawaida zao. Ni kama mnavyowaambia Mawaziri mmeapa mkienda kwenye Wizara, watumishi wanasema kwamba huyu ni Waziri wa nane mimi huyu, mwenzake alikuja hapa na ukali huu huu, lakini alitulia. Kwa hiyo, twendeni tukafanye hayo mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tuangalie nafasi za wenye viti na *mayor* wa Halmashauri. Hivi kwa mtindo wa sasa hawa kweli wana uwezo wa kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa? Nani anamsaidia Mwenyekiti wa Halmashauri kuifahamu vizuri Halmashauri yake kwa sababu Mkurugenzi anamficha taarifa muhimu Mwenyekiti wa Halmashauri ili asimsumbue kwenye vikao, anapata wapi zile taarifa? Anapata wapi usaidizi na anakwenda siku mbili tu kwa wiki? Tena siku nyingine anaambiwa leo hakuna gari tutakutumia posho yako huko huko ulipo anasema sawa, basi hafiki Halmashauri. Kwa hiyo, naomba tufanye mabadiliko kama hayo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, vilevile…

**SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Jafari Chege atafuatiwa na Mheshimiwa Michael Mwakamo, Mheshimiwa George Mwenisongole ajiandae.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi

ya kusimama ndani ya Bunge na mimi kutoa maoni yangu juu ya Taarifa tatu za Kamati zilizowasilishwa katika Bunge lako hili.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kudumisha utulivu, amani lakini pia kwa kujituma na kuhakikisha tunapata fedha za miradi ya maeneleo zinakuja kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kwa maana ya *CAG* pamoja na ofisi yake kwa uzalendo wake mkuu na namna ambavyo anawajibika kuhakikisha angalau anadumisha na kurudisha uzalendo na uimara katika fedha za Serikali kwenye miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tunakubaliana kwamba Ofisi ya *CAG* kama Mdhibiti wa Hesabu za Serikali ametimiza wajibu wake. Mbele yetu sisi tunao mtego, sisi kama Bunge la watunga sheria ambao kimsingi yanayokwenda kukaguliwa na *CAG* na yanayotekelezwa na watumishi mbalimbali yanaendana na sheria mbalimbali ambazo zimetungwa ndani ya Bunge hili na sisi ndiyo watungaji wa sheria hizi.

Mheshimiwa Spika, mtego ulioko mbele yetu ni pale ambapo taarifa hizi zinakuja na baadhi yetu wataalam na watumishi mbalimbali wamekiuka sheria na taratibu mbalimbali ambazo zinatungwa ndani ya Bunge na sisi kama Wabunge tunaingia mjadala wa kuweza kuzijadili.

Mheshimiwa Spika, kwa kuendelea kutoa maoni ya Taarifa ya *CAG* ningetamani tutakapopata nafasi ya Waheshimiwa Mawaziri mimi ningependa sana nitoe ushauri, watakaposimama kwanza tupitie mapendekezo ya Bunge hili ya Taarifa ya *CAG* ya miaka miwili au mitatu iliyopita kabla hatujaanza kupitia mapendekezo ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa kufanya vile tutakuwa moja; tunadhibiti na kuimarisha maelekezo ya Bunge hili kwamba Bunge linapotoa mapendekezo ya kwenda kufanyiwa kazi basi uimara wa taarifa huo uweze kufanyika. Kwa mfano, wakati tunajadili mwaka jana Taarifa ya *CAG* ilionekana kwenye fedha za mikopo peke yake, mikopo ya vijana, wanawake na walemavu, taarifa ya mwaka jana kwa maana ya 2020/2021 zaidi ya shilingi bilioni 47 zilikuwa zimekwenda mahali ambapo kuna utata hazieleweki. Mwaka huu Taarifa ya *CAG* inazungumza zaidi ya shilingi bilioni 88 kwa maana hiyo zimeongezeka zaidi ya mara mbili na kwenyewe matumizi yake hayaeleweki.

Mheshimiwa Spika, kwenda kujadili shilingi bilioni 88 peke yake tukaacha kupata maelekezo ya Serikali na Wizara husika hatua walizochukua kwa Wakurugenzi, Maafisa Maendeleo na Wakuu wa Idara mbalimbali waliosababisha hasara ya shilingi bilioni 47 tunakoenda kujadili shilingi bilioni 88 maana yake tunaacha kiporo huku nyuma na inawezekana mwakani tukarudi tena kujadili zaidi ya shilingi bilioni 88. Kwa hiyo, uendelevu huu ni lazima tuhakikishe kwamba sisi tunausimamia.

Mheshimiwa Spika, la pili, kwenye Bunge hili tumetunga Sheria kwamba mwananchi akinunua chochote, akihitaji mahitaji yoyote au bidhaa yoyote ni lazima aombe risiti. Sheria hiyo tumekwenda kutengeneza Kanuni kwamba asipoomba risiti mwananchi mnyonge wa kule kijijini anatakiwa kulipa shilingi milioni tatu kwa ile risiti ambayo hakuomba. Hili limekuwa likifanywa na *TRA* na wenzetu na linasimamiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, sasa tujiulize sisi Serikali imefanya malipo ya zaidi ya shilingi bilioni 10 na hawajaomba risiti ya eletroniki, lakini wamelipa fedha. Sasa tunataka tujue nani anayewajibika hapa na ndiyo maana ninasema Waheshimiwa Mawaziri sisi inawezekana hatuna ubaya na ninyi tunataka tujue mtakavyokuwa mnatoa majibu hasa Waziri husika. Wakurugenzi wa hizi Halmashauri wote waliotoa risiti ambao kimsingi mmeshindwa kuwaomba ile shilingi milioni tatu ambayo mwananchi wa kawaida anatoa. Ukisimama kutoa majibu…*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi jana Mawaziri walikuwa wanatoa taarifa sana kwa Waheshimiwa Wabunge, naomba na sisi uturuhusu leo Waziri atakapokuwa anatoa majibu ambayo hayaridhishi kwenye kipengele ambacho tunahitaji majibu tupe nafasi tumpige taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningetamani Waziri husika aniambie Wakurugenzi waliolipa fedha hizi bila risiti za elektroniki wako wapi na asiniambie wahewahamisha kutoka kituo "A" kwenda kituo "B." Nataka aseme hadharani wamefukuzwa, wako kwa mujibu wa sheria mahakamani au wako wapi. Ukiniambia umewatoa sehemu "A" kwenda sehemu "B" nitaomba unipe nafasi ya kum-*correct* Mheshimiwa Waziri huyo ili angalau twende sawasawa. Kwa kufanya hivyo tutakuwa angalau tunakwenda kama vile inavyotakiwa.

Mheshimiwa Spika, la pili, Mheshimiwa Waziri husika atakaposimama leo atuambie leo ndani ya Bunge fedha ya *POS* ambayo imekusanywa shilingi bilioni 11 hazikupelekwa benki, hizi fedha hawa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wamezipeleka wapi? Aseme yeye yaani natamani jibu liwepo kwamba hawa Wakurugenzi wa hizi Halmashauri waliosababisha upotevu wa fedha hizi leo watatu wako mahakamani, wanne wako sehemu fulani na usiniambie umewahamisha kutoka sehemu "A" kwenda sehemu "B."

Mheshimiwa Spika, inauma sana na naamini wote tutakubaliana, ni sawa na mtu una duka lako umemuweka kijana asimamie mauzo ya duka lako, halafu yule kijana anakuibia fedha ya kwako wewe mfukoni. Anachokiuza anakipeleka mfukoni hapeleki benki wala hakupi wewe eti kwa kujifurahisha na kuchukua hatua unamhamisha kutoka kwenye duka "A" unampeleka kwenye duka "B" halafu unapiga makofi kwa kujipongeza kwamba nimechukua hatua zinazostahili, hii si sawa.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba kama wewe una uchungu na yule kijana aliyekuibia fedha yako maana yake utachukua hatua stahiki. Tunataka tuone Waheshimiwa Mawaziri

mtakapokuwa mmesimama kutoa taarifa hapa mtuambie hawa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara mmechukua hatua gani za kinidhamu? Hili nadhani litaongeza umaarufu.

Mheshimiwa Spika, pia natamani nitoe ushauri kwa Mheshimiwa Waziri na kwa Serikali kwa ujumla wake. Haya yote yanafanyika kwa sababu ya sheria zilizopo, Sheria ya Utumishi wa Umma, sheria mbalimbali za usimamizi wa manunuzi na sheria zote zinazoendesha miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aone namna ya kurekebisha hizi sheria. Kwa mfano, leo kijana analipwa mshahara wa shilingi 800,000 mpaka shilingi 1,000,000, afisa wa kawaida. Shilingi milioni moja au laki nane kwa mwezi kwa mwaka maana yake anachukua milioni kumi huyu kijana. Kwa miaka mitano ukizidisha shilingi milioni kumi maana yake ana shilingi milioni hamsini peke yake, kwa miaka kumi ndiyo ana shilingi milioni 100. Amekutana na *deal* la shilingi bilioni mbili mezani kwake ambayo akifanya kazi ya utumishi wa umma kwa zaidi ya miaka 30 hata 50 mpaka anastaafu hawezi kupata ile shilingi bilioni mbili maana yake atakupiga shilingi bilioni mbili na akikupiga shilingi bilioni mbili anajua sheria yenyewe iko *weak*. Kwa sababu sheria yenyewe ni kwamba utamsimamisha, utamchukua utampeleka TAKUKURU, utampa barua ya kujieleza, ndivyo zinavyozungumza maana yake huyu hawezi kuogopa kuiba fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nikaishauri Serikali ifanye mabadiliko ya sheria na ndiyo maana jana tulisema hapa ikibidi iseme mtu wa aina hii kama siyo kunyongwa basi itamke kitu ambacho kinaweza kikafanya watu wote wakaweza kuogopa kuchezea fedha za umma.

Mheshimiwa Spika, lingine ni TAKUKURU; nataka nijue ni chombo gani kinachowasomamia TAKUKURU? Leo Mkuu wa Wilaya akienda kukagua miradi akikuta kuna ubadhirifu utasikia anasema hili liende TAKUKURU. Mkuu wa Mkoa hivyo hivyo akija Waziri hivyo hivyo, akija Waziri Mkuu hivyo hivyo; najiuliza TAKUKURU ukiacha haya ambayo yametajwa humu kwenye

Taarifa ya *CAG* haya ambayo yanatolewa matamko na viongozi wa kisiasa na viongozi wa Serikali TAKUKURU anayo mangapi?

Mheshimiwa Spika, nani anaki-*regulate* kile chombo kuhakikisha haya maelekezo, hizi kesi mbalimbali TAKUKURU anazipeleka mahakamani na zinafanyiwa kazi? Nani anaye-*regulate*? Ndiyo maana ukiangalia hii Taarifa ya Kamati wanasema TAKUKURU ni kichaka cha taarifa mbalimbali kwa sababu hakuna chombo na kama kipo maana yake kimeshindwa kusimamia TAKUKURU kuhakikisha kesi mbalimbali zinakwenda mahakamani.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana tunashauri kiwepo chombo maalum ambacho kinafuatilia kesi mbalimbali zote na matamko ya wanasiasa ambayo TAKUKURU wanapewa jukumu lake ili angalau kila mwezi kwa miezi mitatu tupate taarifa kwamba wanachukua hatua gani juu ya utekelezaji wake.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jafari Chege kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa kwamba baada ya Wilaya ya Bunda kupokea kesi zaidi ya 40 za TAKUKURU nilipoenda kwa TAKUKURU Wilaya akasema yeye hana uwezo wa kupeleka hao watu mahakamani mpaka apate idhini ya TAKUKURU Mkoa, kwa hiyo ni *process*. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jafari Chege unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ndiyo maana nikashauri kwamba kiwepo chombo ambacho kinawa-*regulate*, kinawa-*control* hawa watu. Kwa sababu TAKUKURU ukiacha kesi ambazo zimetajwa kwenye taarifa wewe ni shahidi haiwezi kupita mwezi hujasikia viongozi wa kisiasa au Kiserikali kusema jambo hili, kama imetokea mradi wowote wa wananchi, jambo hili TAKUKURU chukua ukalifanyie kazi. Nani

anayeyafuatilia yale mambo kama yanafanyiwa kazi sawa sawa ili mwishoni angalau Wabunge au Serikali au wananchi wote tupate taarifa sahihi kwamba kesi hizi zinakwenda inavyotakiwa. *(Makofi)*

*(Hapa kenhele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana kengele ya pili ilikuwa imeshagonga.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana. Naunga mkono hoja, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Michael Mwakamo atafuatiwa na Mheshimiwa George Mwenisongole na Mheshimiwa Mwanaisha Ulenge ajiandae.

Mheshimiwa George Mwenisongole? Mheshimiwa Aisha Ulenge? Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka?

Mheshimiwa Jesca Msambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi…

**SPIKA:** Sasa mbona husimami Mheshimiwa?

Haya Mheshimiwa Jesca Mtambatavangu atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Saashisha Mafuwe ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante…

**SPIKA:** Ngoja ngoja, Mheshimiwa Maganga?

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Maganga ajiandae.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia katika ripoti hizi tatu ambazo zimewasilishwa.

Mheshimiwa Spika, mimi na-*declare interest* kwamba ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC*. Nachukua nafasi hii kwa kweli kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya *LAAC*, haya ambayo Waheshimiwa Wabunge ninyi mnakutana nayo sasa hivi sisi kwetu imekuwa ni kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaona uzito wa kazi yetu kwa kweli kama Wajumbe wa *LAAC* na namna ambavyo tunaathirika sana kwenye akili tunapokuwa tukichambua ripoti hizi za *CAG* hasa kwenye suala la Serikali zetu za Mitaa.

Ndugu zangu mimi nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambavyo mmeongelea kwa uchungu na sisi mmetuunga mkono kwenye uchungu wetu na hayo ndiyo ambayo yapo ndani ya nchi yetu na kwa kusema hivyo hatuna maana kwamba pamoja na haya ambayo yapo haina maana kwamba hakuna mazuri yaliyofanyika. Mazuri yapo mengi sana lakini katika hayo mazuri madoa yake makubwa ndiyo haya.

Mheshimiwa Spika, *CAG* ni chombo ambacho sisi wenyewe tumeridhia, tumeweka utaratibu ili kuiendesha nchi yetu, lakini inaonesha kwamba baadhi ya wenzetu wanaona anakuwa kama adui. Hili tunalipata kutokana na namna ambavyo *CAG* akitoa maoni yake yanashughulikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, zipo Halmashauri nyingi sana hazijibu hoja za *CAG*, hoja ambazo zinaelezea ubadhirifu na upotevu wa hivi vitu na rasilimali za nchi katika Taifa letu. Sasa mimi nashindwa kuelewa kama sisi wenyewe tumepitisha na tumekubali kiwe ni chombo ambacho kinaweza kutusimamia, ni kwa nini hatuwezi kusimamiana na kuhakikisha kwamba hoja za *CAG* zinajibiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu cha kwanza ambacho mimi nakiomba, kwanza zile Halmashauri ambazo hazijibu hoja za CAG ndiyo *indicators* za kwanza kwamba haziko tayari kuhakikisha kwamba zinasimamia rasilimali za nchi hii zinatumika kama zilivyopangwa na hiyo iwe ni *indicator* ya kuanza kuwafuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine nilichokiona, mfumo wetu wa uendeshaji, hapa kila mtu analalamika. Mheshimiwa Rais amekabidhiwa hii ripoti analalamika, Wabunge tumekuja tunalalamika na Serikali nayo ikija italalamika, watendaji nao wanalalamika, sasa ni nani atakayekwenda kutatua hili tatizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru, nampongeza Mheshimiwa Jesca kwa mchango wake, lakini naomba niweke sawa mchango wake pale anaposema kwamba Mheshimiwa Rais analalamika, hapana, Rais hajalalamika, kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 34 ama 36 Mheshimiwa Rais amepewa majukumu ya kukasimu madaraka yake kwa watendaji mbalimbali kwenye taasisi.

Mheshimiwa Spika, alichokuwa anakifanya Mheshimiwa Rais ni kujaribu kuwakumbusha watendaji wote wajibu wao wa kusimamia na kuhakikisha kila jambo linakwenda sawasawa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ukimtafsiri Rais kwa kuendelea kuwasimamia watendaji wake na kuwaelekeza kazi zinavyotakiwa kufanywa kule siyo kulalamika. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kumpa taarifa Rais hajawahi kulalamika, anaendelea kutoa maelekezo. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika,…

**SPIKA:** Ngoja Mheshimiwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Msambatavangu unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, sijui niipokee au nisiipokee? Nitabaki *neutral* lakini nataka kusema hivi, wakati Mheshimiwa Rais anakabidhiwa taarifa hii sisi wote ni Watanzania na tulikuwa tuna masikio, tulimsikia akilalamika kutokana na ubadhirifu uliofanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuendelea kujipamba hapa na kujitekenya wenyewe kwamba hakulalamika haisaidii. Kulalamika siyo dhambi, ni kutoridhika na hali inavyokwenda. Sasa sisi Wabunge hapa tunalalamika, Rais analalamika, ninyi Mawaziri ndiyo mnatetea, kwa hiyo ninyi mnakubaliana na huu uovu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watanzania wamelalamika, sisi tunalalamika kwa sababu hatukubaliani na hii hali kwamba hiki kinachoendelea siyo sawa. Kwa hiyo, hakuna aliyepongeza, Rais hakupongeza kwamba hii taarifa iko sawasawa. Sisi tunachowaomba wao waende wakasimamie na mimi naomba tusichekeane, unajua kila mtu Mungu kamuumba kwa ajili ya uwezo wake. Kuna mahali…,kwa mfano naweza nikatoa mfano mdogo hapa kuna mahali tunahitaji daktari mpole wa kumfariji mgonjwa, kuna mahali tunahitaji nesi mkali wa kumpiga mama ili ajifungue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huwezi kuwalaumu manesi wote kwamba wote wanafanya kitu…hapana, kwa sababu watoto hawatazaliwa kama manesi wote wakianza ku-*act* kama wapole fulani hivi kama wachungaji. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lazima tufike mahali tusimamiane, Mheshimiwa *CAG* anaongea hapa *mass dropout* ya watoto, amesema watoto wa shule za msingi karibu 19,000 wameacha shule. Watoto hawa ni kati ya umri wa miaka sita mpaka 13 - 17

wamekwenda wapi? Tuna Wizara inashughulika na watoto, watoto leo ukipita wanavuta shisha, watoto leo ukipita kuna *snacks* zinawekwa bangi watoto wanakula. Serikali ipo mnaona, Waziri Mkuu alisimama hapa akazuia *package* za viroba ili watoto wetu wapone. Leo mmerudisha tena vinywaji vilevile vyenye *package* ndogo watoto wetu wanalewa mitaani, wanakufa tu haya yote *CAG* ameyasema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunakaa hapa tunachekeana mimi nataka niwaambie hivi Taifa hili lina Mungu na nafasi uliyopewa Mungu ameamua uwepo. Ikishindikana sisi humu tunasema halafu hatua hazichukuliwi sisi tunaingia kwenye maombi Mungu atusaidie namna ya kuwa-*overhaul,* hatuwezi kuacha watoto wetu wanangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *CAG* anasema hapa, leo kuna sababu *CAG* ametoa za *mass dropout;* ngoma, watu wanakwenda kwenye ngoma. Mkurugenzi wa Bagamoyo tunamuuliza kwa nini watoto wengi hawaendi shule namna hii anasema ngoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi kweli watu tumekaa ni viongozi…, wewe nikuulize kina mama tupo humu ndani, Wabunge wanawake tupo humu ndani, wewe unaweza kuolewa na miaka 13 ukashika mimba kwa ile *labor pain* ukaenda kujifungua?

Mheshimiwa Spika, leo *CAG* anasema watoto wanapata mimba wakiwa na umei kati ya miaka 13 – 11. Watoto darasa la saba hawamalizi, tuna Wizara ya Elimu, tuna Maendeleo ya Jamii sijui tuna nini, watoto wanapotea hatuoni. Watoto wa sekondari, *mass dropout* sekondari, sisi zaidi ya asilimia 50 watoto wanatoka na *division zero* na *division four* kwenye *public schools.*

Mheshimiwa Spika, tuwashukuru Manispaa ya Moshi; Moshi tulipowauliza kwa nini watoto wanatoroka shule? Mkurugenzi akasema Moshi watoto wengi wametoka kwenye *public schools* wamehamia kwenye *private schools.* Sasa ndiyo tuulizane humu ndani wengine wanatoka kwenye shule za Serikali kwenda kwenye shule za watu binafsi, ni *dropout* hiyo. Lakini wengine

wamekwenda ngoma, ni *dropout* hiyo, lakini wengine wanakwenda masoko ya usiku. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Buhigwe, Kasulu eti kuna watoto wanakwenda masoko ya usiku; mnauza nyama kule, mnauza vitu, mnauza na watoto huko huko. Watoto wanashindwa kusoma, tumekaa hapa kama viongozi tunafanya nini? *(Kicheko)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Sekunde 30 Mheshimiwa malizia mchango wako.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, kitu kingine wafanyakazi; watumishi bado wanadai shilingi bilioni mia moja naa, kweli leo kuna Halmashauri moja ya Pwani watumishi saba wameamua wachange hela wapeleke kwenye Mfuko wa *NSSF* kwa sababu Serikali haikuwachangia ili walipwe mafao yao, wazee wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mbunge wa Kigoma alisema hapa kule mnafanya ni sehemu ya adhabu ni kweli. Kigoma na Nkasi watumishi wanadai mishahara, hawajalipwa mafao yao, tumesema kwa nini? Mkurugenzi anasema mimi nilikuwa bado sijafanya uhakiki. Kuna mtu anaitwa Urassa kutoka Kigoma ni Afisa Uchaguzi anadai shilingi milioni 63, mwingine anadai shilingi milioni 71. Kuna Godigodi anadai shilingi milioni 53 hawa ndiyo mnategemea wakasimamie miradi ya shilingi bilioni mbili, bilioni sita wakati wanawadai fedha zao, *arrears* za mshahara zaidi ya shilingi milioni 19 wataweza wapi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Nicodemas Maganga atafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Ole-Shangai, na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi ajiandae.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante nashukuru kwa kunipa nafasi asubuhi ya leo ili niweze

kuchangia hii Ripoti ya *CAG* pamoja na Kamati zilizowasilishwa juzi hapa upotevu wa mabilioni uliopatikana katika Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge Duniani, Mungu akubariki sana na akuongoze, akupiganie katika utumishi wako, wanawake wenzako uwaonyeshe mfano kwamba wanawake kweli mnaweza, kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kutuchagulia Makonda kuwa Mwenezi wa Chama Cha Mapinduzi. Nampongeza kwa roho ya dhati kabisa, tunamuona Makonda anavyopambana na sisi vijana niseme kwa niaba ya vijana wote Taifa hili tunamuunga mkono Makonda.

Mheshimiwa Spika, Makonda ameanza na Baraza la Mawaziri, ni kwa nini? Ni swali la kujiuliza kama ni mtu mwenye akili timamu. Ni kwa nini ameanza na Baraza la Mawaziri? Kama kweli ni hoja ya Kamati Kuu yote ile ya CCM naipongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kiukweli kila nitakapopata nafasi kusema, nitakuwa nasema ukweli tu. Sitaki siasa za kibabaishaji na bora niache kuchaguliwa ila nimesema ukweli na siku nikifa nitaenda mbinguni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikupe taarifa tu kwamba, mpaka jana tumefika Wabunge 168 ambao tumekubaliana kwa pamoja kabisa tutengeneze mpango tupitishe sheria ya kunyonga watu. Tunaangalia mataifa yaliyoendelea, mengine yanatupa misaada na wanazo hizo sheria, ni kwa nini waliweka hizo sheria, watu ni wagumu, watu hawaelewi kabisa, watu huwezi ukawapeleka mahakamani tu na kulipa pesa hizi ambazo wameshaiba. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, sio maigizo ni suala ambalo limeorodheshwa humu na *CAG*. Wezi wote wanajulikana na mimi ninamuomba Mungu nisije nikaponyoka nikaanza kuwataja kwa sababu wanafahamika wezi waliotuibia kwenye hili Taifa.

Mheshimiwa Spika, isipokuwa ninaomba Mungu anisaidie sana nitumie nafasi yangu ya Ubunge kuishauri Serikali. Wananchi wana kilio kikubwa sana. Wanateseka na michango ya kila aina. Ukifuatilia michango wanayochangisha wananchi unakuta kuna shilingi bilioni 11 ambazo zimepotelea kwenye *POS*. Ninampongeza Mheshimiwa Halima juzi alitusomea hapa kwa wenye weledi mkubwa. Ametaja mpaka na majina ya halmashauri zilizotumika kuiba hizi shilingi bilioni 11. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimsapoti sana Mheshimiwa Simbachawene. Unajua mtu akiongea ukweli wakati mwingine anachukiwa na watu. Jana Mheshimiwa Simbachawene uliongea jambo la ukweli kabisa. Sisi Wabunge kwenye mabaraza ya Madiwani ni wajumbe wa Kamati za Fedha, ninaiomba Serikali hata chama kiwe na muda wa kuwauliza Wabunge kwanza, wewe kwenye halmashauri yako umefanya nini? Kila Mbunge ajieleze hadharani, mpaka upotevu wa fedha unapatikana wewe ulishauri nini kama Mbunge? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ukisoma hii Katiba inajieleza baina kabisa kwamba, Mbunge ni mtu wa aina gani, anatakiwa afanye majukumu gani. Humu tuna hatari, tuna Wabunge wasiojielewa wanasubiria siku ya kuja kulalamika hapa mbele yako. Lakini niwasemee kidogo wale watumishi wanaoisimamia Serikali. Wapo watumishi wengine wana roho ya dhati kuitumikia nchi yao, lakini Serikali Kuu mnawakatisha tamaa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, unakuta mtumishi anafanya kazi halipwi mshahara. Ukiangalia hapa kuna shilingi bilioni zaidi ya 11.998 hii ni malimbikizo watu hawalipwi mshahara mpaka zimefika hizi pesa. Hata kama ni wewe lazima ufikirie, mtu anafanya kazi, mlishakubaliana nae kumlipa mshahara, hammlipi, mnampelekea pesa nyingi za miradi ya maendeleo, hana pesa ya kula nyumbani, matokeo yake afanye nini? Lazima aibe, mimi hapo ndiyo maoni yangu.

Mheshimiwa Spika, shilingi bilioni 11.9 ninaiomba Serikali, kwanza watumishi hawa wana mishahara midogo, ione kila sababu ya kuweza kuwalipa watumishi hawa ili wawe na moyo

ule wa kufanya kazi zao kama walivyopangiwa kwenye mikataba yao.

Mheshimiwa Spika, lakini nizungumzie hili, tuna hawa wazabuni wa ndani, kilio ni kikubwa sana kwa wafanyabiashara. Wamenituma Wafanyabishara kujaribu kuishauri Serikali. Kuna wafanyabiashara wameikopesha Serikali, wengine wamekopesha sementi, wengine mafundi wamefanya kazi kwenye shughuli za Serikali wakiamini kwamba hii Serikali ina pesa, hawalipwi. Niwaombe wasimamizi wote wa Serikali waweze kuwanea huruma hao wazabuni ili waweze kulipwa fedha zao.

Mheshimiwa Spika, nirudie tena kumpongeza Makonda na nimuombe Makonda andelee kuwa na msimamo wa hivyo hivyo, asirudi nyuma na sisi tupo nyuma yake. Tutampa ushirikiano wa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kweli anakuwa akifanya ziara tunamuona, juzi alikuwa Bukoba tulimuona, juzi amefanya kikao kwenye vyombo vya habari tukamuona, anakemea wezi lakini siwapongezi Mawaziri wale ambao wapo *special* kumpongeza Mheshimiwa Rais. Ukiangalia kwenye ndimi zao *special* kumpongeza Mheshimiwa Rais tu. Tukiwauliza wao wamefanya shughuli gani, tukitoa shughuli za Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa lakini sisi wanasiasa huwa tunasema mwisho lakini hoja nyingine zinakuja. Kwenye upande wa mchanga wa ujenzi, Serikali iliweka ushuru wa madini ujenzi. Wananchi wa Mkoa wa Geita wameniomba sana, halmashauri zinazoanzishwa sasa hivi zinashidwa kuendelea kujengwa kwa sababu ya huu ushuru wa madini ujenzi. Serikali iachane na huo ushuru kwa sababu, huo mchanga hauna madini, huo mchanga hauna madini kabisa toka miaka ya nyuma watu walikuwa wakichota bure na matela yao. Kuna wengine walikuwa wana miradi ya matela. Walikuwa wakisomba mchanga wanauza *trip* moja shilingi elfu tano. Wanajipatia fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wameshapaki matoroli yao kwa ajili ya huo ushuru ni mkubwa, unawasababisha wasiendelee na biashara yao ya mchanga. Serikali iondoe huo ushuru ili kusudi mchanga ambao hauna madini watu waweze kuchota bure, waweze kujenga halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, narudia kukushukuru tena wewe kwa sababu nikiendelea kuzungumza mimi kadri hasira zinavyopanda na wezi waliotoajwa humu na *CAG* wanajulikana naogopa nisiharibu mchango wangu. Niwaombe tu Wabunge wenzangu wote wale waliobaki kujiorodhesha kwenye hii sheria tunayotaka kuipitisha ya kunyonga, waorodheshe kama na wao sio majambazi, ila kama ni majambazi wanaogopa wasinyongwe basi wasitupe ushirikiano.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Emmanuel Oleshangai atafuatiwa na Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Mheshimiwa Kunti Majala ajiandae.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia taarifa ambazo zimewasilishwa na Kamati zetu za Kudumu za Bunge kuhusiana na Ripoti ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutumia nafasi hii, kabla sijachangia naomba kuwapa pole wananchi wa Jimbo langu, kaya 30 ambao wametaifishiwa mifugo yao 900 na *TANAPA* wiki hii. Inafadhaisha, yanayotokea sasa hivi hapa, inaonesha kuna watu hawatekelezi majukumu yao vizuri. Kwa sababu, kwa suala hili la hawa wananchi kutaifishiwa mifugo ninaamini kwamba walipelekwa mahakamani wakasema hawana mwenyewe na wala hawana wenyewe.

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia hili suala lilikuwa linajulikana. Kwa hiyo, tutoe tahadhari kwamba Serikali yetu isije ikawa ni sehemu ya kuwafanya wananchi wawe maskini. Kwa sababu,

kutaifisha mifugo 900 kaya 30 maana yake wale wananchi wameshakuwa fukara. Sijui tutawaingiza kwenye mfumo wa *TASAF* au tutafanyaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana nilikuwa ninatafakari kuhusiana na Ripoti ya *CAG*…

**SPIKA:** Mheshimiwa Oleshangai ngoja hili Bunge tulielekeze vizuri kwenye kufanya maamuzi. Jambo hili unalolizungumza sasa ni sehemu ya Taarifa ya *CAG* au ni la kwako kama Mbunge kwa sababu linawagusa wananchi?

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, ni la kwangu kama Mbunge kwa sababu linawagusa wananchi wangu.

**SPIKA:** Sawa, sasa ngoja tuliweke vizuri. Kwa sasa, kwa sababu umesimama kuchangia hoja iliyoko mezani, ikiwa kuna jambo ambalo unataka kulifikisha ili Serikali ilifanyie kazi, inabidi utumie kanuni nyingine ili Taarifa zetu za Bunge zikae vizuri. Kwa sababu, kwenye hoja hii, hoja ni ya Kamati. Kwa hiyo, hata uhitimishaji watakuja kuhitimisha Wenyeviti ambao hawana uwezo wa kulizungumzia hilo. Ili likae vizuri, utakapomaliza mchango wako unaohusu Taarifa ya *CAG* baadaye tukishamaliza hayo tafuta kanuni ambayo itakufanya uliseme hilo jambo la wananchi wako.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru na ninaomba kuendelea kuchangia Ripoti ya *CAG*. Nilikuwa natafakari kuhusiana na yanayotokea. Kwenye taarifa zetu kuhusiana na Ripoti ya *CAG*. *CAG* amepewa majukumu, ukijaribu kusoma ni kwamba anaitwa ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Ninaamini kwamba *CAG* amekuwa akitekeleza jukumu moja la ukaguzi lakini udhibiti imekuwa labda sio sehemu ya kazi zake.

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye Mfuko wa *NHIF* tumekuwa tukilalamika kwamba mfuko hauwezi kusaidia kuhudumia wananchi ambao wanaenda hospitali kwa ajili ya

kutibiwa, cha kushangaza ni kwamba, kuna fedha ambazo watumishi wa *NHIF* wamekopeshana zaidi ya shilingi bilioni 41. Hizi fedha wamekopeshana wakati sheria inawaruhusu kukopeshana kutumia mfuko wa kuzungusha au *revolving funds,* lakini wao wamekuwa wakikopeshana fedha ambazo zinatokana na michango ya wanachama wa *NHIF*.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo ninataka kulichangia kuhusiana na *NHIF*, Waziri wa Afya kila siku hapa amekuwa akisema mfuko wa *NHIF* unakufa. Lazima ufe, kwa sababu, Serikali yenyewe inadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 228 na hamtaki kulipa, Serikali haitaki kulipa fedha hizo kwa mfuko wa *NHIF* kwa ajili ya kuwahudumia wanachama wake na leo hii tumeondoa ile *Toto Afya Card* lakini Serikali ingeweza kulipa fedha nyingine ambazo zingeweza kuwahudumia watoto wa maskini ambao hawapati huduma.

Mheshimiwa Spika, suala lingine. Kuna ununuzi wa vifaa ambavyo vilifanyika kupitia bohari ya dawa. Kuna Kampuni ya Alhandasia ambayo walipewa kandarasi ya kununua vifaa aina 75 kwa shilingi bilioni 3 lakini mpaka kufikia tarehe 30 Oktoba, 2021 kampuni hiyo imeonekana kwamba ni kampuni hewa. Ukiwauliza watu wa bohari ya dawa wanasema tuliwatafuta *online* tukalipa fedha *online* na fedha zikapotea na yule mtu ajulikani alipo.

Mheshimiwa Spika, tunashangaa. Ni mtumishi gani wa Serikali ambaye unaweza ukalipa fedha *online* halafu ukasema huyo mtu hayupo na namba ya *account* baada ya kulipa ikatoweka. *Are we serious?* Kwa sababu, leo unalipa fedha halafu unasema baada ya kulipa, halafu mtu anatoweka. Anajitokeza mtu mwingine anaitwa *EPICO* anasema mimi nitaleta hivyo vifaa pamoja na zile za Alhandasia. Maana yake inawezekana kuna ushirika fulani ambao unatengenezwa halafu baadaye tunasema hatumjui mtu, kumbe huyo *EPICO* ndiyo huyo huyo tena amebadilika jina alikuwa anaitwa Alhandasia sasa hivi anaitwa *EPICO*. Kwa nini sasa yeye akubali kubeba gharama za yule mtu ambaye ametoweka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kila mtu akiweza kutimiza wajibu wake tunaweza ku-*control* haya matatizo yanayotokea. Hivi kweli mtu anasema alitoweka, wewe ulimlipaje mtu kama haumjui. Bahati mbaya au nzuri walimwandikia Balozi wa Misri, Balozi wetu. Akawaambia huyu mtu sisi hatumfahamu, baadaye wao wakaamua kulipa. Halafu hawa watu bado wanatembea mitaani. Huku tunakimbizana na machinga kuwanyanganya shilingi elfu 20 wakati huku tunapoteza shilingi bilioni 5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadaye huyu mwingine anaitwa *EPICO* anajitokeza anasema ataleta hivyo vifaa aongezewe shilingi bilioni 10 ili alete zile za shilingi bilioni 3 lakini sharti lake alipwe shilingi bilioni 10. *Imagine!*

Mheshimiwa Spika, ninaamini kwamba, tuna tatizo ambalo tusipoamua kulitibu kama nchi tutaendelea kuwaumiza Watanzania. Leo tukifikiria shilingi bilioni 3 tutajenga vituo vya afya vingapi? Lakini zimepotea. Nimeangalia ripoti… *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa dakika moja malizia. Kengele ya pili imeshagonga.

**MHE. EMMANUEL L. SHANGAI:** Mheshimiwa Spika, kuna suala lingine la halmashauri zetu, halmashauri zetu kuna tatizo moja kubwa la ukusanyaji wa mapato. Niishauri TAMISEMI, kule chini ukijaribu kuangalia ukusanyaji wa mapato kuna *POS machine* lakini zinapoletwa kwenye Taarifa ya *CAG*, kuna *POS machine* ambazo hazifanyi kazi moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Mheshimwa Waziri itabidi uwaagize Wakurugenzi, zote zipitiwe zile ambazo hazifanyi kazi tuondoe hizo quarries. Mimi nimekuwa Mwenyekiti wa Halmashauri, unakuta kuna *POS Machine,* tumewapa wale watu wa mitaani waingize au wakusannye ushuru. Badala ya kuandika shilingi elfu nane unakuta ameandika shilingi milioni 8. Halafu ndiyo hizo *CAG* anaenda kusema ni fedha ambazo hazijakusanywa. Kuna *POS errors* ambazo watu wanaingiza fedha. Mfano, mbuzi mmoja ni shilingi 2500 lakini unakuta kwenye *POS Machine* mtu anaandika

vibaya, anaandika elfu 25 kufuta hawezi mpaka atoke mtu makao makuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwenye halmashauri zetu kuna vitu vingine ambavyo vinahitaji hekima pamoja na ku-*act* haraka ili tuweze kuondoa hizi *querries* ambazo hazina maana. Kwenye halmashauri zetu, unakuta mtu anataka aandike shilingi elfu 80 anaandika shilingi laki 8. Hawezi kurekebisha mpaka atoke mtu makao makuu. Hiyo kama Serikali tunahitajika kuchukua hatua pamoja na kuwatafuta wataalamu wa kukusanya mapato wengine kule chini.

Mheshimiwa Spika, ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa George Mwaisongole ajiandae.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia ripoti hizi tatu, Ripoti ya *PAC, PIC, LAAC*. Pia, nichukue fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mungu Azza wa Jalla kwa kunijalia siku ya leo kuamka salama na mimi kupata nguvu ya kuchangia ripoti hii ya leo. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Rais *Dkt*. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya.

Mheshimiwa Spika, anafanya kazi kubwa sana kuhakikisha ya kwamba anatutafutia fedha nyingi sana na kuzileta hapa nchini ili ziweze kutekeleza miradi mbalimbali. Ni ukweli usiopingika, mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anapambana usiku na mchana kuhakikisha ya kwamba taifa letu la Tanzania linajenga mahusiano mazuri nje ya nchi lakini pia, linatengeneza fursa ya kupatiwa fedha mbalimbali zinazokuja hapa nchini ili ziweze kutekeleza miradi hii.

Mheshimiwa Spika, nilishuhudia siku moja nikiwa kwenye mkutano mmoja, siku ya walimu duniani. Mheshimiwa Rais alipiga simu akaongea hadharani kuwapongeza walimu siku yao ya walimu Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya hapo alisema yupo safarini anaelekea India na akasema ninaenda India wanangu kwenda kuwatafutia fedha. Ni ukweli usiopingika kwamba Mheshimiwa Rais amekuwa na kasumba ya kusafiri kwenda kutafuta fedha na fedha hizo zinakuja kwenye nchi yetu ya Tanzania. Kazi ya kusafiri kwenye ndege si kazi rahisi. Inawezekana watu wengine wakahisi kusafiri kwenye ndege ni furaha na starehe, kazi ya kusafiri na ndege ni kujitoa muhanga kwa sababu, wakati wowote ule likitokea la kutokea wewe safari yako imeishia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kazi ya kusafiri kwenda kutafuta fedha si kazi rahisi. Hivyo, hatuna budi sisi kama Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kumsaidia kuhakikisha kwamba fedha ambazo anazileta hapa nchini zinaenda kufanya kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, sitaki kurudia, mambo mengi yamezungumzwa hapa. Amezungumza Mheshimiwa Luhaga Mpina juu ya *Lot* namba 3&4 ya reli, wamezungumza hapa habari ya *TANOIL*, wamezungumza hapa habari ya fedha ambazo zimepotea katika ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, mimi niseme, inawezekana chanzo cha upotevu wa fedha, chanzo cha mafisadi kwenye nchi hii ni kizazi ambacho sisi wenyewe tumekiandaa. Mimi ninapenda kuchukua fursa hii kuishauri Serikali. Moja, iweke utaratibu kabla ya vijana wetu na vijana wenzetu kupatiwa ajira, moja kuanzishwe chuo maalumu cha uwajibikaji ili kabla ya watu hawa kwenda kuajiriwa Serikalini wapite kwenye chuo cha uwajibikaji ambacho kitakachowafundisha namna bora ya kwenda kuwajibika kwenye taifa letu hili la Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuwaelekeza wawe wazalendo kwa nchi yao hii ili waweze kutimiza majukumu yao ya kuwasaidia Watanzania. Ninaamini kabisa, kama mpango huu utaanzishwa unaweza ukarekebisha taifa hili la Tanzania kuwa na watumishi ambao wana maadili.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, hapa tunapozunbgumza ninaona Mawaziri hapo wanachati. Mawaziri acheni kuchati, nisikilizeni hapa. Tusikilizeni. Mnanong'ona nini hapo? Lengo sisi hapa tunataka tuwasaidie nyinyi. Tunataka tumsaidie Mheshimiwa Rais fedha hizi zinazotafunwa za wananchi walipa kodi… *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mbunge anachangia tujitahidi kusikilizana, tupunguze sauti tafadhali. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Niseme tu Waheshimiwa Mawaziri mtuheshimu Wabunge, heshimuni Wabunge. Nyinyi mmekuwa tukiwapigia simu, amezungumza Mheshimiwa Maganga hapa, mimi nampinga kwamba Wabunge tunafanya nini?

Mheshimiwa Spika, Wabunge tunatekeleza majukumu yetu huko tunapoona ubadhirifu kwenye maeneo yetu huwa tunawatumia meseji na kuwaeleza Waheshimiwa Mawaziri juu ya mambo yanayoendelea kule lakini hawachukui hatua. Ninao ushahidi hapa kwenye meseji, sitaki kumtaja leo, nimemtumia Waziri kumweleza juu ya fedha ambazo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta kwa ajili ya ujenzi wa shule na shule hiyo haijakamilika.

Mheshimiwa Spika, nimemtumia meseji kumweleza juu ya fedha za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta kwa ajili ya kukamilisha zahanati hazijakamilisha na zimeibiwa fedha lakini hawajajibu na hakuna hatua zozote zile zinazochukuliwa, matokeo yake wanatuchonganisha Mawaziri na watumishi wetu kwenye maeneo yale. Tunapowaambia matatizo ya fedha kuibiwa kwenye maeneo yetu wanarudisha taarifa kwa watendaji wetu wa kule kututengenezea fitina sisi Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, hii haikubaliki, haikubaliki, mtaona ya kwamba labda tunawaonea wivu lakini hatuwaonei wivu, sisi tuko hapa kuwasaidia wananchi, tuko hapa kumsaidia Mheshimiwa Rais.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassim kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jerry Silaa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa rafiki yangu na swaiba wangu Mheshimiwa Iddi Kassim kwamba hoja ya Mheshimiwa George Simbachawene ya jana iliyoungwa mkono leo na Mheshimiwa Maganga ya wajibu wa Waheshimiwa Wabunge kwenye halmashauri zetu ni hoja ya kisheria na kikanuni; kwamba sisi ni wajumbe wa kamati za fedha na uongozi kwenye halmashauri zetu. Kwa hiyo masuala ya usimamizi wa fedha kwenye halmashauri sisi tuna nguvu ya kikanuni ya kusimamia kwenye halmashauri zetu na hatupaswi kutuma meseji kwa Waziri bali kutimiza wajibu wetu kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba kumpa taarifa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jambo analolizungumzia Mheshimiwa Waziri Silaa liliombewa mwongozo hapa na kiti hakijatoa bado mwongozo. Sasa, pamoja na sheria kusema hivyo kama huo ndio uelewa sisi kama Wabunge sina hakika kuna Mbunge atasimama hapa ambaye halmashauri yake haipo kwenye taarifa ya *CAG,* kwa sababu kama sote taarifa zetu mbaya ziko kwenye taarifa ya *CAG* na sisi ni sehemu ya hicho kilichotokea hatuna sababu ya kukaa hapa ndani tukawa tunajadili hii taarifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, natoa huu ufafanuzi kabla ya mwongozo ili tuelewe tunasimama wapi. Huwezi kuwa mwamuzi kwenye kesi inayokuhusu; na kama sisi Wabunge kila mmoja wetu anahusika kwenye halmashauri zetu ambao ndio uhalisia; kama kila mmoja wetu anahusika na ule ubadhirifu iliofanywa kule

hatuna mamlaka sasa hivi ya kukaa hapa ndani kujadili hiyo taarifa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, maana yake tutafute chombo kingine cha kujadili jambo hili na kufanya maamuzi. Kwa hivyo kwenye hili kwa sababu mwongozo uliombwa na haujatolewa tusubiri Mwongozo wa Kiti haya ni maelezo ya awali. Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi malizia mchango wako. *(Makofi/Vigelegele)*

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, lakini pia rafiki yangu Jerry mimi na wewe tunaheshimiana sana. Tulipo hapa tupo kumsaidia Mheshimiwa Rais hatuko hapa kutetea majambazi, hatuko hapa kutetea wizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesema kwamba kianzishwe chombo cha kufundisha uwajibikaji kabla ya watumishi kwenda kupata ajira mpya Serikalini. Ni ukweli usiopingika karne ya sasa mtumishi yeyote yule akiajiriwa leo anataka aanze kuishi maisha kama ya Mo Dewji, anataka aanze kuishi maisha kama ya *GSM* na watu wengine, matokeo yake yanapelekea ubadhirifu mkubwa kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imetajwa hapa moja ya Halmashauri ya Ushetu ambayo ni miongoni mwa Halmashauri inayopatikana kwenye Wilaya ya Kahama. Mimi nimpongeze *CAG* kwa kazi kubwa anayoifanya pia na mimi leo niseme kwamba *CAG* naye tuone namna ya yeye kurekebisha kuanzia ngazi ya mkoa kwenda huko na wao wana changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi halmashauri yangu imetajwa kuwa ni halmashauri iliyopata hati safi lakini mpaka mwenyewe najishangaa wakati mwingine hii hati safi tumeipataje! Yaani mimi mwenyewe najishangaa. Kuna ubadhirifu mkubwa unafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo hii utaona kuna fedha za miradi ya *CSR* iko kule inatafunwa, kuna fedha zinapelekwa kule hazikamilishi miradi. Tumesema kwamba fedha zinakuja ziende zikakamilishe miradi, tumepewa fedha za kujenga shule, shule

hajakamilika mpaka leo, matokeo yake ni nini? Matokeo yake wanaanza kutafuta fedha *(cash)* kwenye mapato ya vyanzo vingine wanaenda kuziba mapengo kwenye fedha ambazo zimeletwa na Mheshimiwa Rais zikamilishe miradi. Miradi haiendelei, fedha ile ambayo ingeenda kutumika kujenga darasa lingine inatumika kuziba mwanya wa wizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niombe sana Mheshimiwa Waziri Mkuu unafanya kazi kubwa mno. Mimi wakati mwingine huwa nakuonea huruma, unazungumza mpaka sauti inakwama, majambazi haya hayakomi. Nikuombe utembelee pia Wilaya ya Kahama uangalie uone ni nini, inawezekana Halmashauri ya Ushetu kupata hati chafu ni kwa sababu kipindi hicho Mkurugenzi hakuwepo, hawa pia huwa na wenyewe…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa

**SPIKA:** Mheshimiwa Iddi Kassim Iddi muda wako umekwisha.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana ninaunga mkono hoja kwa asilimia 100. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kunti Majala atafuatiwa na Mheshimiwa George Mwenisongole, Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ajiandae.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru na mimi kunipatia nafasi ili niweze kutoa mchango wangu wa hizi taarifa zetu za Kamati za Bunge tatu.

Mheshimiwa Spika, pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uhai na tatu niwapongeze Kamati hizi tatu kwa kazi kubwa ambayo wameifanya kwa maslahi mapana ya Taifa letu na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hii ripoti wakati inasomwa mbele ya Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais alikasirika na alichukia sana kitendo hiki cha ubadhirifu ndani ya Taifa letu. Lakini kinachonisikitisha ni Mawaziri wetu ambao ni wasaidizi wa

Mheshimiwa Rais kutetea ubadhirifu ambao umefanyika huko chini kwa watendaji wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuko hapa si kwa maslahi ya mtu mmoja mmoja anayesimama kuchangia hoja hizi, tuko hapa kwa maslahi ya Taifa letu; na hiki tunachokisema Waheshimiwa Wabunge si kwamba tunawachukia Waheshimiwa Mawaziri bali tunataka Waheshimiwa Mawaziri watimize na wao wajibu na majukumu yao ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kwenye nafasi walizonazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hapa leo miradi ya maendeleo huko chini iliyopo asilimia kubwa Watanzania wanachangishwa na kwenda kujitolea nguvu kazi kwenye maeneo yao. Na Wakurugenzi wetu wanapoambiwa kwenda kumalizia kazi zile ama miradi ile ya maendeleo kwenye maeneo yetu Wakurugenzi wamekuwa wakisema hawana fedha za kwenda kumalizia miradi ya maendeleo ambayo wananchi wetu wamejitolea.

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye taarifa ya *CAG* hapa nianze kuzungumzia halmashauri tu kushindwa kukusanya shilingi bilioni 37 kwenye vyanzo ambavyo vipo. Shilingi bilioni 37 halmashauri zimeshindwa kukusanya, Serikali inajua, Mawaziri wenye dhamana mpo na mnajua hamjachukua hatua. Tukisema mnakinga kifua hamtaki tuyaseme haya, mnachotaka tufanye ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halmashauri zinajulikana zimetajwa tangu mwezi wa nne wamesema halmashauri zimeorodheshwa hapa zimeshindwa kukusanya hiyo fedha bado Mkurugenzi yuko ofisini, bado watendaji wako ofisini, wanalipwa mshahara, miradi ya maendeleo Watanzania wajitolee, Watanzania wachange na kodi wamelipa, hiki kitu hakiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ambazo zimeshindwa kukusanya fedha hii, hao wakurugenzi na watumishi waliopo hawafai, wameshindwa kazi, wakapumzike tutafute watumishi na watendaji wengine waweze kwenda kutimiza huu wajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili leo Watanzania vijana wako wengi huko mtaani, wamebeba mabegi yana vyeti wanahangaika kutafuta kazi; ni kwa nini tunaendelea kuwakumbatia watu ambao hawako tayari kufanya kazi ya kuwatumikia Watanzania? Isitoshe Watanzania hawa ambao wanafanya ubadhirifu wamesoma na kodi za Watanzania. Mama zetu huko vijijini ndio wametengeneza pombe, wamelima kwa shida bila pembejeo, bila mbegu bora, bila usimamizi mzuri, mvua za shida, kilimo duni wamelipa kodi hatimaye leo watu wachache ambao wamepewa dhamana na Watanzania wenzao wakasimamie rasilimali zao wanakwenda kufanya haya wanayoyafanya. Kama Taifa hatujitendei haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la Halmashauri kufanya malipo ya shilingi bilioni 11.78 bila viambatanisho, hivi hata haya nayo Waheshimiwa Waziri mnataka nako mkinge kifua? Kanuni na sheria zinaelekeza kila Afisa Masuuli anapolipa chochote ni lazima alipe kwa kutumia viambatanisho aoneshe kalipa kitu gani; hawafanyi hivyo. Shilingi bilioni 11, washikaji wamelamba wametulia wanakula bata na wanasema hata wakipeleka huko wataenda watapiga kelele watatuacha maisha yataendelea; na ndivyo ilivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaletewa taarifa hizi hapa tunazijadili, tukimaliza hakuna hatua yoyote inayochukuliwa; hatujitendei haki na mnavyofanya hivyo hamumkomoi mtu yeyote, tunalikomoa Taifa letu la Tanzania na kizazi chetu kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika malipo au madeni ya watumishi wetu wanaodai. Watanzania wenzetu ambao tumewapa majukumu ya kutusaidia huko chini wanadai shilingi bilioni 119. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninajiuliza, hivi humu ndani leo ni Mbunge gani anayeidai Serikali hata shilingi mia? Nani Mbunge humu ndani asimame anyooshe kidole kwamba mimi naidai Serikali? Lakini hawa watumishi wana madai miaka mitano, miaka kumi, miaka ishirini na ni haki yao hawaombi wamefanya kazi, wanadai stahiki yao miaka na miaka bilioni 119, watumishi wanaofanya

kazi; Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema; mtu huyu unataka awe na morali ya kwenda kufanya kazi? Umempelekea shilingi 2,000 ataenda kuitumia kwenye kazi uliyomtuma? Lazima aichukue.

Mheshimiwa Spika, haya madeni ni ya miaka mingi, Halmashauri ya Chemba kuna watumishi 79 wanaodai madeni yao tangu wakiwa wako Kondoa mpaka leo Halmashauri ya Chemba iko pale hawajalipwa hela zao za likizo, hawajalipwa malimbikizo yao ya mshahara, hawajalipwa hela zao za uhamisho, hawajalipwa madeni mbalimbali, kwa nini hatuwalipi?

Mheshimiwa Spika, hela za kuiba zipo, hela za kulipa watumishi wetu hazipo. Hiki kitu hakiwezekani, hawa watu ni lazima Waziri mwenye dhamana kwa kuwa kuna hela ambazo zinachezewa huko chini tunaomba watumishi wetu wanaodai hizi shilingi bilioni 119 waende wakalipwe fedha hizi.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu Halmashauri zina uwezo wa kulipa ndio maana zinaiba.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**TAARIFA**

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Kunti nataka nimpe taarifa pia; katika madeni ya watumishi kuna wazee ambao wamestaafu milioni 309 ambao hawajalipwa hela zao za kurudi vijijini sasa sijui wako wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala unaipokea taarifa hiyo.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na unacheka si kwa sababu una furahi bali unaumia ndani ya moyo hivi vitu vinakwaza vinaumiza. Sisi kama wawakilishi, sisi kama watumishi wa umma tunaowahangaikia Watanzania, hivi ni kwa nini mzee aliyezeeka shilingi milioni 300 ya mzee aliyelitumikia Taifa hili kweli Serikali inashindwa kulipa?

Mheshimiwa Spika, mimi nikuombe, kama sio kikao hiki basi kikao kijacho, hebu usitulipe Wabunge na sisi tuonje uchungu wa kutokulipwa, usitulipe. Mwezi huu usitulipe mshahara na posho zile zingine Bunge lijalo usitulipe ili tuonje uchungu huu ambao wanakumbana nao Watanzania wenzetu waliolitumikia Taifa hili pamoja na wazee wastaafu waliostaafu ambao mmeshindwa kuwalipa fedha zao. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Ngoja kwanza, subiri kwanza Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge kuna hoja imetolewa hapa wanaounga mkono hoja, hakuna, haya ahsante sana. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Kunti Majala kuna mmoja ameunga mkono kwa hiyo ni wachache, Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa mchangiaji anayechangia vizuri kwamba jukumu la kuwalipa hawa ambao hawajalipwa ni la Serikali, kwa hiyo ambao mishahara yao izuiliwe ni ya Mawaziri wote. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Naona hoja nyingine imetolewa sasa hiyo sitaitoa ili nione nani anaunga mkono. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kunti Majala malizia mchango wako. *(Kicheko)*

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nilikuwa nimesema hii nilikuwa nataka nione ni kwa namna gani Mawaziri wanauwezo wa kunyoosha mikono kwa makosa yao wenyewe ya kutokusimamia watumishi wetu kule chini ili

watendaji wengine waweze kulipwa haki zao watanyoosha mikono.

*Umeona uzalendo wa Mawaziri wetu, kosa wanafanya wao, wameshindwa kuwasimamia watu kule chini wameshindwa kunyoosha mikono wasipate mishahara; ubinafsi uliopitiliza na unafiki uliokithiri.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Timizeni wajibu wenu na majukumu yenu wasaidieni Watanzania walioko kule chini, acheni kula nyinyi raha wenzeu wanateseka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti Majala.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Spika, Waziri una gari, mtumishi anatembea kijiji kilometa 20, 30 hana gari, hana mafuta anatembea kwa miguu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kunti muda wako umeshaisha. Mheshimiwa Waziri amesimama; Mheshimiwa Waziri.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, ninaheshimu sana mchango wake; lakini kwa kweli kwa sababu tu muda wake umeisha. Kanuni zetu haziruhusu kutumia lugha za kuudhi na lugha zinazodhalilisha watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba hili nizungumze kwa muktadha wa Bunge lako, ninaamini kabisa hakuna Waziri yeyote ambaye amesimama hapa akajipiga kifua mbele anatetea ubadhirifu wa fedha hizo ambao umekuwa ukifanywa na Watumishi wa Serikali; hayupo. Tunachokisema; na tutapata muda hapa; tunachokisema hapa ni kwamba ziko hatua zilizochukuliwa labda kwa mfumo, utamaduni wa kuendesha mijadala hapa Bungeni tutakapopata fursa ya kueleza mafanikio ya kazi nzuri ya Serikali

hii inatokana na kazi nzuri iliyofanywa pia na Mawaziri katika udhibiti kama mnavyotuagiza Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kweli hizo lugha hata sisi zinatusikitisha hatuwezi kuambiwa lugha hizo ambazo kwa kweli siyo za kistaarabu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri nisaidie ili niweze kufanya maamuzi, ni maneno gani ya kuudhi ili nataka niyafute.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba sana kiti chako ikiwezekana na ikikupendeza lugha ya kwamba Mawaziri ni wanafiki siyo kweli. Hatukai hapa na hatujakaa hapa tukiwa wanafiki katika kuisaidia hii Serikali yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyokuwa nimesema muda wa Mheshimiwa Kunti ulikuwa umeshakwisha na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi inahusu utaratibu kwa maana ya matumizi ya lugha ambayo kanuni zetu zinakataza. Kwa hivyo katika mchango wa Mheshimiwa Kunti Majala maneno ambayo yametokeza kwa namna ya kuashiria Mawaziri ni wanafiki yanaondoka kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. *(Makofi)*

Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa George Mwenisongole, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, Mheshimiwa Omar Ali Omar ajiandae.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi muhimu sana ya kuchangia taarifa hizi za Kamati hizi tatu *PAC, PIC* na *LAAC*.

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kutujaalia afya na siku njema lakini kipekee niwashukuru sana Wabunge wenzangu. Nirudie tena; kipekee niwashukuru sana Wabunge wenzangu ambao kwa kweli kwa hizi siku mbili nimelala vizuri. Mimi sikuweza kutathmini wingi wa Wabunge ambao wamejitokeza kuongea kwa hisia kuhusu kupinga ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye Biblia, Eliya siku moja alilalamika kwa Mungu kwamba yuko peke yake ambaye haabudu sanamu lakini Mungu alimwambia hauko peke yako wako zaidi ya 7,000. Na leo nimetambua ndani ya hili Bunge kumbe kuna watu 7,000 ambao tunapinga kwa dhati ubadhirifu, ufisadi na wizi. Kwa kweli Wabunge najisikia fahari sana kuwa sehemu ya hili Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze mchango wangu kwa kueleza masikitiko. Mwaka jana Bunge hili lilitoa Maazimio lakini leo ni asilimia 47 tu ya Maazimio yaliyoazimiwa na Bunge kwenye taarifa hii ya *CAG* yametekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa mwaka huu tunakwenda tena kutoa maazimio wakati tuna asilimia 50 ya maazimio tuliyotoa mwaka jana hayajatekelezwa. Kwa mfano, Wabunge wenzangu niwarudishe nyuma, kuna hii Kampuni ya *KADCO* ambayo ilianzishwa na watu binafsi wawili kwa kushirikiana na Serikali kwa ajili ya kuendesha Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa *KIA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 Baraza la Mawaziri lilitoa agizo kwamba hisa zote za *KADCO* zinunuliwe na zikanunuliwa kwa thamani ya Dola za Kimarekani milioni tano, karibu bilioni sita za Tanzania, lakini mpaka leo uwanja huo bado haujarudi na *KADCO* wanaendelea kuuendesha licha ya maagizo ya Bunge hili tuliagiza mwaka jana. Nashukuru Mungu Waziri wa mwaka jana bado anaendelea na nafasi yake, bado anaendelea na hiyo nafasi yake na Bunge liliagiza na yeye akatuahidi kwamba, muda siyo mrefu *TAA* itachukua Uwanja wa Ndege wa *KIA* na kuundesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nimhoji Mheshimiwa Waziri hivi nani yuko nyuma ya *KADCO*? Hili ni lazima Wabunge tusiliache, tunataka tumjue nani yupo nyuma ya *KADCO* ambaye anakiuka maagizo ya hili Bunge na Serikali inaogopa kuurudisha ule uwanja ambao tayari ilishaununua na kulipa hisa zake. Hivi kweli Wabunge tufumbie macho na hilo? Tufumbie macho na hilo? hivi Watanzania watatuelewaje? Leo tena tutoe agizo lingine kusema

Uwanja wa Ndege wa *KIA* urudishwe Serikalini wakati tayari maagizo yalishatolewa na hela ilishalipwa. Hivi tunaipeleka wapi nchi hii na nani huyo ambaye anamiliki hiyo *KADCO* mpaka ana kiburi cha kukataa Maazimio rasmi ya Bunge, Serikali na Baraza la Mawaziri ambayo vyote viliagiza?... *(Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa naomba taarifa yako iwe ya afya maana yake nahutubia Taifa…

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest…

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa naomba taarifa yako iwe na afya maana yake nahutubia Taifa hapa. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, hiyo *KADCO* inayoendesha Uwanja wa Ndege wa *KIA,* inaendesha bila hata Mkataba, kinyume na Sheria za Nchi na bado inaendesha huo uwanja na siyo hiyo tu bado imeisababishia Serikali hasara ya kutosha…

**SPIKA:** Mheshimiwa taarifa ni moja…

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo taarifa yangu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa George Mwenisongole unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, kwa kichwa, mikono na miguu naipokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kama hili Bunge litashindwa kuchukua hatua kuhusu *KADCO,* hakuna maana basi ya Taarifa

ya *CAG* kuletwa Bungeni, hakuna maana. Hili liko dhahiri kabisa, liko dhahiri kabisa na hata tukisema kwamba, Mheshimiwa Waziri ambaye alituhaidi kwamba *KADCO* itarudishwa Serikalini mpaka sasa hivi bado yupo kwenye nafasi yake kwa kweli mimi nashindwa kuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge, tumetumia hizi siku mbili kulalamika, lakini niwaulize Sheria za Nchi anatunga nani, si sisi? Naomba tufanye maamuzi magumu na nikushukuru Mheshimiwa Maganga, naomba uingize jina langu katika orodha ya Wabunge wanaotaka Sheria ya Watu Kunyongwa wanaofanya ufisadi, George Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, hakikisha unaandika jina langu leo, sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu sisi ndiyo tunatunga sheria, naomba kabla ya Bunge hili kwisha tujitolee Wabunge tulete Muswada binafsi kwamba, taarifa ya *CAG* inapotoka tutunge sheria Serikali ilete taarifa ya utekelezaji wa Maagizo ya *CAG* na Maamuzi ya Kamati na Maazimio ya Wabunge ndani ya miezi mitatu baada ya taarifa ile kutoka. Kama Serikali haitaleta maazimio ya kuonesha utekelezaji wa hizi taarifa tutakuwa tunafanya kazi bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, naomba Wabunge mniunge mkono na Watanzania wote wananisikia. Naomba tutoe azimio wezi wote wa kuku, wezi wote waliopora simu waachiwe. Kama hatuwezi kuwafunga watu wanaoibia ushirika, kama hatuwezi kuwafunga Wakurugenzi wanaotafuna fedha, kama hawa watu wa *KADCO* wanaiibia Serikali mchana kweupe hatuwezi kuwafunga, kwa nini tuwaonee wezi wa kuku? Kwa nini tuwaonee hawa wezi, hawa wezi tuwaachie. Kuna sababu gani ya kuwakamata watu wa hao wezi, wakati majizi makubwa wanaoitia hasara Serikali wanaachia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili Bunge litaingia katika historia kati ya Mabunge bora duniani kama tutatoa azimio la kuwaachia wezi wote wa kuku. Hakuna sababu ya kuwaweka ndani wakati wezi wakubwa tunashindwa kuwachukulia hatua, kuna maana gani basi ya sisi kuwa Wabunge? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tumechoka, kule kwetu Mbozi kinachoendelea ni vichekesho, kinachoendelea ni vichekesho. Watu wamekamatwa, Viongozi wa Vyama vya *AMCOS* wamekatwa na wamekiri kwamba wameiba hela, eti wameambiwa rudisheni hela halafu wakaachiwa. Waliyofikishwa Mahakamani ni wale ambao waligoma kurudisha hela hivi kweli mtu ameiba, amekiri…

**MHE. ALLY M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** …kwamba ameiba halafu wanawaachia, hivi hii nchi tunaipeleka wapi?

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole, kuna taarifa kutoka Mheshimiwa Ally Mlaghila Jumbe.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, nimesema taarifa naomba iwe ina afya maana yake nahutubia Taifa. *(Kicheko)*

**TAARIFA**

**MHE. ALLY M. JUMBE:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba hata Kyela ni hivyo hivyo kwenye *AMCOS,* watu wameiba pesa lakini wanasema zichangwe kokoa ndiyo zilipe wakati aliyeiba yupo anaonekana.

**MHE GEORGE R. MWENISONGOLE:** Lakini…

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole muda wako ulikuwa umeisha, sekunde thelathini malizia.

**MHE GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu. Niliomba ukaguzi maalum wa *CAG* na *CAG* ametoa taarifa yake. Nimemkabidhi Mheshimiwa Waziri Mkuu, ameniahidi ndani ya wiki mbili anakuja Mbozi.

Mheshimiwa Spika, kipekee nimshukuru Waziri wa Kilimo ambaye alileta timu ya wakaguzi kule Mbozi, imeifanyia kazi na naamini Mheshimiwa Bashe ataongozana na Mheshimiwa Waziri Mkuu anapokuja Mbozi ndani ya wiki mbili tunataka tufanye mfano, tunataka tufanye Mbozi iwe *pilot study,* sisi hatutaki ufisadi Mbozi…

**SPIKA:** Haya ahsante sana…

**MHE GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Omar Ali Omar na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi ya kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa zawadi ya kukutana siku ya leo. Nichukue nafasi hii kukupongeza wewe kwa heshima kubwa uliyolijengea Taifa hili, Bunge hili na Afrika kwa kuchaguliwa kwako kuwa Spika wa Umoja wa Mabunge yote Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natamani kama ningepata nafasi ya kusimama kwenye Jukwaa la Mji wa Mbeya kuwaambia watu wa Mbeya kwamba mmeipa Tanzania zawadi njema kabisa, mmeipa Afrika zawadi, mmeipa dunia zawadi ya kiongozi kijana, makini na msomi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado nitasema hivi ndani ya Bunge, nitasema popote nitakapokwenda kwa sababu maandiko matakatifu yananiambia Yesu Kristo alisema; "Atakayenionea haya mbele za watu na mimi nitamuonea haya mbele za Baba yangu."

Mheshimiwa Spika, unazo sifa mdogo wangu na bosi wangu, endelea Mungu atakubariki, huu ni mwanzo tu wa mchango wako katika ulimwengu tunaoukanyaga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Biteko kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kwa nafasi ya kuwa Naibu Waziri Mkuu. Kwa namna ya pekee naungana na Wabunge wenzangu wote kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi njema anayolifanyia Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mashaka juu ya dhamira njema aliyokuwanayo Mheshimiwa Rais kwa nchi, hii amejitoa kwa hali na mali, ametafuta fedha kwa kukusanya kodi ya wananchi, ametafuta fedha za wafadhili za misaada na mikopo ili kuhakikisha kwamba ustawi wa nchi unapatikana. Nataka niseme wazi, sina mashaka kwamba mafanikio haya ya Mama Samia yana mkono wa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri waliopo, Makatibu Wakuu pamoja na Makamu wa Rais anayemsadia, lakini yana mkono pia wa Bunge hili lilosimamia fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende moja kwa moja kwenye mchango wangu na naanza kuwakumbusha vijana na Taifa hili juu ya maneno ya aina ya viongozi wanaopaswa kukabidhiwa dhamana za kutumikia umma katika Serikali na taasisi zingine zilizoko chini ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa 81 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ukurasa wa 103 na ukurusa wa 104 inasema hivi naomba ninukuu: "Kwa hiyo hata katika hali ya demokrasia na ujamaa wakati wote ni muhimu kwa chama na umma kuwa na hakika na anayekabidhiwa madaraka haya ya Serikali maana yakiangukia katika mikono ya wapinga mapinduzi, madaraka hayo yanaweza kutumika dhidi ya maslahi ya umma wenyewe, hivyo chama kuongoza maana yake ni kuhakikisha pia kuwa madaraka muhimu ya Serikali na ya Mashirika ya Umma wanakabidhiwa watu ambao pamoja na uwezo wa kitaaluma…" naomba sana nikazie hapa; "pamoja na uwezo wa kitaaluma ni wenye msimamo wa kizalendo, waaminifu kwa chama na wakulima na wafanyakazi wa Tanzania." Mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna mashaka kwamba Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu yetu Kichere inathibitisha pasipo shaka juu ya matumizi mabaya na upotevu wa fedha za umma kwa muda mrefu sana. Sasa kosa liko wapi? Kosa lipo katika upangaji wa safu ya watendaji na viongozi katika Serikali hii yetu. Naomba kusema hakuna namna unaweza kutenganisha uongozi na maadili, kwa sababu maadili ni sifa ya uongozi, lakini siku hizi mkiangalia leo, mkipitia Ripoti ya *CAG* ya 2021/2022 na mkaenda 2020/2021 na mkaenda 2019/2020 hakuna shaka kwamba waliohusika katika miaka yote hiyo bado ni watumishi walioko katika Ofisi za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, rai yangu nakusudia kuleta marekebisho hapa ya kuliomba Bunge hili liliridhie na kukuomba wewe uridhie tuunde Kamati Teule ya kuchunguza, kwa sababu tumekuwa tunapokea Ripoti ya *CAG,* inakuja Bungeni, tunafanya maazimio, sasa baada ya maazimio tunaishia wapi? Lazima tuangalie namna bora ya kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge na hatua zilizochukuliwa dhidi ya wale ambao wamefanya makosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namna pekee ni kwa kuunda Kamati Teule ya Bunge itakayokwenda kuangalia ukaguzi wa miaka mitatu, waliotusababishia dosari hizo, wamechukuliwa hatua gani, bado wapo maofisini au wameondolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukifanya hivi tutakuwa tumekusaidia wewe, tumeisaidia nchi kuhakikisha kwamba Bunge linatimiza wajibu wa Bunge makini ambalo litaacha rekodi ya kuhakikisha kwamba fedha za walipa kodi zinafika maeneo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, haivumiliki, haivumiliki kwamba wanafanya maamuzi kama haya *KADCO,* Bunge lifanye maamuzi, Baraza la Mawaziri linafanya maamuzi, halafu tumelipa na fedha za kununua hisa, bado wanashindwa kukabidhi shughuli za *KADCO* kwa *TAA,* kuikabidhi kwa Serikali, tulimlipa nani fedha hizo? Tulifanya uamuzi huo, wewe unayekaidi wewe ni nani wa kukaidi maamuzi ya Bunge na maamuzi ya Baraza la Mawaziri? Naungana wa Wabunge kusema kuna haja ya kuchunguza na

kujua ukweli juu ya jambo hilo kwamba nani anajificha hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme wazi tatizo tulilonalo na ukinzani ambao tunao na wenzetu waliopo kwenye *front bench* ni vizuri Mawaziri wakajua, viongozi makini hawawezi kuishia kwenye *dilemma*. Wote, tumekula kiapo kwamba rushwa ni adui wa haki, sitapokea wala kutoa rushwa, cheo ni dhamana, nisitumie cheo changu wala cha mtu mwingine kwa faida yangu. Ziko kwenye ahadi ya mwanachama wa chama chetu na hii ndiyo inatujengea uhalali kwamba chama hiki kimeendelea kuwa mtetezi wa kuaminika wa maslahi ya wakulima na wafanyakazi pamoja na madaraka yao ya uwajibikaji wa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere alizungumzia shida ya *dilemma* ya viongozi wasiokuwa madhubuti kwenye kitabu cha Uongozi Wetu na Hatima ya Tanzania anasema hivi: "Kifo cha maji kushoto, kulia kifo cha moto, kukubali, kukataa kila moja ni balaa, kote huko hatarini, hujui ufanye nini?" Ninyi mko kwenye *dilemma* na mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viongozi wako kwenye hatari ya kufanya maamuzi, wanakumbuka ahadi yao ya CCM? Wanakumbuka maamuzi ya Bunge? Wanakumbuka wajibu na hasira ya Rais, dhidi ya Ripoti ya *CAG*? Kinachonitatanisha kwa nini hawafanani na uso wa Mama Samia siku anapokea Ripoti ya *CAG? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ningekuwa Waziri, ningelikuwa Waziri miezi sita hii, hakuna ambaye angebaki aliyetuhumiwa kwenye ufisadi, kwenye Wizara yangu. Hata hivyo, nataka niwaambie wako watu wamefanya ufisadi kuanzia kwenye *IPTL* na leo wako Serikalini, pamoja na Maazimio ya Bunge, wako watu na nataka kusema ni leo tu nanyamaza, kesho kutwa katika mjadala mwingine nitataja nani wako nyuma ya *IPTL*, nitataja nani wako nyuma ya ufisadi wa *Standard Gauge Railway* ambayo manunuzi ya *lot one* imetugharimu hasara ya zaidi ya trilioni 1.45. Hizo fedha tungegawawi Majimboni, tungegawiwa Majimboni, Zanzibar…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, dakika moja malizia.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, tungegawiwa Majimboni maana yake hata Zanzibar kwa mgao wa kanuni ile ile, wangepata zaidi ya bilioni karibu mia tatu, mia tatu na sisi tungepata katika Majimbo yetu zinazotosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakusudia kuleta marekebisho haya, nimeshayaweka mezani ili tufike mahali tutafute dawa na nitaomba Bunge hili liniunge mkono ili tuweze kuunda Kamati Teule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nitakuwa sijavunja Kanuni chini ya Kanuni ya 139 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la mwaka 2023, baada ya *CAG* kuchunguza habari hizi na kuzileta, nataka kutoa hoja na naomba niungwe mkono kama Kanuni zinaruhusu kwa sababu nimeshaweka kwenye meza, nimempa Katibu wa Bunge kuundwa kwa Kamati Teule ya kuchunguza ufisadi huu na kuweza kutusaidia Bunge hili tuweze kutoka, hii itatenda haki kwa sababu Mawaziri watakuwa hawajaonewa kwa sababu watapata haki ya kujieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge itakayoshughulikia mambo haya. Naomba mniunge mkono kabla sijavunja Kanuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siko nayo hii hoja hapa mbele, siko nayo na yeye amewaambia kwamba amekabidhi. Kwa hiyo, pengine wanatazama utaratibu mzuri wa kuitumia, siko nayo hapa mbele. Kwa hivyo siwezi kusema kama imeungwa mkono ama kwa namna gani. *(Kicheko)*

Sawa nilikuwa nimeshawataja Mheshimiwa Omar Ali Omar, atafutiwa na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga na Mheshimiwa Kihenzile, ajiandae.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii adhimu. Kwanza, sina budi kumshukuru *Allah Kareem* aliyeumba mbingu na ardhi na vilivyomo vyote tukapata uhai huu ambao tumo katika siku ya Jumamosi tukiwa sote tuko wazima.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa na ufahari mkubwa leo nimesimama katika Bunge lako Tukufu ukiwa wewe ndiye Rais wa Mabunge ya Dunia. Kwa kweli nakupongeza sana na nina imani kwamba, Wabunge wote wataunga mkono hili la kukupongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili kwa heshima na taadhima, naomba uniruhusu kidogo nitoe ushairi ambao mtaalam wa Lugha ya Kiswahili kule Zanzibar ndugu yangu Haji Gora aliutoa katika kitabu chake cha kimbunga. Katika kitabu cha kimbunga ndugu yangu Haji Gora alizungumza maneno yafuatayo; katika ushairi wake alisema kwamba: "Chura kakausha mto, maji yakamalizika, Pwani kuliwaka moto, mawimbi yaliyowaka usufi nusu kipeto, rikama likavunjika, nyoyo zikafadhaika." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana ya ushairi huu ni kwamba sote Wabunge tuliomo humu, tumefadhaika sana na Ripoti ya *CAG* na tumefadhaika kwa sababu ya hali ya upepo wa fedha za walipakodi wa nchi hii zinavyotafunwa, zinatafunwa mkono wa kulia wa kushoto haupati. Zinatiwa kwenye pua ya upande wa mkono wa kulia wa kushoto haupati, matokeo yake hali ya uchumi inadorora na matokeo yake Wananchi wetu wanabaki katika umaskini uliokithiri.

Mheshimiwa Spika, nataka nizungumze kuhusu Wazabuni na Wakandarasi ambao imezungumzwa katika ripoti zetu hizi tatu kwenye ukurasa wa 44. Taasisi 259 zinadaiwa na Wazabuni, zinadaiwa na Wazabuni ambapo Serikali inadaiwa jumla ya trilioni 4.82 kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha sana, lakini wazabuni

pekee wanadaiwa fedha trilioni 3.40 sawa na asilimia 83, hilo ni deni la wazabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri nina *documents* ninataka nitaje baadhi ya taasisi za Serikali ambazo zinadaiwa madeni makubwa. Kwa mfano, kuna Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania inadaiwa bilioni 60. Wakala wa Ufundi wa Umeme *(TEMESA)* bilioni 49, Wakala wa Huduma ya Ununuzi wa Serikali *(GPSA)* inadaiwa bilioni 13. Kwa kweli hicho ni kimbunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, SUMA JKT Kampuni ya Ujenzi inaidai Serikali, wazabuni hao jumla ya bilioni 10. Mfuko wa Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* bilioni 90. Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA)* bilioni 41. Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano Dar es Salaam bilioni 137. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa angalia kimbunga hiki, Mamlaka ya Mapato Tanzania ambao ndiyo Taasisi Mama inayokusanya mapato inadaiwa bilioni 224, hawa ni wazabuni ambao wanaidai Serikali kwa kipindi kirefu sasa. Sasa nenda basi ukaangalie katika hospitali zetu. Ukienda Benjamin Mkapa, wazabuni hawa wanapima *pressure* kipimo kinasoma juu moja kwa moja. Ukienda Hospitali ya Mirembe, ambako huko ndipo wagonjwa wanaoshikwa na matatizo ya akili, napo huko wapo wazabuni ambao tayari wameshakwenda kule, kwa sababu akili hazifanyi kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo yake watanzania hawa ndiyo wale ambao sasa hivi waliokuwa sasa hawana uchumi tena, nyumba zao zimepigwa mnada na mabenki, viwanja vyao walivyokuwa navyo vimeuzwa, magari yao waliokuwa wakitembelea waliokuwa wakifanya kazi nayo yamepigwa mnada, matokeo yake ni kwamba hawa wamekuwa masikini. Hii ni kuionesha kwamba Serikali haijawa makini katika kulishughulikia suala la hawa wazabuni.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika hii *paper* niliyonayo, mpaka Wizara zote zimo humu, Wizara zote zinadaiwa na

wazabuni! sasa hii tunakwenda wapi? tunafika wapi ikiwa Serikali inadaiwa namna hii na deni kubwa kama hili, je tunafanyaje? Mawazo yangu mimi, maana yake najua kwamba wasimamizi wa Serikali ni Mawaziri, lakini kuna watendaji wao. Hao watendaji ndio wanastahiki sasa wawajibishwe, kwa sababu hizi fedha nina imani kwamba zinakwenda, Mheshimiwa Waziri wa Fedha anatoa Fedha na anazipeleka, kwa sababu tunampitishia fedha kwenye bajeti lakini matokeo yake fedha hizi zinaliwa na watu wachache.

Mheshimiwa Spika, mawazo yangu mimi, wenznagu wengi walisema kwamba wanyongwe lakini ukinyongwa ndio umeshakufa, utakuwa huonekani wala hupati uchungu, kwanza wezi hawa tuanze kuwakata mkono, wakiona mkono mmoja hawana watajua kwamba kweli waliiba pesa za watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia wafungwe jela wawekewe daftari maalum la uzalishaji, kwamba ikiwa umezalisha kule mali ya 10,000 na ionekane deni letu lile tulilokuwa tunawadai tayari 10,000 imetoka, mpaka muda wao umeisha. La tatu na mwisho, wafilisiwe mali zao hadharani na kila mtanzania ajue kwamba mali hii inafilisiwa kwa sababu ya kuibia Serikali mali ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno hayo mafupi mimi naunga mkono hoja asilimia 100, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge kuna Wabunge wawili ambao nilikuwa nimewataja lakini walikuwa na dharura, kwa hiyo nimeletewa taarifa hapa kwamba, wameshakuja.

Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mheshimiwa Abubakari Asenga, ajiandae.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja hizi tatu za *CAG* zilizoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja za Kamati zote tatu na pia naunga mkono mapendekezo yote ambayo Kamati hizi tatu zimependekeza.

Mheshimiwa Spika, hii Taarifa ya *CAG, CAG* mwenyewe anasema ukaguzi anaoufanya kwa sasa, ni kwa asilimia 16 peke yake. Waheshimiwa Wabunge, haya ambayo tunayaona na tunayasikia ni kwa asilimia hizo peke yake, wakati atakapokuja kufika kwa asilimia 50 hali itakuwaje? Kama hii ni 16% peke yake ukaguzi huu alioufanya haya ndiyo tunayaona, akija kufika asilimia 50 hali ya nchi yetu itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amekuwa akipeleka fedha nyingi katika Halmashauri zetu. Wabunge wengi nilivyokuwa nawasikia wakichangia, hakuna mtu anayekataa *force account*. Hapa Kamati tumesema na tumetoa mapendekezo kwenye Kamati ya *LAAC* lakini fedha hizi zinazokwenda miradi mingi iliyopo ya *force account* haina ubora. Hata kama imekamilika mingine ukipita madarasa yana nyufa, madirisha hayafai, *ceiling boards* ni za hovyo, kuna vitu vinavyotendeka kule ni vya ajabu kweli kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naomba niseme, hakuna aliyekataa suala zima la *force account* lakini mimi binafsi nilikuwa kwenye Kamati ya *LAAC* na nimeshawahi kutembelea miradi mbalimbali, ipo Halmashauri moja ambayo sisi tuliietembelea, wanasiasa miongoni mwetu tunasababisha ubadhilifu wa hizi fedha kwenye maeneo yetu baadhi ya maeneo. Kuna hiyo Halmashauri na nimpongeze huyu Mkurugenzi wala sitamtaja, baada ya kuona sintofahamu ya hizi fedha wanasiasa wameingia humo, watendaji wanagambana, Mkurugenzi huyu aliamua kutafuta Mkandarasi na kukaa naye chini. Akamwambia Mkandarasi nimeletewa milioni 500, sina hela ninataka kujenga majengo moja, mbili, tatu, fedha niliyonayo ni hii hapa, angalia unaweza kuchukua mradi ama huwezi kuchukua mradi, kazi inafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge kwenye Kamati tumeiona kazi inafanyika, kwa sababu Mkurugenzi huyu aliona hali inapoelekea ni mradi kutokukamilika na mwisho wa siku yeye ndiyo atakayekuwa *responsible,* akaamua kufanya alichokifanya. Kwa hiyo, kuna uwezekano yapo maeneo ambayo unaweza ukafanya *negotiation* na Wakandarasi na wakaweza kufanya kazi vizuri kama ambavyo wanafanya hawa watu wengine ambao tunasema ni wa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakuta Mkandarasi amekaa miaka mitatu, minne, mitano, hana kazi, anakuja kuambiwa kuna milioni 500 kuna Mkandarsi atakayekataa? Hayupo. Kwa hiyo, zipo kazi zinafanyika na wapo Wakurugenzi ambao wanaamua kufanya maamuzi hayo ili yeye aweze kuwa salama na zile fedha zilizopelekwa ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa iliyopo katika Halmashauri hizi ni usimamizi wa fedha hizi. Watu wamesema hapa, ni ukweli usiopingika fedha nyingi zinakwenda, miradi inafanyika lakini fedha nyingi zinapigwa. Watu wanakula fedha kweli kweli huku chini lakini yote hii ni kwa sababu ya usimamizi mbovu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mnaenda Kamati mnafika mnakuta mradi, Wabunge tuliokwenda kwenye Kamati tunashangaa, timu ya TAMISEMI tuliyoongozana nayo inashangaa, timu ya Mkuu wa Mkoa tuliyonayo inashangaa, timu ya Mkuu wa Wilaya tuliyonayo inashangaa, Uongozi wa Chama Cha Mapinduzi ambao ndiyo wenye Ilani na wenyewe unashangaa kwa hali ambayo tunakutana nayo kwenye maeneo hayo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jiulize sisi Wabunge tumuulize nani? Kama wote walioko hapa na wote ambao ni wahusika wanashangaa, sisi Wabunge ambao tunatoka huko tukamuulize nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapozungumza kuhusu suala zima la Wabunge ni kweli Wabunge tupo kwenye Halmashauri lakini siyo Wabunge wote ambao tuko kwenye Kamati ya Fedha. Hata hao walioko kwenye Kamati za Fedha tumeshaomba Bunge hili kila

mara, ratiba zibadilishwe, ratiba zisiwekwe kipindi ambacho Bunge linaendelea. Ratiba nyingi zinawekwa kipindi ambacho Bunge linaendelea, kule Halmashauri kwetu kuna vikao, unaenda kule unakimbia huku, unarudi huku, jamani! Yapo mambo mengine hata Wabunge wakisema na wapo Wabunge ambao wanazungumza hapa wengine ni wenzetu Wabunge ambao ni Mawaziri. Majimbo yao na Halmashauri zao ni hovyo kweli kweli. Tumekagua tuomeona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo hizi *POS*…

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nilitaka kumpa taarifa ni kweli kwamba Wabunge ni Wajumbe wa Kamati za Fedha kule, sisi tunapokea tunapitisha ile miradi lakini sisi hatuendi kusimamia mifuko ya *cement* inayoachwa kuoza, hatuendi kusimamia hela zimeibiwa au panajengwa vipi, wapo wataalam, ipo Serikali.

Mheshimiwa Spika, ni kweli Chama cha Mapinduzi kinashangaa, chenyewe ni bosi kimeweka Serikali ndiyo *contractor* wa kuhakikisha anatekeleza mradi. Kwa hiyo anayeharibu ni yule *contractor* aliyepewa kujenga siyo sisi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga unaipokea taarifa hiyo? *(Kicheko)*

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, usimamizi kwenye suala zima la miradi ni changamoto na hilo tulikubali. Kwanza tukushukuru na tukupongeze kwa kuamua kuboresha

mambo mbalimbali kwenye hizi Kamati tatu wakati wanapokuwa wanafanya majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika tulikuwa tunakaa mpaka saa sita za usiku, lakini tulikuwa tunataka kuhakikisha tunapokuja na taarifa tuje na taarifa inayokamilika. Ni kweli kuna mambo ambayo tayari yanafanyiwa kazi, mengine tayari hatua zimeshachukuliwa lakini tulikuwa tunapata changamoto kubwa sana. Unakuta kuna Mkurugenzi amefanya ubadhilifu wa hali ya juu baada ya taarifa ya *CAG* ya Mama aliposema, Mkurugenzi huyu kashachukuliwa hatua, ameshapelekwa kwenye Muhimili mwingine unakuja hapa unataka kuhoji ujue nini kilichoendelea humpati yule mwizi. Unampata mtu mwingine ambaye hawezi kukueleza chochote ambacho kimeendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hiyo nayo pia ni chagamoto na ni tatizo ambalo tulikuwa tunakutana nalo. Kitendo cha kuongezea muda Kamati hizi kimesaidia kuweza kuhoji Halmashauri nyingi kwa wakati mmoja, kiasi kwamba tumegundua Halmashauri nyingi zina mambo mengi kwa sbabau haziitwi na Kamati ya Bunge kwa muda mrefu hivyo kupelekea mambo mengi zaidi kuharibika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ninakupongeza lakini pia tunaendelea kuomba utusaidie hizi Kamati ziweze kufanya kazi zake kwa ufanisi kwani mambo yaliyoko huku chini na hizi Kamati ikiwepo Kamati ya *LAAC* ndiyo Kamati ambayo ina TAMISEMI kwa wananchi na wananchi hao ndiyo wanaitegemea Serikali iweze kufanya mambo mazuri.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Saashisha Mafuwe atafuatiwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mheshimiwa David Kihenzile ajiandae.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja zilizoko mezani.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kukupongeza wewe mwenyewe kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, hongera sana. Hii siyo kwa sababu ya jambo jingine unao uwezo mkubwa na umetuheshimisha sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anazozifanya kwa ajili ya nchi yetu na nimefurahi sana juzi wananchi wa Hai walikuwa barabarani, umeme ulizimika sasa tumewekewa pale taa za barabarani Bomang'ombe barabara kama nne, wanasema wanamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimshukuru Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu. Hapa niseme kidogo, Mheshimiwa Waziri Mkuu anafanya kazi kubwa, tunaona anavyohangaika haya majizi tunayosema huko, siyo tu kwamba wanatudanganya sisi, hata Waziri Mkuu akienda huko mnaona wanavyomjibu. Mheshimiwa Waziri Mkuu nikupe pole sana hao ndiyo watumishi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu kwa kuaminiwa na kupewa dhamana kubwa, mimi nimwambie tu Watanzania wanataka umeme na mafuta ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze na *issue* ya *KADCO* imezungumzwa hapa. Mimi niwaambie Waheshimiwa Wabunge pamoja na *investment* kubwa inayofanyika, sasa hivi Serikali imetoa bilioni 11 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi waliokuwa kwenye eneo lile la Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro watoke na wamekubali. Mimi nashangaa tumepitisha hapa tuambiwe kiwanja kile kisimamiwe na Mamlaka ambayo ni ya Serikali mpaka leo halijafanyika.

Mheshimiwa Spika, jambo hili linaudhi na mimi niwaambie nipo kule *site*, likichelewa jambo hili tutazungumza lugha nyingine baadae, siyo vyema. Ninaomba sana Serikali ifikie mwisho ichukue maamuzi.

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Ole-Sendeka kwamba tuunde Kamati Teule iende awamu tatu taarifa ya *CAG,* tuone *CAG* aliagiza nini, nini kimefanyika na kwa nini na hatua gani zinapaswa kuchukuliwa?

Mheshimiwa Spika, tusipofanya hivi, tutakuwa tunazungumza hapa kila mwaka tunajaa gesi hapa mambo yanaendelea vilevile. Waheshimiwa Wabunge sote tunafahamu Utumishi wa Umma kuna shida. Kuna shida kubwa hawa watu wameshakuwa sugu, hivi nawaambia wengine wako mule, hawa wanasema majamaa wanapiga stori wataondoka, *business as usual!* wako pale wanatusikiliza, wanajua kabisa hakuna kitakachofanyika. Mheshimiwa Waziri Mkuu wanakusikiliza pale! Wanajua hawa wataongea wataendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niwaambieni tumepita Kamati ya TAMISEMI huko Halmashauri, tunawasilikiza wakija kwenye Kamati, anakuja Mkurugenzi pale unamsikiliza huyu mtu hata kujumlisha hesabu zinawashinda, unamuuliza swali mtu mwepesi kabisa. Hapa kwenye Taarifa ya Kamati ya *LAAC* wameandika naomba nimnukuu "Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kujiridhisha kutokuwepo kwa ufanisi wa utendaji wa Wakurugenzi". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama watu hawana ufanisi Mheshimiwa Waziri Mkuu wameshindwa kazi hawa watu. Tunaenda mahali pale Iringa ni aibu, tukaenda kuangalia soko lile ni kilio. Mheshimiwa Waziri Mkuu utembelee pale. Nadhani awamu hii utawapiga makofi, kwa sababu ni aibu! Ni vitu ambavyo havifai. Mheshimiwa Waziri Mkuu hebu tufikirie Mheshimiwa Rais wetu amefanya kazi kubwa, ametupatia fedha, mtu anapewa trilioni 1.2 nenda kajenge madarasa kwa mradi wa *SEQUIP*, pesa umepewa *cash,* tengeneza ramani wewe, tengeneza mpago wa ujenzi wewe, tengeneza *feasibility* wewe, unaenda kujenga madarasa hayakamiliki, kama siyo maksudi, kama siyo hila, kama siyo mpango mbaya wa kumuhujumu Mheshimiwa Rais, ni kitu gani? Kwa sababu siyo pesa ya mkopo, pesa ipo *cash*. Unaenda pale darasa halijakamilika havieleweki vitu vinavyofanyika, haya ni maksudi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niseme tubadilishe mazungumzo namna ya kuzungumza na hawa watumishi. Mheshimiwa Jenista Mhagama hapa Mama yangu ameongea kwa uchungu sana na mimi nikamuonea huruma, lakini Mheshimiwa Waziri tumkamate nani zaidi ya ninyi? Sisi tuwabane na ninyi mkawabane wale. Ninyi ndiyo *size* yetu. Tunafahamu mnafanya kazi nzuri sana, lakini hawa majizi mnayo humo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Bashe ana majizi yake kwenye Ushirika kibao ya kutosha, Mheshimiwa Kaka yangu hapa Mchengerwa una majizi yako kule TAMISEMI ya kutosha na unayajua, nenda kayatoe, ukiyatoa sisi tutakuja hapa tutapongezana, kwa sababu hivi vitu vinafanyika ni maksudi kabisa! Haya majizi ya Ushirika Mheshimiwa Bashe anayajua, kila mwaka tunazungumza anayo mule ndani, sasa mnataka tukamwambie nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa TAMISEMI unafahamu majizi unayo, Wakurugenzi ambao hawaeleweki wanafanya miradi ya hovyo, unafahamu na wewe upo kwenye Kamati yetu! Sasa usipochukua hatua unataka tukamwambie nani? Hawa watu wanamhujumu Mheshimiwa Rais na sisi ndiyo kazi yetu kusema hapa. Hizi fedha hizi hebu fikiri…*(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa Mheshimiwa Saashisha. Ndugu yetu Waziri wa Ujenzi, nyumbani kwao kwa Mama yake Sengerema kuna kituo kinajengwa cha afya na yeye alikuwa ni Waziri wa TAMISEMI. Imepelekwa pesa imeliwa na madarasa hayajaisha. Karibu sana Mchengerwa Sengerema. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, unapokea taarifa hiyo?

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, naipokea na bahati nzuri tulienda Mwanza, tuliona hilo jambo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa kweli nilikuwa nasema hizi fedha ifike mahali tumuonee huruma huyu Mama, anayo dhamira ya dhati ukimsikiliza unaona huyu Mama anatamani mabadiliko, anatamani watu wapate huduma. Hivi hawa watu wanaomsaidia mbona hawafanani na huyu Rais wetu, mnataka tufanyaje?

Mheshimiwa Spika, unajua tunafikia mahali watu wanafikiri, mimi tukiwa pale Mbeya kwa kweli nilijikuta nimesema tu, hivi kwa nini hawa watu wasipigwe risasi? Inafika mahali unaona ni hujuma fedha hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nizungumze tu kwenye elimu, TAMISEMI wamepewa trilioni 1.2 kwa ajili ya *SEQUIP,* wamepewa pesa za *BOOST* bilioni 1.15, wamepewa fedha kwa ajili ya vyoo bilioni 230 haijawahi kutokea! Hawa watu wamechanganyikiwa wanafikiri hela ni za kwao hizi, Mheshimiwa Mchengerwa usipochukua hatua wanadhani ni zao. Hawa watu hawako na mama tukuambie hapa uelewe, nendeni mkachukue hatua kwenye utumishi wa umma kuna jambo la kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa ndio mahiri wa kusema aah, wanasiasa ndio wanaharibu nchi, Wabunge; wanatusema sisi wakati wao ndio wanaoharibu vitu, wao ndio hawafanyi kazi. Mheshimiwa Ndejembi tumeendanaye ziara, ni aibu tupu. Anasimama Mkurugenzi, unajiuliza, huyu mtu katokea wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami niseme jamani, turudi kwenye utaratibu. Kanuni za kudumu za Utumishi wa Umma, namna ya upatikanaji wa Wakurugenzi, imeelezwa. Sheria za utumishi zipo wazi, awe amefanya kazi miaka 12, awe na uzoefu. Wakati mwingine ni sawa hatujadili kuhusu namna ya uteuzi, lakini

tunashauri, turudi kwenye sheria kwa sababu, Mkurugenzi anaenda pale Halmashauri ni mpya, katokea kwenye taasisi nyingine, hajui chochote. Anakuta Wajumbe, wale Wakuu wa Idara, ni magwiji yako pale miaka na miaka. Mkurugenzi anakuja maskini wa Mungu ni mwepesi, hajui kinachoendelea, wale ndio wanamtengenezea ramani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unajikuta Mkurugenzi yuko pale, hajui kinachoendelea kabisa, haijui Halmashauri. Ndiyo maana akija hapa kila ukimwuliza swali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umekwisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Dah!

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja zote za Kamati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, atafuatiwa na Mheshimiwa David Kihenzile, na Mheshimiwa Judith Kapinga, ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kupata nafasi hii nami niweze kuchangia. Kwanza kabisa kabla sijasahau, niseme naunga mkono hoja za taarifa za Kamati zote tatu.

Mheshimiwa Spika, kwanza nami napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa fedha nyingi ambazo ametuletea katika Halmashauri yetu ya Mji wa Ifakara na Jimbo la Kilombero. Sasa hapa lazima tutofautishe kuletewa fedha na matunda ya zile fedha katika miradi ile.

Mheshimiwa Spika, ukienda huko kwenye kuona miradi kutokana na fedha ambazo Wizara ya TAMISEMI imetuletea na Mheshimiwa Rais ametuletea ni vitu viwili tofauti na ni vitu viwili mbalimbali. Napenda sana kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt.

Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea Mkuu wa Mkoa wetu, Dkt. Malima na Mkuu wetu wa Wilaya, Dunstan Kiwobya. Waziri wa TAMISEMI na viongozi nataka niwaambie, kama sio huyu *DC* mpya aliyekuja, Wakili Dunstan Kiwobya, basi miradi yetu ingekuwa mibaya mara tatu. Huyu Mkuu wa Wilaya aliyekuja naye ameshaanza kuletewa chuki na hao ma-*tycoon* wa Halmashauri kwamba anaingilia mpaka kwenye kusimamia, mpaka kwenye kufunga taa usiku ili miradi iende. Kwa hiyo, pamoja na hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kweli, kwa mabadiliko haya ya kutuletea Mkuu wa Wilaya, yamesababisha angalau kidogo miradi ya Halmashauri tunaanza kuiona.

Mheshimiwa Spika, nitagusia upande wa TAMISEMI. Najua maeneo mengi sana yamesemwa kuhusu wizi na ubadhirifu, lakini nataka kusema kwenye TAMISEMI na Halmashauri kwa sababu nilikuwa Mjumbe kwenye Kamati ya *LAAC,* na tuliyaona mengi sana na mengine leo yanajirudia yale yale. Tulikuwa na Mwenyekiti wetu, mama pale katika Kamati ya *LAAC*.

Mheshimiwa Spika, nina imani sana na Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Mchengerwa. Kwa kweli, kwa dhati ya moyo wangu nina imani naye sana kwamba atafanya mabadiliko. Kwa nini nina imani na Mheshimiwa Mchengerwa? Kwa sababu, ameteuliwa tu, ameenda kule Lindi na Mtwara akazitaja Halmashauri ambazo miradi mibovu na miradi haiendi. Hata sijamlalamikia, hata sijamwambia, kataja huko kwenye vyombo vya habari, nikasema eh, Waziri ndio huyu sasa tumempata. Basi hatua zitachukuliwa na tutaona mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kule kwangu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wameiba mpaka vile vifaa vya maafa ya mafuriko ulivyonipa. Mimi nimepata mafuriko Ifakara, nimekuja kwa Waziri Mkuu nimelia, naomba magodoro, naomba sufuria, naomba mablanketi. Mheshimiwa Jenista Mhagama akaniambia nakusaidia, Waziri Mkuu kaniambia nikusaidie. Nimeenda bohari, nimepakia vifaa, magodoro, blanketi, sufuria, na kadhalika, nimeendanavyo mpaka Ifakara. Namwambia Mkurugenzi,

tugawie watu waliopata mafuriko vifaa hivi. Wameiba katika stoo ya Halmashauri bila kuvunjwa kwa stoo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nimemwambia *DC* wetu Dunstan Kiwobya akahakikisha, akathibitisha. Watu wameandikiwa barua rudisheni kimya kimya. Vingine Naibu Waziri wa Uchukuzi pale, Rais wa *RedCross,* Mheshimiwa David Kihenzile, *RedCross* nao walinipa, wameiba. Vifaa vya maafa wameiba Ifakara.

Mheshimiwa Spika, ukisema, chuki, na Wakurugenzi wengine wanaingia kwenye siasa wanasema huyu tunamsubiria 2025 tutashughulika naye. Wameiba. Hakuna mtu yeyote ameenda Polisi, magodoro yale na mablanketi yale yana ubora wa namna yake, wanaambiwa warudishe yale ya dukani hayaeleweki. Fuatilieni mtaona, hakuna hatua iliyochukuliwa. Kwa hiyo, nasema kwa dhati kwamba, nina imani na Mheshimiwa Mchengerwa kwa sababu bila kukwambia uliitaja Halmashauri yangu kuzembea katika miradi, kukamilika katika miradi nikajua utachukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili nikwambie, Mheshimiwa Rais na Wizara mmetuletea shilingi milioni 528 za kujenga sekondari. Mmeleta tarehe 25 mwezi wa Sita, juzi ndiyo ujenzi umeanza. Hakuna hata wiki. Ukifuatilia unaambiwa wanabishana wampe mkandarasi huyu, wampe mkandarasi huyu, mradi haujakamilika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nafikiri …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asenga, ngoja nielewe vizuri hapo. Hizo ni hoja zako ambazo unataka Serikali isikie ama ziko kwenye taarifa ya *CAG?*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, zipo kwenye taarifa. Nataka kusema kuhusu ubadhirifu katika Halmashauri ambazo Taarifa ya Kamati ya *LAAC* imesema hapa kuhusu kuchelewa kwa miradi na ubadhirifu katika Halmashauri. Ndiyo ninachokisema.

**SPIKA:** Haya.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Kwa hiyo, hiyo ni mifano nimetoa kwenye jimbo langu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, nimetoa mifano ili kuthibitisha ukweli wa Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa, mifano ndiyo hiyo. Miradi inachelewa. Kamati imesema, nami natoa mfano Ifakara mradi hela zimepelekwa tarehe 25 mwezi wa Sita, mradi umekuja kuanza tarehe 15 mwezi wa Kumi ambapo ndiyo tarehe ya mwisho kwa mradi kukamilika. Kwa namna hii hatuwezi kufika, hatuwezi kuendelea.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema suala la vikao na sisi kuwa Wajumbe wa Kamati za Fedha na Mabaraza ya Madiwani. Waziri Ummy akiwa Waziri wa TAMISEMI hapa, hii hoja imetolewa hapa, alitoa maelekezo kwamba ni vizuri Wakurugenzi wakaongea na Wabunge wao namna ya kuandaa vikao hivi. Jambo hilo halijafanyika, lakini leo tunaweza tukawajibishwa sisi kwamba ni Wajumbe wa Kamati za Fedha, Wajumbe wa Mabaraza ya Madiwani, lakini wewe unatupangia hapa ziara za Kamati, unatupangia Bunge lako, kwa nini vikao hivi visifanyike hata *weekend* kwa umuhimu wa sisi kushiriki ili tuseme?

Mheshimiwa Spika, vinginevyo nataka nikwambie, kama hatuingii kwenye Kamati za Fedha hizi, na watu wanapanga ratiba tofauti na Bunge, wana malengo yao. Siyo kwamba watu hawajui kwamba kuna siku moja inaweza ikapatikana Mbunge akapata nafasi akashiriki Kamati ya Fedha, akashiriki Baraza la Madiwani, wanapanga wanajua, Mbunge akiwa hapa hili hatakubali. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa inatoka wapi? Mheshimiwa Mtaturu.

**TAARIFA**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba, sehemu pekee ambayo tunashirikishwa Wabunge ni kipindi ambacho Halmashauri zinaitwa kwenye Kamati ya *LAAC* na *PAC*. Hapo ndiyo tunashirikishwa vizuri sana na tunaweza kushiriki ili kwenda kuchangia mawazi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, unapokea Taarifa hiyo?

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa mikono miwili. Pia, hata vile vikao kimoja kimoja unachovizia ama Katibu wako anaenda kwenye Baraza la Madiwani, maana Kamati ya Fedha hata Katibu wako haruhusiwi kwenda. Wanasema Mbunge mwenyewe uwepo. Sasa wakichengesha ile tarehe huwezi kushiriki, watu wameshapitisha mambo kule. Unakumbuka Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa, *Comred* Abdulrahman Kinana, katika semina alituambia, katika mambo muhimu ya Mbunge kufanya ni kutokupoteza hii Kamati ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, haya la pili, makabrasha hayo yanakuja lini? Kabrasha unaletewa kama nyumba hivi, siku moja, labda saa sita, kesho kikao. Utapitia nini, utaacha nini?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunachoomba ni kwamba, wanapoandaa hivi vikao washirikiane nasi, tupate makabrasha kwa wakati, tujue tukienda kwenye Kamati ya Fedha tunapitia nini na tukienda kwenye Baraza tunapitia nini? Wako Madiwani wazuri sana. Sio Madiwani wote wanahusishwa ama wanatuhumiwa na kadhalika, lakini wako Madiwani ambao ni wazuri, wanasimamia, lakini baadaye wanaitwa wanaambiwa mradi wako utahamishwa, sijui nini, wanatishiwa na hatimaye unakuta, ile kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba Madiwani chukueni hatua, fanyeni kazi yenu, inakuwa inakwama.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Kihenzile, atafuatiwa na Mheshimiwa Judith Kapinga, na Mheshimiwa Nape Nnauye ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii ya kuweza kuchangia katika mjadala unaoendelea. Pengine nitajikita zaidi kwenye hoja ile ambayo inazungumzwa ya ongezeko la gharama kwenye *lot 3* na *lot 4* na nafasi ikitosha, basi nitaendelea na mengine.

Mheshimiwa Spika, moja ya hoja ambayo imezungumzwa ni kwamba, tulipotumia *single source,* taarifa yetu ya uchukuzi, tulipotumia *single source* gharama zilizongezeka *by 1.3 million* na *1.6 million per kilometer.* Kabla sijaanza hata kujibu au kuingia kwenye kuchambua, *logic* pia nyepesi kabisa, unapojenga mradi mbali kutoka Dar es Salaam, unapoenda mbali zaidi gharama za usafiri na vitu vingine zinaongezeka. Hiyo ni kwa lugha nyepesi kabisa, lakini kwa kuwa imezungumziwa hoja ya kwamba ni kinyume na sheria za manunuzi, napenda pia kuzungumzia kwenye sheria yetu ya manunuzi Na. 7 ya mwaka 2011 na kanuni zake ambayo imetoa fursa na mazingira gani unayoweza kutumia *single source.*

Mheshimiwa Spika, ukienda Kifungu cha 161 (c), imeeleza kwa kirefu sana, lakini mojawapo ni kwamba, pengine kama mtu huyo yupo *site* au mmeona kuna faida kubwa ya kufanya hivyo. Tayari mkandarasi aliyekuwa anajenga *lot 1* na 2 moja alikuwa *site,* pili alikuwa na mitambo, tatu Mradi wa *lot 3* na 2 alikuwa ameshafika asilimia 97 na 95 *respectively.* Kwa hiyo, kwa wakati huo ilikuwa ni muhimu pengine kumtumia.

Mheshimiwa Spika, pengine wakati naendelea na hilo, kabla hatujachambua *lot No. 3* na *No. 4*, hebu tuchambue gharama za *lot No. 1* na *No. 2* zimefanana ili tuweze kujenga hoja kumbe gharama za Na. 3 na Na. 4 kwa nini ziliongezeka? Ukienda kwenye Na. 1 na Na. 2 zilitofautiana kwa karibu dola 500,000 na

sababu zilikuwa ni nyingi. *Lot No. 1* inatoka Dar es Salaam mpaka Morogoro, ya pili inatoka Morogoro mpaka Makutupora. Na. 1 haikuwa na mahandaki, *lot No. 2* ilikuwa na mahandaki karibu kilometa tatu. Hivyo usingetegemea zifanane. Pia, *lot No. 2 vis-a-vis No. 1* ilikuwa inapita kwenye Mto Kondoa, kwa ambao ni wenyeji, pembezoni, jambo ambalo litakutaka katika eneo kubwa sana ujenge madaraja. Sasa katika hali hiyo, kama namba I na II hazikufanana, kwa nini tuseme Na. 3 na Na. 4 zifanane?

Mheshimiwa Spika, Na. 3 na Na. 4, tofauti za bei, *it is very obvious,* yako mambo kama 11, lakini kwa sababu muda leo ni mdogo naomba nitaje machache:-

Mheshimiwa Spika, nilisema na jana *lot No. 3* na *No. 4* inategemea kupita kwenye *rift valley* karibu kilometa 50 wakati lot *No. 1* na 2 haina bonde la ufa. Gharama zitatofautiana. *Lot No. 3* na *No. 4* zina *junction* kubwa ambapo pale tunajenga karakana yetu, lakini pia tunakwenda kujenga Chuo cha Reli Tabora, *center* ya *excellence* ya Reli itakayohudumia karibu nchi zote za Afrika. Katika hali ya kawaida haiwezi kufanana na *Lot No. 1* na *No. 2* ambako kitu hicho hatuna.

Mheshimiwa Spika, ukiacha hilo, tunakwenda kujenga kituo kikubwa cha mizigo ambacho kinaunganisha karibu pande tatu. Kinaunganisha upande wa Dar es Salaam, reli inayokuja Dar es Salaam, inayokwenda Kigoma na inayokwenda Mwanza. Hii kwenye lot *No. 1* na *No.* 2 hazipo. Ni vizuri Watanzania wakafahamu katika mazingira hayo haziwezi kuwa sawa.

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, eneo la Malongwe na Nyahua, wenyeji wa hapa wapo watanisaidia, karibu kilometa 40 inapita kwenye *swamp.* Huwezi kufananisha reli unayoijenga kutoka Dar es Salaam kupitia Pwani na ambayo inapita kwenye *swamp.* Kule kwenye *swamp* utajenga madaraja, utajenga makalavati, utainua matuta, kwa nini tunafikiri kwamba gharama zitakuwa sawa sawa? Ni vyema Watanzania wakalifahamu hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, kati ya Salanda na Manyoni kuna miinuko miwili…

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa David Kihenzile, kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mpina.

Mheshimiwa Naibu Waziri, kaa kidogo.

**TAARIFA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, la kwanza, haya yote anayoyaongea Naibu Waziri, Mheshimiwa Mkaguzi wetu aliyakataa.

Mheshimiwa Spika, la pili, anachozungumzia kuhusu suala la mazingira ya mradi wa kutoka Morogoro kuja Makutupora…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, Taarifa ni moja.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, basi niiweke hiyo moja.

**SPIKA:** Haya, ahsante.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, hiyo moja …

**SPIKA:** Aah, umeshasema ya kwanza.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Aah, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa David Kihenzile unaipokea Taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, namwomba tu aendelee kunisikiliza kama nilivyokuwa namsikiliza huko nyuma. Taarifa yake naikataa, kuweka *record* vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sawa. Sasa ngoja niweke sawa.

Waheshimiwa Wabunge, hoja hii ni ya Kamati zetu tatu. Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri kwenye hoja hii ni wachangiaji kama mchangiaji mwingine. Kwa hiyo, inaruhusiwa kutoa Taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa David Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda ni mdogo, naomba niseme jambo moja muhimu sana kwa kuhitimisha kabla sijaendelea pengine.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, *engineering estimate* ambazo zinatumika kwenye mradi huu zilifanywa kati ya 2012 na 2016.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Ngoja. Mheshimiwa Halima, sasa hapo utakuwa unanipa mimi Taarifa kwa sababu, ndiye niliyetoka kuzungumza.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, alikuwa ameshaanza.

**SPIKA:** Ngoja achangie halafu utapewa, maana la sivyo, utakuwa unanipa mimi Taarifa.

Mheshimiwa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilitaka niwarejeshe Waheshimiwa Wabunge…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** …kwenye Ripoti ya *International Union of Railways,* yaani Taarifa ya Reli Duniani. Ni

vizuri tukaelewana hapa, tukasikilizana kwa faida yetu sisi kama Wabunge pamoja na Waheshimiwa wananchi.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Kumbe inauma!

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, katika ripoti hiyo, imeainisha na ninaomba tutembee kifua mbele Watanzania; imeainisha Barani Afrika zimejengwa kilometa 7,200 katika hizo, 2000 ni za Tanzania. Katika mchanganuo…

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Kihenzile kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee.

**TAARIFA**

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kuhusiana na *SGR* na kwa mujibu wa mahojiano ambayo Kamati ya *PAC* imefanya kuhusiana na *SGR,* tumeambiwa wazi kwamba, mlilazimika kumpa mkandarasi *Yapi Markezi,* huyo Mturuki kwa sababu ya masharti ya Benki ya *Standard Chartered.* Masharti ya mikopo ndiyo yamewalazimisha mfanye maamuzi ambayo hayana maslahi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Taarifa ni moja Mheshimiwa.

Mheshimiwa David Kihenzile, unaipokea Taarifa hiyo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa hiyo ninaikataa kwa sababu, haipo sehemu ya mjadala wangu. Tulimpa huyo baada ya kujiridhisha na vigezo vya Kitaifa. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninaendelea kwa sababu, nimekuwa Mwenyekiti, huwa ninafahamu taratibu na Kanuni.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kuweza kuniruhusu. Nataka nitoe taarifa ya hali ya ujenzi wa reli Barani Afrika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ngoja.

Mheshimiwa Anatropia, unatakiwa usubiri kidogo kwa sababu, sasa utakuwa unampa Taarifa juu ya nini? Maana la sivyo, utakuwa unampa Taarifa Mbunge mwenzio. Kwa hiyo, unamwacha achangie kidogo ndiyo umpe Taarifa kwenye hiyo hoja yake.

Mheshimiwa David Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Nilitaka kuzungumza kwamba, katika kilometa 7,200 karibu kilometa 2,000 zimejengwa Tanzania. Mataifa mengine wanakuja kujifunza tumefanyaje Watanzania?

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, katika gharama, Tanzania tumejenga kwa gharama ndogo ya shilingi *4.3 million per kilometer.* Nchi nyingine ni kama ifuatavyo: Nigeria *6.1 million,* Kenya milioni 7.3, Ethiopia milioni 5.9, Morocco *6.5 million,* sisi ni *4.3.* Tutembee kifua mbele tujisifu, Mheshimiwa Rais Samia anatuongoza vizuri. Huko tunakoenda ni kuzuri zaidi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kihenzile kwa sentensi yako naona hujamaliza, nataka kukuongeza dakika moja ili umalizie mchango.

Mheshimiwa Anatropia, Taarifa gani?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nataka kumpa Taarifa, hoja ya *CAG* ni ku-*award* kandarasi bila kufanya ushindanishi, *single source*. *Single source* ambayo angepaswa kuifanya ingekuwa na *economic value*. Mkaguzi amejiridhisha kwamba, ame-*award* bila kuwa na *economic value*. Hiyo ndiyo hoja yetu.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Kihenzile, dakika mbili, malizia mchango wako na kama unaikubali hii Taarifa au hapana.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Taarifa ninaikataa kwa sababu nimeshasema mwanzoni kwamba sheria inaruhusu. Tunaongelea sheria ya nchi. Kama nchi saba zimejengwa kilometa 7,200 na zinakuja Tanzania kujifunza tumejengaje kwa *4.3* dola kwa kilometa moja, kwa nini Watanzania tusijivunie mambo mazuri?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Kwa nini msiyafurahie?

Mheshimiwa Spika, tutembee kifua mbele kwa sababu tumejenga reli kwa gharama ambazo ni nafuu ukifananisha na wengine. Hilo ni moja. Pili, *engineering estimate* ambayo tumejengea reli zetu iko chini. Kwa mfano, wakati *engineering estimate* ya *lot No. 3* ilikuwa ni *4.9,* tumejenga kwa *4.05* wakati ile ya *lot No. 4* ilikuwa ni *4.8* tumejenga kwa *4.3.* Kwa hiyo, tuko vizuri, tutembee kifua mbele, tujidai, miradi iko kimikakati, wengi wangetamani kuwa kama sisi, tujivune, tuchape kazi. Tumuunge mkono Rais wetu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mbunge akisimama kuchangia hawezi kupewa Taarifa zaidi ya tatu. Maana sasa zitakuwa siyo Taarifa tena. Kwa hiyo, Wabunge watatu walikuwa wameshampa Taarifa Mheshimiwa Kihenzile.

Mheshimiwa Judith Kapinga, atafuatiwa na Mheshimiwa Nape Nnauye. Mheshimiwa George Simbachawene, ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Awali ya yote naomba kuanza kwa kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya na

uwekezaji mkubwa anaoufanya kwenye Wizara yetu kupitia sekta ndogo tunazozisimamia za umeme, mafuta na gesi.

Mheshimiwa Spika, pili, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Naibu Waziri Mkuu, Dkt. Doto Mashaka Biteko, kwa kazi nzuri anayoifanya kwenye Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, tatu, napenda kukupongeza Mheshimiwa Spika, pamoja na Kamati kwa kazi nzuri ambazo mmefanya ya kuhakikisha kwamba mnatupa maelekezo na kutusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nne, napenda kumpongeza Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya katika kuangazia masuala yanayofanywa na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa pongezi, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuonesha uzalendo kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya pongezi hizo napenda sasa nitolee ufafanuzi baadhi ya hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezizungumzia. Moja, kuhusiana na kampuni tanzu ya shirika letu la petroli, *TPDC (TANOIL)*. Kampuni hii pamoja na historia ya huko nyuma, ilianza biashara mwaka 2021. Pamoja na majukumu ambayo wamepewa, kampuni ya *TANOIL* ilipewa jukumu la kununua mafuta lakini vile vile kuuza mafuta kwa wafanyabiashara wadogo, wafanyabiashara wa rejareja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafuta kwa Taifa letu ni uchumi. Kwa hiyo, kama Serikali isingewezekana kuwachia wafanyabiashara binafsi watawale soko kwa asilimia 100. Ninyi mnafahamu, Watanzania hawa ni watu masikini. Takribani Watanzania milioni 26 wanaishi chini wa mstari wa umasikini. Kwa hiyo, isingewezekana kwa Serikali makini kuachia soko la mafuta, soko ambalo linabeba uchumi wa Taifa hili liweze kutawaliwa na sekta binafsi peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo lazima kama Serikali tuhakikishe tuna sehemu kwenye soko la mafuta ili kulinda hali za Watanzania.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Simama kwa ajili ya taarifa. Mheshimiwa Mohamed?

**TAARIFA**

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

Mheshimiwa Spika, nataka kumpa taarifa Mzungumzaji. Hatukuanziasha shirika hili kufanya wizi. Tumeanzisha shirika hili kuja kufanya biashara. Mpaka sasa hivi shirika hili lina hasara kubwa. Huyo anayezungumza atueleze, hii ripoti ya mkaguzi ni sawa ama si sawa? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, siipokei na nadhani nikimaliza kuongea Waheshimiwa Wabunge watakuwa wamenielewa, kwa sababu ndiyo kwanza nipo kwenye *introduction*. Subiri kidogo Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wote tunafahamu kama nilivyosema mafuta ni uchumi. Kwa kweli, adhma yetu kama Serikali ni kuhakikisha tuna sehemu kwenye soko la mafuta ili tuendelee kulinda hali za Watanzania. Ninyi mnafahamu, mwezi wa saba tulipata dhoruba ya kukosekana kwa mafuta katika Taifa letu. Wafanyabishara binafsi walikataa kuwauzia wafanyabiashara wa rejareja mafuta. Walileta mafuta kwa ajili ya kampuni zao. *TANOIL* ndiye aliyeagiza mafuta na kuweka mafuta kwa wafanyabiashara wa rejareja ambao wanawauzia mafuta watumiaji wa mafuta kwa asilimia 70. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, … *(Makofi)*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mheshimiwa Judith Kapinga, kuna taarifa kwa Mheshimiwa Mbunge wa Kibamba, Mheshimiwa Mtemvu.

**TAARIFA**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, anavyoendelea kuzungumza anatuchanganya kidogo. *Underpriced* ambayo imefanywa na *management* ya *TANOIL* kwa shilingi 70, imesababisha *economic wealth* ya shilingi bilioni 53. Yaani wasingefanya kushusha hivyo, tungeweza kuokoa shilingi bilioni 53. Pia, kwa sababu unasema sababu ni *market*…

**SPIKA:** Mheshimiwa, taarifa ni moja.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, sababu ni moja hiyo hiyo, kwamba ni *market penetration* ndiyo maana wakawauzia wafanyabiashara wadogo. Ukweli ni kwamba, aliyeuziwa ni mmoja tu. Kituo cha mafuta kimoja tu. Hivyo ndivyo tulivyoambiwa na *CAG*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, taarifa hii siipokei na kwenye ukweli lazima tutasema ukweli juu ya umuhimu wa *TANOIL*. Ninapoelekea mbele nitasema changamoto na hatua ambazo kama Serikali tumechukua. Pamoja na kazi ambayo *TANOIL* imefanya, zipo changamoto ambazo zimejitokoza. Wote tumeona, watumishi wasio waaminifu na wafanyabiashara wasio waminifu waliunda mtandao kwa ajili ya kuhujumu masuala yanayofanyika na *TANOIL*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpaka sasa tunavyoongea, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutuongoza, alishaanza kuchukua hatua. Kwa upande wa watumishi, pamoja na watumishi wale kukaa kando, jana Mheshimiwa Waziri wa Nishati ameshapokea taarifa kutoka kwa TAKUKURU ya kwamba, wameshakamilisha uchunguzi na watumishi wale watapelekwa Mahakamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, sisi tumechukua taratibu za ndani.

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa watu hawa ni watumishi, kwa taratibu na sheria ambazo tulizitunga sisi wenyewe, tumeshaanza utaratibu wa ndani ili kuhakikisha watumishi hao kwa kufata sheria, tunawaondoka kwenye utumishi. Wakiwa wanaenda Mahakamani, waende kushtakiwa wakiwa raia wa kawaida. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Condester Sichalwe.

**TAARIFA**

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya *PAC*. Taarifa tuliyowasilisha hapa, ni ambayo sisi Kamati tumejadili tukiwa na *CAG* mwenyewe na tukiwa tumewaita hao watu wa *TANOIL*. Anachotueleza Mheshimiwa Naibu Waziri, kinakinzana na kile ambacho kwenye majadiliano yetu tumejadiliana na *CAG* na tumewahoji wale watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunataka kujua, tuitishe *Hansard* zije hapa kwa sababu Kamati yetu ni *Oversight Committee*. Tunazo taarifa ambazo tumewahoji wale watu mbele ya *CAG*, wakatujibu na hiki ambacho anatujibu kinakinzana. Tushike kipi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Judith Kapinga, unaipokea taarifa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, sipokei kwa sababu nimeongelea masuala kadhaa… *(Kicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hakuna taarifa juu ya taarifa. Mheshimiwa Judith Kapinga.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ameongezea masuala kadhaa, sasa sijajua mahsusi alikuwa anazungumzia eneo gani. Tumechukua hatua kama ambazo nimezisema lakini vile vile kuendelea mbele, suala hili lina sehemu mbili. Lina suala la watumishi na lina suala la wafanyabiashara. Wafanya biashara wale kwa mtandao wao, ndiyo ambao wamekubali kuchukua *discount* nje ya utaratibu. Vilevile, wamekuwa na madeni makubwa ambayo wamegoma kuyalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, kupitia Bunge lako Tukufu naomba niwataarifu…

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**….kwamba kama ni mtumishi kama ni mfanya bishara anayehusika, wote hawako salama na tutachukua hatua kwa pande zote mbili. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakasaka, nadhani ameshapewa taarifa tatu. Ameshapewa taarifa na Wabunge watatu tayari. Mseshimiwa Judith Kapinga.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, hatutaishia kwa watumishi kama nilivyosema. Mfanyabishara yeyote ambaye anafahamu amenufaika kwa *discount* ambaye anafahamu amechukua mafuta bila kulipa, tutachukua hatua. Kwa kumalizia, nafahamu baada ya leo hii simu zitakuwa nyingi. *Message* zitakuwa nyingi, vi-*note* vitakuwa vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie hatutaangalia. Msumeno ambao umewakata watumishi, ndiyo msumeo ambao utaenda kuwakata wafanya biashara bila kuangalia ni nani. Baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Unatokea wapi Mwongozo? Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ninaomba Mwongozo wako. Tunachojadili hapa ni taarifa ya *CAG*. Kinachonichanganya ni kwamba sasa tunatoka nje. Tunapokea majibu kutoka kwa wafanyabiashara mara hivi mara hivi. Amesimama Mjumbe wa Kamati hapa, anasema hiki ndicho tulichojadili kwenye Kamati, kinakinzana na majibu tunayopewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa, tunaomba kwa ule ule kama upande wa pili watakuwa na hoja nyingine kama ulivyokuwa unatuongoza sisi, alisimama Mbunge mmoja hapa rafiki yetu akatoka hoja ukamwambia, kama ana hoja nyingine tofauti na kwa *CAG* basi utampa nafasi baadaye alete hoja hiyo. Tunachoomba hapa tujibu kwenye hoja ya *CAG*. Ama uikatae hoja ya *CAG* twende hatua nyingine. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza niseme huo ndiyo uhalisia, ndicho kinachotakiwa. Kwa sababu, kinachojadiliwa sasa hivi na Bunge ni hoja zilizoletwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, si rahisi sana Spika akajua kila kitu. Ni mpaka akijua kile ambacho kimeenda kidogo nje atajua. Kwa sababu Mheshimiwa Judith Kapinga alikuwa anataja *TANOIL* na *TANOIL* ndiyo iko kwenye hoja. Kwa hiyo, ni ngumu sana mimi kujua hiki anachoeleza kiko nje ya ile hoja ya *CAG*. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huo ndiyo utaratibu. Hoja inayojadiliwa hapa ni hoja ya *CAG* na tujielekeze huko. Kwa sababu, tukijielekeza nje hayo maelezo yatakuwa nje na hata Wenyeviti wetu wa hizi Kamati tatu kama nilivyosema, wanaokuja kuhitimisha hizi hoja baada ya huu mjadala ni Wenyeviti wa Kamati. Kwa hivyo, hoja zote zinazochangiwa wao ndiyo wanakuja kutoa ufafanuzi wa

hoja lakini pia kutueleza maazimio baada ya michango hii. *(Makofi)*

Maana yake ni nini, ukisema jambo nje ya hapo wao siyo Serikali, hawawezi kukujibu. Ndiyo maana nilimweleza Mbunge kutoka Ngorongoro, kwa sababu hawa Wajumbe, yaani hawa Wenyeviti watatu hawawezi kujielekeza kwenye hoja hiyo maana hawafahamu. Kwa hiyo, nia ni hiyo na huo ndiyo mwelekeo. Hoja inayojadiliwa ni ya *CAG* lakini Serikali inapotoa ufafanuzi, na yenyewe ipo katika mchango yaani katika kuchangia hoja za Kamati. Kwa hiyo, na wao wanapaswa kuchangia hoja za Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Judith alikuwa ameshamaliza muda wake na …

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**SPIKA:** Unatokea wapi?

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, huku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mohamed.

**MHE. MOHAMED SAID ISSA:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 76, naomba Mwongozo wako. Mheshimiwa Naibu Waziri amesema hapa kwamba, haitaishia hapo, hata wale wafanyabiashara ambao wamepewa *discount* nao watakamatwa. *Discount* katika biashara ni jambo la kawaida. Kwa hiyo, sidhani kwamba ni halali mfanyabiashara kupewa *discount* halafu akawa yuko kwenye makosa. Naomba Mwongozo wako kwa hili. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza wakati akitoa taarifa Mheshimiwa Condester, amesema hizi hoja zingine zilizosemwa na Mheshimiwa Judith Kapinga, haziko kwenye hoja

ya *CAG*. Sasa, nataka hapa ili nijue natoa Mwongozo gani. Kwenye hoja ya *CAG*, wale Wajumbe wa Kamati ya *PAC*, hoja ya *discount* kusababisha ile hasara ya mabilioni yanayotajwa, ipo ama haipo? Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*. *(Makofi)*

**MHE. JAPHET N. HASUNGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):** Mheshimiwa Spika, hoja ipo kwenye taarifa yetu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Hoja ipo. Kama hoja ipo basi ufafanuzi alioutoa Mheshimiwa Judith Kapinga kwenye hoja hii uko sawa sawa. Kwa hivyo, Mwongozo kwa hiki nilichoombwa kama hili jambo linaruhusiwa ama haliruhusiwi. Kama *CAG* kalileta, maana yake hizo *discount* zilitolewa bila kufuata utaratibu na ndiyo Serikali inasema kupitia Naibu Waziri kwamba, watachukua hatua. *(Makofi)*

Sasa, sisi kazi yetu kama wasimamizi wa Serikali ni kuchukua hayo wanayoyasema, maana baadaye tutahitaji taarifa juu ya haya. Kwa hiyo, maadamu hoja hiyo ipo kwenye taarifa, ufafanuzi alioutoa Mheshimiwa Judith Kapinga uko sawa sawa. Kwa hiyo, unaruhusiwa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Wahehsimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, atafuatiwa na Mheshimiwa George Simbachawene. Mheshimiwa Prof. Mbarawa ajiandae.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye hoja tatu zilizoko Mezani. Pamoja na kukupongeza kwa kazi nzuri ya kuliongoza Bunge na kuaminiwa na dunia, umeiheshimisha sana nchi yetu. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri aliyofanya ya Kidiplomasia ambayo kwa kweli ndiyo imejenga msingi wa Tanzanaia kuendelea kuaminiwa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazipongeza ripoti zilizowasilishwa Mezani za Kamati zetu, ripoti zote tatu. Wamefanya kazi nzuri. Najua walikuwa wanakesha, wanahangaika kuhakikisha ripoti zinafika

hapa. Nichukue nafasi hii kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na ofisi yake. Wanatufanyia kazi nzuri sana. Kwa siku tatu nimeona uzalendo wa Wabunge hapa, jinsi wanavyopiga kelele, jinsi wanavyohangaika kuhakikisha kwamba, nchi yetu inatendewa haki kwenye kusimamia rasilimali za nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huu ni ushahidi kwamba Chama cha Mapinduzi kinalea vizuri, kwa sababu Wabunge wengi ni wa CCM. Ripoti zi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali zimekuwepo kwa muda na mimi nimepata bahati ya kuzipitia sana. Nikiwa Katibu Mwenezi, tulikuwa na utaratibu zilikuwa zinaletwa pia CCM, tunazipitia. Nimekuwa Mbunge hapa mwaka 2015 na sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja kubwa kwenye hizi ripoti, toka zimeanza kuletwa na toka zimeanza kufanyiwa kazi kwanza, kuna kazi kubwa sana ambayo imefanyika ya kuboresha mambo kwa kuzitumia hizi ripoti. Ndiyo maana ukienda kuangaliwa takwimu zinaonesha kwamba, kule yako matatizo yaliyokuwa yanatokea ambayo leo hayatokei. Ukiangalia ripoti baada ya ripoti yako mambo mengi sana yamebadilika. Hati safi zimeongezeka. Baadhi ya *query* ambazo zilikuwa zinatokea nyuma, nyingi zimerekebishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi Waziri nasimamia *TEHAMA*.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Moja ya uamuzi wa kwenda kushushughulikia makusanyo ya Serikali kwa kuweka TEHAMA, yametokana na ripoti za CAG katika mkakati wa Serikali wa kuziba myanya ya kupotea kwa mapato ya Serikali.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** …Nilichokuwa nataka kusema ni kwamba, ripoti hizi zina manufaa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa Mzungumzaji anayeeleza vizuri. Kwa mujibu wa *CAG* anasema, "Hizo hati zimebadilika kwa sababu wezi wamejua namna nzuri ya kuiba au kutumia risiti kuwasilisha vielelezo." Kwa mujibu wa *CAG* wanawasilisha vielelezo hata baada ya kufanya wizi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape Nnauye, unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo. Mheshimiwa Nape subiri kidogo, inaonekana kuna Kanuni imevunjwa hapa.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nimesoma ripoti tatu, zina kurasa 889. Mheshimiwa amesema hapo kwamba, *CAG* amesema kwamba, hati safi zimepatikana baada ya wizi kuanza. Naomba kiti chako kielekeze kama anaweza akatuonesha hiyo sehemu kwenye *CAG Report*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kitila Mkumbo, kwa sababu hapa ni jambo la Kanuni kuvunjwa, kwa hiyo Mbunge anasema uongo? Ili tujue tunajielekeza kwenye Kanuni gani, nitoe utaratibu.

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ni uongo kwa sababu hicho kitu kwenye ripoti hakipo. Atuthibitishie na napata Kanuni sasa hivi nitai-*cite* Kanuni hapa. Naitafuta.

**SPIKA:** Hakuna neno. Waheshimiwa Wabunge tutaenda tutaenda. Hakuna neno. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa Mujibu wa Kanuni ya 71 ya …

**SPIKA**: Hakuna neno. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri amesema amesimama hapo kwa mujibu wa Kanuni ya 71 ambayo inazungumza kuhusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Kwa sababu ametaja neno uongo, nadhani kuna Kanuni inayohusu hapo. Kanuni ya 70 ndiyo inahusu uongo na hakuna neno. Nia tu nataka kutengeneza. Hakuna shida, tunataka kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, hakuna shida mtu akitaja 71 wakati ni 70. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa tusikilizane, nimesimama.

Kanuni ya 70 inazungumza kuhusu kutokusema uongo na inaruhusu Mheshimiwa Mbunge kusimama mahali pake na kusema Kuhusu Utaratibu. Fasili ya tatu inasema Mbunge huyo baada ya kuruhusiwa ataeleza hayo maelezo ambayo yanaeleza uwongo unatokea wapi. Kwa ujumla ukiisoma Kanuni hii inataka yule aliyesema kwamba Mbunge mwingine anasema uongo ndiye athibitishe, huo uongo wa huyo Mbunge. *(Makofi)*

Sasa kwa muktadha huo, Mheshimiwa Kitila Mkumbo, alivyosimama hapo ameeleza kwamba katika taarifa zilizopo yeye hajaliona hilo jambo ambalo Mbunge amelisema; kwa maana ya kwamba wale wezi wamejifunza utaratibu mzuri wa kutoa taarifa na kwa hivyo wanapata hati safi. Katika zile halmashauri ambazo zimepata hati safi, zipo ngapi Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC*? Ni hapa tu, unaruhusiwa kusimama na mimi nikiwa nimesimama. *(Kicheko)*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA LAAC:** Mheshimiwa Spika, kumi na tatu zimepata hati zenye shaka na 170 ndiyo zimepata hati safi.

**SPIKA:** 170 zimepata hati?

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika, hati safi. Zenye shaka ni 13, moja chafu.

**SPIKA:** twende kwenye safi 170. Kwa maelezo na kwa michango tuliyoanza nayo Alhamisi, jana na leo, kwa namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge, wameeleza halmashauri zao zilivyo na changamoto; hizi hati 170 ni hati safi; na huu unaoitwa wizi, ubadhirifu umetokea kwenye hizo halmashauri. *(Makofi)*

Hizi hati safi zimetolewa kwa muktadha upi; ni kwa maana ya kwamba zinakaguliwa kwa utaratibu ule wa kawaida na kwa utaratibu ule wa kawaida wamefuata taratibu za upelekaji wa taarifa kwa *CAG*. Kama hivyo ndivyo kwa takwimu hizi, pengine maneno sasa kwa sababu taarifa muda ni mfupi, kwa takwimu hizi zilizopo katika taarifa hii ya kamati na taarifa ya *CAG* ni dhahiri hawa wabadhirifu wamejifunza namna nzuri ya kutoa taarifa. *(Makofi)*

Kwa sababu kama hivyo sivyo, mimi nitachukua mfano mmoja tu na unaotokana na michango ya hapa ndani. Mfano mmoja tu, ukurasa wa 106 wa taarifa ya Kamati ya *LAAC*, halmashauri namba 16, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ina hati inayoridhisha. Hapa tumemsikia Mheshimiwa Mbunge wa Bunda, akieleza taarifa ya *CAG* ilivyoitaja Bunda kwenye mambo mengi ambayo hayaendi sawa sawa. Wametajwa kwenye kuzima *POS* na m kwenye mambo mengine mengi tu ambayo ameyaorodhesha hapa. Kwa hiyo mazingira hayo Mheshimiwa Kitila Mkumbo, inaniwia vigumu kusema Mheshimwa Mbunge kasema uwongo kwa sababu muktadha wa taarifa hii unaashiria hayo. *(Makofi)*

Waheshimiwa wabunge, sasa tunaendelea. Tuliishia ambapo Mheshimiwa Nape alikuwa anachangia, akapewa taarifa na Mheshimiwa Anatropia, katika kutoa zile taarifa ikaonekana kuna kanuni inavunjwa. Kwa hiyo hapa tulikuwa tunashuhurikia ile kanuni iliyovunjwa na kuhusu uwongo. Sasa tunarejea kwenye jambo lile la msingi ambalo ni kumuuliza Mheshimiwa Nape, kwa sababu ile hoja ya uwongo

tumeshaimaliza kazi yake. Mheshimiwa Nape, unaipokea taarifa ya Mheshimiwa Anatropia? *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme Waheshimiwa Wabunge, jambo tunaloliongea hapa linahusu maisha ya watu. Mimi ningewaomba sana, na hasa Waheshimiwa Wabunge wa chama change; nataka kuwaomba sana na kwa unyenyekevu mkubwa sana, kwamba tusiingize ushabiki kwenye jambo kubwa la maisha ya watu, nataka tutafute suluhisho. Mimi nimesema watu wanazungumza kwa uzalendo mkubwa sana hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimesikia mwongozo wako, tunayo ripoti ya *CAG*, *unless we are doubting* kazi ya *CAG*. Ametupatia kwa *numbers and* Waheshimiwa wabunge, *numbers speak clear*. Maneno yanaweza kuongea kwa sauti kubwa sana, lakini *numbers* zinaongea *very clear*. Hoja yangu ilikuwa rahisi na ndiyo maana sipokei taarifa ya Mheshimiwa Mbunge na mimi namheshimu sana dada yangu. Hoja yangu ipo *very clear* kwamba taarifa hizi, zimekuwa zikitumika na Serikali kuboresha mambo ya usimamizi wa shughuli za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nikatoa mfano; hapa tumezungumza habari ya *POS*, habari yakukusanya makusanyo kwa TEHAMA, tulifikaje huko? Yalianzia kwenye ripoti za *CAG* kuonyesha kwamba kunakuvuja kwa mapato ya Serikali. Tukasema katika kushughulikia tuweke mifumo ishughulikie huo wizi, ishughulikie huko kuvuja kwa mapato. Sasa ripoti ipo mezani, ipo *very clear unless we are doubting integrity* na uwezo wa *CAG* kuripoti kazi zake ndani ya Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama hilo ndiyo hoja *then* hoja yangu haipo…

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, lakini kama tunamuona huyu *CAG*, namba zipo wazi *CAG* ametueleza ukweli…

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, upo mezani na ndiyo tunaoujadili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nani alikuwa anasema taaarifa?

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Naambiwa Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, alisimama kwanza.

**TAARIFA**

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kumpa taarifa kaka yangu, kiongozi wangu, mtu mahiri sana, Mheshimiwa Waziri, kwamba katika mjadala huu hakuna ushabiki. Katika mjadala huu tunaoendelea nao tumeweka maslahi ya Taifa mbele, na tunajua kwamba tunashughulika na maisha ya watu, lakini vile vile tunashughulika kukomesha wizi na ubadhirifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili Bunge limejinasibisha kama chombo cha wananchi kushughulika na jambo hili. Kwa hiyo hatuna upande ilimladi mtu yeyote anashughulika na hili sisi tupo pamoja naye. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Nape Nnauye, unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, Kilumbe ni kaka yangu. Pia mimi nilikuwa kiongozi wake. Taarifa hii inamatatizo; *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** sawa. Mimi nina haki kama wabunge wengine. Mheshimiwa Spika, taarifa hii inamatatizo hapa, hivi kweli…

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, hivi kweli sisi Waheshimiwa wabunge, nimesikia maneno hapa jana kuna Mheshimiwa Mbunge, anasema nchi inakuwa. *Extent* ya nchi kufa, miradi yote inaendelea hakuna mradi uliyosimama. Kuna fedha zipo majimboni kwetu mara 10, mara 15, mara 20, nchi inakufa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo maneno tunayomwambia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, kuwa nchi inakufa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, aah! Jamani tusifike huko, mimi nasema tujadilini wizi, tutafuteni *solutioni*. Tusiweke ushabiki. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape. Waheshimiwa wabunge, Mheshimiwa Nape kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Halima Mdee.

**TAARIFA**

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika, naomba ni nukuu ili taarifa yangu ichukuliwe kwa kunukuliwa kwake "Uchambuzi wa jumla wa kamati umebaini kuwa, idadi ya halmashauri zilizopata hati zinazoridhisha zimepungua kutoka 176 iliyotolewa katika mwaka wa fedha 2021 hadi halmashauri 170. Hati zenye shaka, idadi imeongezeka kutoka halmashauri nane mwaka 2020 mpaka halmashauri 13". *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hati zinazoridhisha, zina-*drop*. Hati zenye shaka zinaongezeka, halafu tunasema mambo ni mazuri. *(Makofi)*

**SPAKA:** Sawa, ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunaomba aseme ya kwake katika *context* yake, asiseme kwamba mambo ni mazuri wakati tumeambiwa hapo mambo ni mabaya. Tujadili mambo kwa ubaya wake… *(Makofi)*

**SPAKA:** Ahsante sana, umeleweka Mheshimiwa…

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika, tutafute suluhu.

**SPAKA:** Mheshimiwa Halima. Mheshimiwa Nape Moses Nnauye, unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nilipoanza kuzungumza hii hoja ya utumiaji wa ripoti za *CAG* sikujikita kwenye mwaka mmoja. Mheshimiwa Halima, anatoa takwimu za mwaka mmoja. Na nimeanza nimesema nina bahati nimeziona taarifa nyingi sana nikiwa Katibu Mwenezi miaka sita, taarifa zote nimeziona. Nikiwa hapa Mbunge, tangu mwaka 2015 taarifa zote nimeziona. Ukichukua *cumulatively* ushauria ambao umekuwa unatolewa na *CAG* na Bunge, umekuwa unafanyiwa kazi ndi maana kuna-*improvement*, ndiyo hoja yangu niliyokuwa naisema hapa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, ahsante Mheshimiwa…

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, na mimi sisemi kwamba mambo ni mazuri kabisa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Sekunde 30 malizia mchango.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kuna matatizo na Waheshimiwa wabunge wana haki ya kuwa wakali kwenye matatizo hayo. Hoja yangu matatizo hayo hayajatupeleka kwenye *extent* ya nchi kufa, siyo sawa. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa…

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, matatizo yapo ndiyo kwamba eti…

**SPIKA:** Muda wako umekwisha, ahsante sana.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, leo tunafika mahali kwa hali ilivyo kazi iliyofanyika na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, mnasema nchi inakufa *serious*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Nape, muda wako umekwisha, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wa Spika.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mwongozo ni nani anayeomba?

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, upande wa huku, mwongozo.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nipo huku.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Mwenisongole.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. nimesimama hapa kwa kanuni ya 76…

**SPIKA:** Tujitahidi kuzungumza kwa kifupi.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako naona kama Waheshimiwa mawaziri hawatuelewi. Sisi tunapoijadili hii taarifa ya CAG, kwanza ni kwa mujibu wa sheria na ndiyo maana tupo hapa. Sisi tuna nia nzuri, ukweli kuna tatizo, sasa wao wanataka kutufanya sisi Waheshimiwa wabunge kama tuna bifu fulani na wao kitu ambacho siyo kweli, tatizo lipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wasipige mipira nje lazima watuelewe, kuna tatizo lipo…

**SPIKA:** Sawa, ahsante sana…

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Halmashauri yangu ya Mbozi imepata hati safi, lakini nimeomba *special audit* (ukaguzi maalum) madudu matupu yamekuja. Sasa hatuwezi kukaa kimya… *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, ahsante sana.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Waheshimiwa wabunge, nilisema mwanzo nirejee, hoja hizi tatu ni hoja za kamati, siyo hoja za Serikali. Kwa hivyo wanapochangia Waheshimiwa Mawaziri, wanatoa ufafanuzi kwenye mambo ambayo pengine yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa namna ambayo wao wanaona wanahitaji kutoa ufafanuzi na wanatumia haki yao kuchangia. Kwa hivyo kama inaonekana kama vile wao wanatetea, sijasikiliza michango ya wengi, lakini wengi nilivyosikia wanajaribu kufafanua hoja zilizotolewa na Waheshimiwa wabunge. *(Makofi)*

Hata wao kwa sababu wanatoka kwenye hizo halmashauri. Hata wao kwa michango hii mitatu sijui niliyosikia hapa, hata wao wanakubali kwamba kuna shida. Wanachojaribu kuonyesha ni kwamba katika shida hizo, sisi kama sehemu ya Serikali kuna hatua tumekwenda na kuna hatua tutakwenda. Kwa hivyo tupate tu huu muktadha wakusikilizana, lakini uzuri na wao wanapochangia na ninyi mnatoa taarifa. Kwa hiyo tuendelee kwa sura hiyo, isije ikaonekana huko nje kama vile Waheshimiwa Mawaziri humu ndani pengine wanatetea kwamba yale yaliyosemwa na CAG pengine siyo kweli, ama kwa namna moja au nyingine taarifa za Kamati zinasema jambo ambalo siyo kweli, Hapana, tusije tukatuma picha hiyo huko nje. Serikali iliyopo humu Bungeni inajaribu kuonyesha kwa upande wake kama sisi

tulivyoonyesha kwa upande wetu, Waheshimiwa wabunge. Kwa hiyo tusiwe na wasi wasi…

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPAKA:** Waheshimiwa wabunge, huo ndiyo mwongozo wangu kuhusu hoja ya Mheshimiwa Mwenisongole. Mheshimiwa Salome Makamba.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Nilikuwa nafuatilia mjadala wakati Waheshimiwa Mawaziri, wanatujibu. Mimi ningeomba mwongozo wako, kuna maneno ambayo Mheshimiwa Waziri, wakati anachangia aliyazungumza ambayo kiukweli kwanza yanashusha hadhi ya Bunge kinyume na Kanuni, lakini pili yanatukosea heshima sisi kama Waheshimiwa wabunge, na tatu yanatugawa. Mheshimiwa Waziri anasema sisi tunachangia kishabiki, Mheshimiwa Waziri anasema anawasihi Waheshimiwa Wabunge hasa wa Chama Cha Mapinduzi; anatugawa sisi kama Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anasema hili ni jambo la watu wanaoweza wakafa na wengine wakafanyeje, kama vile sisi tupo kwenye upande mwingine na wenyewe wapo upande mwingine. Mimi naomba mwongozo wako, kwa sababu mjadala unaendelea lakini…

**SPIKA:** Ngoja, ngoja, ili tuweke vizuri, nadhani Mheshimiwa Nape, neno kufa lilipotajwa alikuwa anazungumzia mchango uliyotolewa jana na Mbunge akisema kwamba Taifa hili, nadhani alisema *either* linaweza kufa ama linakufa kitu kama hicho. Kwa hivyo alivyotumia neno kufa, alikuwa anaenda huko, maana mimi nimemsikia labda kama kwa maelezo kuna sura ya namna hiyo basi alimaanisha hicho, ama siyo alimahanisha hicho, ndicho alichokisema. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ukisema kwamba Waheshimiwa wabunge, wanachangia kishabiki ina maana hapa…

**SPIKA:** Hilo umeeleweka huna haja ya kurejea na hilo la pili, hoja ni hiyo ya…

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa natoa mifano. Hoja yangu ya jumla, kuna lugha za staha ambazo zinaongozwa na kanuni lazima zitumike humu Bungeni. Kuna lugha za kutujumuisha kama Taifa lazima zitumike humu Bungeni. Naomba mwongozo wako, kwa sababu michango inaendelea ya Waheshimiwa mawaziri, lakini ninavyoona tunavyoelekea ni kama ni kesi ya paka na panya tunavutana. Sasa mimi naomba mwongozo wako juu ya matumizi ya lugha na namna ambavyo tunaweza tukalinda hadhi ya Bunge tusionekane kwamba humu ndani watu wanashabikia jambo fulani na wengine hawashabikii jambo fulani, ahsante Mheshimiwa.

**SPIKA:** Sawa, ahsante sana.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu.

**SPIKA:** Kaa kidogo nimalize mwongozo Mheshimiwa Waziri Nape Nnauye. Waheshimiwa wabunge, mchango wa Mheshimiwa Nape na matumizi ya neno kushabikia, kwa sababu ni lugha ya mazungumzo. Na sisi wakati tukichangia humu wapo watu wametaja viongozi wa CCM wakiwapongeza na wametaja neno Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo kwenye hoja hiyo nisingependa kwenda mbali zaidi ya hiyo, ni lugha ya mazungumzo kwa hiyo mtu anaweza akatumia lugha maadamu si lugha ya kufedhehesha ikae kwa sura hiyo.

Kwamba yeye anagawa Waheshimiwa wabunge humu ndani na yenyewe nataka kuweka hivi; kwamba kanuni zetu zinatambua kwamba humu Bungeni vipo vyama. Kwa hivyo yeye kama Mbunge anayechangia ameamua kwenda kwa sura hiyo sawa, lakini Bunge linatambua kwamba kanuni zetu zinafahamu

humu ndani tupo kivyama. Kwa hiyo anayepata nafasi ya kuchangia yeye achangie aonavyo inafaa ilimladi havunji kanuni zetu.

Mheshimiwa Olelekaita.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru na mimi nilikuwa naomba mwongozo wako; kwa sababu tunajadili ripoti za Kamati na Waheshimiwa mawaziri, ni sehemu ya Kamati. Sasa mwongozo wangu, wanafafanua nini kama ni sehemu ya kamati hizi na sehemu ya ufafanuzi kwenye ripoti za *CAG* ilitakiwa iwe imeshamalizika siku nyingi, ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ngoja nitoe ufafanuzi. Tusikilizane. Ni hivi, mimi wakati nikitoa maelezo ya namna uchangiaji wa hawa Waheshimiwa Wabunge ambao wananafasi nyingine ndiyo nimesema kwamba wanatoa ufafanuzi. Kimsingi wanachangia, ndiyo maana mnaweza kutoa taarifa kwa hiyo mimi ndiye nimetumia neno kwamba wanatoa ufafanuzi lakini kimsingi wao wanachangia kama sisi wengine. Kwa hiyo katika michango yao wamejielekeza huko kwa sababu wao wana taarifa za ziada kama sehemu ya Serikali; lakini ufafanuzi utatolewa na wenyeviti wetu watatu. *(Makofi)*

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**SPIKA:** Waheshimiwa wabunge.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, mwongozo.

**SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Swalle. Mheshimiwa Nape, ulisema kuna kanuni inavunjwa.

**WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 70 na ina-*refer* maelezo aliyoyatoa Mheshimiwa Makamba.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wangu Mheshimiwa Makamba analipotosha Bunge maneno niliyoyatumia hapa Bungeni. Niliposimama utakumbuka nimesema Waheshimiwa Wabunge wanachangia kwa uzalendo mkubwa na kwa ukali ambao unastahili katika kusimamia rasilimali za nchi. Ilipotolewa Taarifa nikasimama nikawa naijibu, Taarifa ya Mheshimiwa Mbunge mmoja nikasema vizuri kwenye mambo haya tuweke ushabiki pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sijalituhumu Bunge hili na Waheshimiwa Wabunge kuchangia kwa ushabiki. Nilikuwa najibu Taarifa iliyotolewa *very specific to me*. Kwa hiyo, kwa mtazamo wangu nadhani utaratibu ambao anautumia Mheshimiwa Makamba wa kutaka kupotosha Bunge lako lichukue maneno ambayo si yangu, si utaratibu sahihi na ni kuvunja Kanuni za Bunge lako. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Kanuni zetu zinataka nikishaeleza jambo Kuhusu Utaratibu, hapo ndio linakuwa limekwisha na kama mtu hakuridhika anatumia kanuni, nadhani ni Kanuni ya Tano. Kama hukuridhika na uamuzi unatumia Kanuni ya Tano, unaweza ukachukua hatua nyingine. Kwa ujumla, nadhani nilishatoa ufafanuzi juu ya maneno uliyoyasema Mheshimiwa Waziri na namna Mheshimiwa Salome Makamba alivyoyaweka. Kwa hiyo, siwezi kujirejea mwenyewe nikiwa bado nimekaa hapa mbele. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja…

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huu utakuwa Mwongozo wa mwisho. Mheshimiwa Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nimesimama kwa heshima kuomba mwongozo wako juu ya Kanuni ya 71 ya Kanuni za Bunge kwenye

71(g), inayohusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Kwenye mjadala ambao unaendelea Waheshimiwa Wabunge tunajadili Ripoti ya *CAG,* tunajadili changamoto, matumizi mabovu ya fedha, wizi na kadhalika. Mambo yasiyoruhusiwa kwenye Kanuni ya 71(g) ni kutumia jina la Mheshimiwa Rais, kushawishi Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nikuombe kwenye mjadala unaoendelea naomba mwongozo wako. Tusimtumie Mheshimiwa Rais kumuhusisha na mambo ambayo yanaendelea ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Waheshimiwa Wabunge tunajua kazi kubwa anayofanya Mheshimiwa Rais, kwenye Majimbo yetu, sisi kama Waheshimiwa Wabunge tunajua kwamba Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita ndio Rais aliyepeleka fedha nyingi kwenye majimbo yetu, kwenye hilo tupo na Mheshimiwa Rais, kwa asilimia 100. Hapa tupo kumsaidia kudhibiti mianya ya upotevu wa fedha, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, umeombwa mwongozo hapa na nimepelekwa kwenye Kanuni ya 71(g) kuhusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni.

Nirejee tena Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wana nafasi nyingine ya Uwaziri au Naibu Waziri, wanachangia kama sisi tulivyochangia na sisi tangu tumechangia siku ya Alhamisi, jana na leo wote hapa mnasimama mkimpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri zilizofanyika kwenye majimbo yenu na mkieleza kwamba baadhi ya maeneo kuna changamoto pesa zimekwenda zimeliwa. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, hata wao wanapomtaja Mheshimiwa Rais katika michango yao na wao wamechua muktadha wa yale wanayotaka kuyasema. Kwa hiyo, isichukuliwe kwamba wanataka kutumia jina la Mheshimiwa Rais ili pengine Bunge liamue kwa namna fulani, hapana, kwa hiyo, muktadha ni huo huo kama ambavyo sisi tulikuwa tunampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwa kazi alizofanya majimboni na wao

wanampongeza kumshukuru na kutaja mambo aliyofanya Mheshimiwa Rais katika michango yao.

Kwa hiyo, na wao wapo sahihi kwenye matumizi ya jina na haina uhusiano na kufanya maamuzi, kwa sababu Bunge litafanya maamuzi yake baada ya kuwasikiliza Wenyeviti wetu watakavyohitimisha hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo atafuatiwa na Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, Mheshimiwa Profesa Mbarawa, ajiandae.

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nishukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja tatu. Nitakuwa na mambo manne, la kwanza ni muktadha, muktadha ni kwamba humu ndani Bungeni tuna Waheshimiwa Wabunge sisi wote lakini pia kuna Serikali na kila mtu apewe nafasi ya kufanya kazi yake. Kazi ya msingi ya Mheshimiwa Mbunge ni kuhoji Serikali. Kazi ya sisi tuliopo huku ni jukumu letu la msingi kujibu hoja za Wabunge. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaposimama kujibu hoja za Wabunge isionekane kwamba tunatetea majambazi, haiwezekani, Serikali ya CCM ilishafunga Mawaziri. Kwa hiyo, suala la kupeleka majambazi na wezi mahakamani halijaanza leo lipo. Wapo Mawaziri, wapo Makatibu Wakuu walishafikishwa mahakamani, muhimu ni kwamba sheria lazima zizingatiwe. Kwa hiyo, nataka kuweka vizuri hili kwamba tunapofanya shughuli yetu ya msingi ya kujibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge isionekane kwamba tunafanya makosa kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mnahoji kama jukumu lenu na sisi tuna haki ya kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, tupewe nafasi hiyo. *(Makofi)*

Katika Taarifa ya *CAG* mambo ya msingi tunakubaliana na kwa kweli hamna Waziri hapa anayebishia Ripoti ya *CAG,* lakini kuna hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge wamezisema mimi kama Waziri wa Serikali ninawajibika kuzijibu. Kwa mfano, mtu

anasema naomba ninukuu; "na leo nasisitiza kuwa tumepigwa zaidi trilioni 280."

Mimi kama Waziri wa Mipango ninayefahamu kwamba pato la Taifa lote nchi hii ni shilingi trilioni 141, nitaacha vipi kujibu hoja hii? Yaani kutoka Kagera mpaka Pemba, ukikusanya fedha zote za Watanzania ni shilingi trilioni 141. Mtu anasema zimepigwa trilioni 280 *how? Logic* inakataa. Kwenye *argument* kuna kitu kinaitwa *fallacy,* kwamba *premise and conclusion* lazima zioane pale zikigongana ina kuwa *inconsistency* inakuwa ni mkanganyiko huo ni mkanganyiko wa hoja ninawajibika kuizijibu. *(Makofi)*

Mtu anakuambia, Mheshimiwa Mbunge anasema nchi inakufa hiyo kwenye *CAG report* haipo…

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jesca Msambatavangu, Mheshimiwa Profesa Kitila, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nilikuwa naomba kwa kuwa wamesema wanajibu hoja nilikuwa naomba pia anajibu hoja kama Serikali anachangia *whatever*. Hizi anazosema trilioni mia na, zimehusiha na hizi za wizi ambazo *CAG* amezigundua na ambazo hatujazigundua, hizo trilioni. *(Kicheko/ Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ameuliza swali siyo taarifa, kwa hiyo, sihitaji kushughulika nayo hiyo.

Kwa hiyo, nilikuwa natoa mfano, nimetoa mifano miwili tu; mfano wa pili nyinyi wote mliopo Waheshimiwa Wabunge na sisi,

ni nchi yetu. Sisi ni viongozi, mMtu anakuambia nchi inakufa hiyo katika *political science* unaongelea…

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Mkumbo, kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Mpina.

**TAARIFA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, anajieleza vizuri kwamba amefanya *financial analysis* kwamba trilioni 280 haziwezi kupigwa. Sasa yeye katika *financial analysis* yake anajua zimepigwa ngapi? *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naona taarifa zenu zinatoka kwa sura ya maswali ambayo Mheshimiwa Waziri kwa kweli halazimiki kujibu, kwa sababu ili Serikali iweze kujibu maswali ni katika kipindi cha maswali na majibu. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, nirudie tena hoja lazima iwe na mantiki, fedha zote za nchi hii kwa taarifa ya mwaka jana ni trilioni 141. Mantiki inakataa kwamba zimeibwa trilioni 280, ni *logic* ya kawaida. Mantiki inakataa. Ya tatu…*(Makofi)*

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo ni taarifa ya ngapi?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, naomba ya mwisho.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Mtaturu, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nimefurahi sana kaka yangu Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo ni Waziri wa Mipango. Naomba tu nimpe taarifa, kwamba miongoni mwa Taarifa ya CAG mambo yaliyojitokeza makubwa ya upotevu

wa fedha ni pamoja na kuzima *POS* zaidi ya siku 1000. Yeye kama Waziri wa Mipango, tunaomba jibu namna gani Serikali itachukua hatua kwa zile *POS* zilizozimwa?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hiyo ilikuwa ni taarifa ya mwisho kwa Mheshimiwa Profesa Kitila Mkumbo, malizia mchango wako.

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, mfano wa pili, sisi ni viongozi *we must be responsible*. Mtu anakuambia nchi inakufa, hiyo kwenye *political science* maana yake *failed state,* siyo kweli. Unasemaje nchi inakufa inayojenga reli yenye kilometa 2600 kutoka Dar es Salaam hadi Kalema? Unasemaje nchi inakufa iliyotoa Rais wa *IPU* duniani *how?* Nchi ambayo dunia nzima imeiamini ikakubali kutoa Spika, inakufa vipi? *Nonsense*. *(Makofi)*

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mwongozo wa Spika.

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, ndio nasema pale ambapo hoja haina mantiki kama Waziri wa Serikali ya Rais Samia lazima nijibu.

Mheshimiwa Spika, haya niendelee nichangia kidogo kwenye *CAG Report*. Ukweli ni kwamba kisaikolojia macho ya binadamu yameumbwa kuona mabaya kuliko mazuri, ni kisaikolojia, lakini ndani ya *CAG Report* ameonesha yeye mwenyewe kwamba hatua kadhaa zimepigwa kwenye kutekeleza mapendekezo yake naomba ninukuu vipengele vinne muda ukiniruhusu.

Mheshimiwa Spika, kwenye Taarifa ya Ripoti ya Mwaka ya Miradi ya Maendeleo Utendaji wa Kifedha, ukurasa wa pili, *CAG* anasema; "zaidi ya asilimia 90 ya miradi ilipata hati zinazoridhisha kwa miaka mitano mfululizo kuanzia mwaka 2017/2018. Hii ikiwa ni ishara nzuri kwenye matumizi ya fedha na utendaji wa Serikali." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa pili, naomba nirejee tena alisema nini kuhusu Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, kwa sababu hoja imekuja hapa kwamba mradi umechelewa alisema nini. *CAG* anasema na nanukuu; "Nilibaini makadirio ya muda wakumalisjha mradi usio halisi, kwani mradi ulipangwa kumilika katika kipindi cha miaka mitatu, huku miradi ya ukubwa kama huo iliyojengwa duniani huchukua kati ya miaka minne hadi miaka kumi kukamilika, makadiro ya awali hayakuwa halisi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii maana yake ni nini, maana yake ni kwamba wataalamu walitoa mapendekezo yao, lakini kuna mtu akatumia maamuzi ya kisiasa akaweka mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuchelewa kwa mradi siyo kwa sababu ya fedha…

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, mfano wa tatu *CAG*…

**SPIKA:** Mheshimiwa**,** Sekunde 30, malizia.

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, mfano wa tatu, *CAG* kwa miaka mitano mfululizo amelalamika juu ya deni la *TANESCO* na *TPDC*. *CAG* akatoa mapendekezo kwamba Serikali iyageuze madeni haya na kuyasafisha vitabu vya mashirika. Serikali ya Mheshimiwa Rais Samia miaka mitano imekubali na imetekeleza na *CAG* amesema pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mfano wa nne *CAG* alitoa mapendekezo kwamba Serikali ilipe madeni *PSSF* kiasi cha trilioni mbili kupitia Hati Fungani, Serikali imelipa na *CAG* amesema. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umekwishwa.

**WAZIRI WA MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Spika, umeisha? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, haya. Mheshimiwa, George Boniface Simbachawene, atafuatiwa na Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Mheshimiwa Aweso ajiandae.

Mheshimiwa Simbachawene, kabla hujaanza kuzungumza samahani kidogo.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni hapa ndani ni watangaze ili wawe huru. Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Dkt. John Danielson Pallangyo kutoka Arumeru, Arusha, huyu ni Katibu Mstaafu wa CCM Kata ya Mbureni, karibu sana. *(Makofi)*.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 45, wa Mheshimwa Dkt. Angeline Mabula, kutoka kanisa la Moravian Jimbo la Kaskazini, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 12 wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata hawa ni Madiwani na mwalimu kutoka Mkoa wa Rukwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Tunao wanafunzi 120 kutoka Chuo ya Mipango Dodoma, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Simbachawene atafuatiwa na Mheshimiwa Mbarawa, na Mheshimiwa Aweso, ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nikupongeze kwa kuwa Spika wa Mabunge yote Duniani, hongera sana Mheshimiwa Spika wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeanza kuona viwango vya Uspika wa Bunge la Dunia kwa namna ambavyo una-*balance*. Eeh, ni Rais wa Mabunge Duniani. Niwie radhi kwa kushusha kidogo. Wewe ni Rais wa Mabunge yote Duniani na viwango hivyo vimeanza kuonekana hapa namna ambavyo umekuwa *referee* mzuri leo katika hizi timu mbili na ndio raha ya Bunge. Bunge lina pande mbili lazima pande zote zipewe nafasi. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia masuala ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Katika misingi ya utawala bora vipo vyombo ambavyo vinatusaida kutekeleza majukumu yetu. Moja kati ya vyombo vinavyotusaidia katika kusimamia uwajibikaji wa matumizi ya fedha ni Ofisi ya *CAG*. Ofisi ya *CAG* ikishafanya kazi yake, vipo vyombo vingine vinavyokwenda kusimamia na kuangalia utekelezaji wa yale yaliyoonesha mashaka katika Ripoti ya *CAG*. Moja wapo katika vyombo hivyo ni *PCCB* ambayo inasimamiwa na Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, ninataka nikuhakikishie kwamba katika misingi ya utawala bora *CAG* amefanya kazi yake vizuri sana na ninawashukru sana Waheshimiwa Wabunge wote, kwa kupongeza Ripoti ya *CAG* na kama tukitaka *compromise* misingi ya utawala bora ni pale tutakapodharau Ripoti ya *CAG*. Tusidiriki hata mara moja kufanya hivyo tuendelee kushughulika na haya mapungufu kama tunavyofanya na hivi ndivyo mnavyotakiwa kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, isionekane hata mara moja kwamba sisi Mawaziri tunaposimama kutoa taarifa tunatetea wahalifu, hapana. Sisi Mawaziri tunatoa taarifa kwa maeneo ambayo tunadhani pengine wenzetu wanaweza wakawa hawana taarifa ili waweze kupata taarifa na wala hata mara moja si nia yetu kuwatetea wezi, wahujumu uchumi, hapana, hatufanyi hivyo. Serikali hiyo hapo huku ndani haipo hapa Tanzania, tumekuwa tukichukuliana hatua na nitakuonesha ushahidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mitatu kutoka 2021, 2022 mpaka Oktoba, 2023 *PCCB* kutokana na Ripoti za *CAG*

imefungua kesi 1,790. Katika kesi hizo 1,790 kesi ambazo Serikali tumeshinda yaani watu wametiwa hatiani na hawa wamo humo na hao wote mnaozungumzia wapo humo, Wakurugenzi wapo humo, *accountants,* wapo watu mbalimbali ambao wameshughulikiwa. Katika kesi hizo kesi 965 wametiwa hatiani wapo magerezani na wengine wamefukuzwa kazi na hatua nyingine za kisheria. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE**: Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Simbachawene kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninataka kumpa taarifa mzungumzaji kwamba, *PCCB* ambao wanaoshughulika na mambo ya kesi, hivi wale TAKUKURU wa Kilimanjaro ambao *KADCO* imekatalia uwanja wa ndege wa Kilimanjaro, hawajachukua hatua?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ametoa taarifa yake kwa namna ya swali kwa hivyo hulazimiki kujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa hiyo mpaka sasa, kesi 965 Serikali imeshinda na kesi 621 zinaendelea, zipo katika ngazi mbalimbali. Kazi kubwa imefanyika kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais aliyepokea ripoti, kazi ilianza kufanyika kuanzia wakati ule.

Mheshimiwa Spika, tulibadilisha kanuni hapa, tukabadilisha sheria. Tukasema ripoti ya Serikali ya namna tunavyoripoti, tutakuwa tunaleta kabla, tulileta Bunge lililopita. Tumefanya hatua fulani kubwa na mpaka leo hii tunaendelea kutekeleza. Mathalani, katika fedha ambazo TAKUKURU imezirejesha, zilizokuwa zimepigwa, nitumie lugha hiyo hiyo inayotumika. Zilizokuwa zimepotea ni Sh.14,274,000,000 pesa za Kitanzania pamoja na dola 14,571.

Mheshimiwa Spika, la pili, mali zilizotaifishwa ambazo zilikuwa zimepatikana kwa njia hiyo ya mapato yasiyo halali ambazo tumezirejesha (tumezitaifisha) zina thamani ya Sh.2,051,000,000.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene kuna taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Mpina.

**TAARIFA**

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, mchangiaji anaendelea vizuri lakini kwenye taarifa ya majumuisho ya majibu ya Serikali ambayo ina kurasa 1,111, hilo jambo analolizungumza na hatua anazozizungumza hazimo kwenye majibu ya Serikali.

**SPIKA:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri anaweza akasema ni kipindi gani, lakini ile taarifa mtakumbuka ililetwa hapa Bungeni mwezi Juni, nadhani Tarehe10. Kwa hivyo, kwa maelezo ya Waziri nilivyomsikiliza labda kama nimemsikia peke yangu, amesema tangu taarifa hiyo iletwe yapo mambo mengine yaliyofanyika katika hiyo miezi kuanzia Juni. Kama hivyo ndivyo, inawezekana yale majibu yalipokuja mwezi Juni mpaka sasa ndiyo hizi hatua anazozisema, lakini kama Bunge bado nafasi yetu ipo pale pale ya kuendelea kufuatilia utekelezaji wa haya ambayo Serikali inasema imeyafanya. Mheshimiwa Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli. Hii ni mpaka Oktoba yaani mpaka mwezi huu uliopita, ndiyo Serikali tumefanya hizi kazi zote. Kwa hiyo, kusema Serikali haijachukua hatua yoyote, nilitaka nitoe taarifa kwa Waheshimiwa Wabunge kwamba hatua zimechukuliwa na zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Spika, fedha tunazozungumzia za *POS,* mpaka sasa tuna kesi ya uhujumu uchumi kesi Namba ECC 32 ya Mwaka 2023 ambapo, watuhumiwa 16 wanaotuhumiwa kupoteza au

kufanya ubadhirifu kwenye karibu shilingi 8.9 *billion out of* ile bilioni 11 waliyoisema kwenye mashine za *POS*.nnKatika fedha hiyo, 8.9 *billion* zote hizi watu wapo *tasked* na kesi zimefunguliwa na wapo mahakamani.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya ahsante sana, kuna taarifa kutoka kwa… sasa Waheshimiwa mmesimama watatu wote mnataka kutoa taarifa kwa mchangiaji mmoja? Mheshimiwa George Kakunda.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, maneno ambayo ameyazungumza Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana, lakini naomba nimpe taarifa kwamba, Maafisa Masuuli walipokuwa wanakuja kwenye Kamati, walikuwa wanakuja kujibu hoja ambazo wamekaa na *CAG* siku tatu zilizopita. Kwa hiyo, ni muhimu Serikali ikiri kwamba, bado kuna kazi kubwa ya kufanya ya kurekebisha mambo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simbachawene unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naipokea kwa sababu kazi hii ni endelevu. Hii kazi ni endelevu, tunashughulikia uhalifu. Waheshimiwa viongozi tuzungumzie mambo halisi, yaani tusitafute humu, hii kazi ni endelevu, inaendelea. Mimi ninavyozungumza, *out of* ile *11 billion*, *so far 8.9 billion* tayari tumekwishazirejesha Serikalini. 5.2 billion zilizokuwa zimepotea kwenye *POS Machine*. Hii ni kutoka kwenye Halmashauri ya Ilala, Ilemela na nyingine nyingi zimerejeshwa kwa sababu ya kazi nzuri inayofanywa na TAKUKURU.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo…

**SPIKA:** Muda wako umekwisha. Sekunde 30 malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nimalizie. Imeelezwa hapa kwamba watumishi wa Serikali hawajalipwa malimbikizo ya mishahara. Hivi ninavyozungumza mpaka mwezi Oktoba Serikali ya Awamu ya Sita imelipa watumishi 137, 599, fedha zenye thamani ya shilingi bilioni 235.16. Hizi fedha zipo kwenye halmashauri zetu, watumishi wetu wamelipwa.

Mheshimiwa Spika, nimetembelea mikoa minne tulivyomaliza Bunge, nimeenda ninakuta furaha waliyonayo watumishi wetu. Kwa hiyo, nimalizie. Watumishi wa nchi hii, pamoja na mapungufu yanayozungumzwa hapa, lakini wapo waliofanya vizuri na ndiyo maendeleo tunayoyaona. Hao wachache ambao wanafanya vibaya tutawashughulikia na sheria zipo na ndiyo maana ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shigongo, karibu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ERIC J. SHIGONGO:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako kwa jambo moja kubwa ambalo naona ni vizuri nilizungumze, halafu utoe muongozo. TAKUKURU kama Taasisi yetu ya Kupambana na Rushwa inayo majukumu makubwa mawili. La kwanza, kuzuia rushwa na la pili ni kupambana na rushwa. TAKUKURU imesahau jukumu lake la msingi la kuzuia na imejielekeza kwenye jukumu la kupambana, kwa sababu hiyo wanakuja kuingia kwenye suala la kupambana wakati fedha zimeshaibiwa.

Mheshimiwa Spika, la pili, ni suala la *CAG*. Kama nilivyozungumza katika suala la TAKUKURU, *CAG* kazi yake ni

*control and audit*. Ninapotazama *CAG* amejielekeza kwenye *audit* na amesahau jukumu lake la *control*. Sasa naomba mwongozo wako, nini kifanyike ili tuzirejeshe taasisi hizi kwenye majukumu yake hayo yaliyosahaulika, kuzuia pamoja na ku-*control.*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwenye mwongozo huu ambao ameuomba Mheshimiwa Mbunge, kwa maoni yake yeye anaona *CAG* hafanyi ile kazi yake ya *control* kwa Kiswahili kudhibiti. Wakati huo huo na TAKUKURU haifanyi ile kazi ya kuzuia. Nafikiri tunaweza tu kusema hivyo, ikiwa tumejiridhisha na taarifa za utendaji kazi wa hivi vyombo vyetu. Maana yake kije chombo kimtazame *CAG,* kitupe taarifa halafu kije chombo kiitazame TAKUKURU, kitupe taarifa.

Hatutaweza kusema hivyo kwa kuitazama Taarifa ya *CAG* kwa sababu, kwa ujumla wake hilo hatutaweza kulifanya katika mazingira haya. Basi muongozo wangu kwa sababu ameomba baada ya Mheshimiwa pale kusema mchango wake labda unaruhusiwa? Maana ameitaja hapo TAKUKURU na mambo iliyofanya na mambo kama hayo. Kwamba, unaruhusiwa au hauruhusiwi mchango wa Mheshimiwa Simbachawene unaruhusiwa. Kwa sababu, ndiyo kanuni yetu ya muongozo huwa inataka jambo liulizwe kama linaruhusiwa hapa Bungeni ama haliruhusiwi. Kwa hiyo, mchango wa Mheshimiwa Simbachawene unaruhusiwa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, atafuatiwa na Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro ajiandae.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja zetu tatu zilizopo mbele yetu. Mchango wangu kwanza utajikita kwenye Azimio la Bunge ambalo lilitolewa mwaka jana kuhusu kuhamisha *KADCO* kwenda *TAA.*

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu yeyote kwenye Serikali ambaye anapingana na maagizo ya Bunge na sisi kama Serikali tunathamini sana maagizo yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Bunge lako Tukufu. Mara baada ya kikao kile tulianza kujipanga kwenda kuangalia jinsi gani tutaweza kutekeleza agizo hili, lakini kulitokea changamoto kubwa kuhusu Sheria ya *TAA* ambayo ni sheria ya *Executive Agency, Act No.3* ya mwaka 1977 hairuhusu utaratibu wa kutoa hizo fursa moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, baada ya kushauriana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, tuliamua kutengeneza sheria mahususi ya *TAA* ambayo itaruhusu uendeshaji na uendelezaji kupewa Taasisi za Serikali na *Private Sector.* Sheria hiyo imepita katika maeneo mbalimbali na ngazi mbalimbali na wadau mbalimbali wametoa maoni. Tarehe 20 mwezi uliopita, Serikali ilitoa maamuzi kwamba sheria hiyo iundwe ambayo itatoa fursa mahususi sasa kwa ajili ya mpango huo wa kuhamisha *KADCO* kwenda *TAA*, pamoja na kuipa fursa *TAA* kuingia mikataba na kampuni za *private*, pia kuipa fursa *TAA* kushirikiana na Taasisi mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, hatua tuliyofikia sasa sheria inaendelea kutungwa na Bunge letu linalokuja la Februari, sheria hiyo itawasilishwa hapa Bungeni ili Waheshimiwa Wabunge waijadili. Naamini kwa hamu waliyonayo sheria hiyo itapita na tutaendelea kufanya mchakato wa kuhamisha *KADCO* kwenda *TAA* bila matatizo

Mheshimiwa Spika, tulilazimika kwenda na utaratibu huo kwa sababu tulitaka na sisi tusivunje sheria. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, *KADCO* ni Kampuni ya Serikali ambayo ipo chini ya Msimamizi wa Msajili wa Hazina na itaendelea kuwa hivyo hata ikienda huko *TAA,* kwa sababu, kampuni zote hizi za Serikali zipo chini ya Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijikite kwenye hoja za *CAG…*

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarawa kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mtemvu.

**TAARIFA**

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anazungumza vizuri juu ya jambo la *KADCO,* kwamba, sasa hivi wanatengeneza sheria ili *TAA* iweze kuimiliki na hii *private company*. Tukiwa tunatambua *TAA* inamiliki viwanja vingine Tanzania hapa ambayo tungeamini na *KIA* kingekuwa ndani. Kama Kamati, nikiwa Mjumbe wa *PAC* tunatambua *KADCO* imemaliza mkataba wake uliokuwepo Tarehe 16 Mwezi Julai, 2023. Sasa, Mheshimiwa Waziri atuambie sasa hivi *KADCO* inaendelea kuwepo pale kama nani? Ikiwa haina mkataba wowote na mkataba wake umeisha?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pengine hii hoja ya *KADCO* inaleta ugumu kidogo kwa sababu nakumbuka mwaka jana na ninayo *Hansard* hapa, Bunge lilikuwa kali sana kuhusu jambo hili. Serikali ilikuwa imeshatoa maelezo inaenda kufanyia kazi Maazimio ya Bunge. Hili ni Azimio mojawapo ambalo ni kati ya yale ambayo Bunge limeazimia, Serikali ikaleta taarifa Juni, ikasema jambo hili wameshafikia hatua nzuri kufikia sijui mwezi wa ngapi litakuwa tayari na sasa tena tunaambiwa bado. Sasa naambiwa huko na Wajumbe wa Kamati kwamba mkataba ukwisha. Mkataba umekwisha lakini *KADCO* bado wapo.

Waheshimiwa Wabunge, wakati huo huo *KADCO* ni ya Serikali, wakati huo huo haiwezi kukabidhi kiwanja *TAA* ambayo nayo ni ya Serikali. Sasa, mazingira hayo Mheshimiwa Waziri, leo nitakupa muda wa kutosha tuelewe vizuri hili jambo la *KADCO,* kwa sababu, lina Azimio maalum la tangu mwaka jana.

Mengine yote najua huko mwishoni nitapata nafasi ya kuzungumza lakini hili la *KADCO* kelele zilikuwa nyingi na Mheshimiwa *AG* upo hapa, nitawapa nafasi wewe na Mhehishimiwa Waziri mtueleze vizuri hilo jambo. Kwamba, viwanja vingine vyote vimewezekana kwenda *TAA*, isipokuwa kiwanja cha *KIA* kimeshindikana kwa sababu *KADCO* yupo pale na ni wa

Serikali. Sijui ugumu unatokea wapi mpaka mnahitaji sheria mpya ili *TAA* akabidhiwe *KADCO*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, halafu Mheshimiwa *AG*.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, *TAA* inaendesha viwanja 54 vya Serikali, *KADCO* hakipo. Vilevile TAA ni taasisi ambayo ipo chini ya Msajili wa Hazina. *KADCO* sasa ipo chini ya Msajili wa Hazina. Sasa, kwa Sheria ya *TAA* ilivyo sasa kama nilivyosema na Sheria ya *KADCO* ilivyo, hatuwezi kuihamisha *KADCO* moja kwa moja kuipeleka *TAA* kwa sasa.

**SPIKA:** Malizia, nawasha najiandaa.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, tuliomba ushauri kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuhusu jambo hili na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ikatwambia kwa jambo lilivyo kwa kuwa kampuni hizi ni tofauti, ile moja ni kampuni ambayo imenzishwa kwa *Executive Agency*, nyingine imeanzishwa kwa utaratibu mwingine, inabidi muanzishe sheria maalum ambayo itaifanya *TAA* kuchukua viwanja kwa mfano cha *KADCO* na viwanja vingine vya *private*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala hili ni kweli *KADCO* muda wake wa uendeshaji umemalizika, lakini na hilo tulilipeleka kwa Mwanasheria Mkuu akasema, hili lazima tuandike waraka kupeleka kwenye mamlaka na tumefanya hivyo, tupo katika hatua za kutolewa maamuzi.

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niunge mkono sehemu ya maelezo iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana na Uchukuzi. Suala la *KADCO* lina historia ambapo uamuzi wa awali kabisa ulikuwa ni Serikali kuichukua hisa zote kwenye kampuni hiyo. Hilo likakamilika.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili, katika hatua ya kuhamishia *TAA* kukajitokeza kulikuwa na *liabilities* za *KADCO* ambazo

hazikuwa sahihi, *TAA* izirithi. Kwa hiyo, pamoja na Azimio la Bunge hili, vilevile kulikuwa na maamuzi ya Baraza la Mawaziri. Waziri alilazimika kurejesha suala hili kwa kutoa taarifa kwenye mamlaka zinazohusika na baadaye sasa maamuzi yamekwishafanyika kama alivyosema Mheshimiwa Waziri. Kwa sasa, *concessional agreement* imemaliza muda wake mwezi Julai, *lease agreement* muda wake utaisha mwezi wa kumi na moja.

Mheshimiwa Spika, kipindi hiki hapa katikati, kabla Bunge hili halijafikia mwisho wiki ijayo, naamini mchakato wa kuletwa Bungeni kusomwa mara ya kwanza kwa Sheria ya *TAA* ambayo sasa itakuwa imewekea mawanda makubwa ya kuendesha viwanja vyote vya ndege nchini, nafikiri sasa tutakuwa tumefikia kwenye ukamilifu wa Azimio la Bunge la mwaka jana.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali tusaidie, hii *KADCO* mkataba umeisha, inafanya kazi. Unasema *liabilities* za *KADCO* ambazo hamkutaka ziende *TAA* ndiyo zilizozuia kumalizika huu mkataba. Hizi *liability*, maelezo ya ukweli kabisa ni kwamba asilimia mia moja *KADCO* inamilikiwa na Serikali, nipo sahihi? Kama hivyo ndivyo, maana yake Serikali si inamiliki na na hizo *liability* ama *liabilities* ameachiwa yule aliyekuwa mmiliki wa *KADCO* kabla Serikali haijachukua umiliki? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu *KADCO* kama kampuni iliyosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni ilikuwa ina hadhi za kisheria. Kwa hiyo, *transition* iliyofanyika baada ya Serikali kuwa na hisa zote ilikuwa ni kuiweka sasa chini ya muundo wa Serikali ambapo sasa mambo ambayo yanafanyika sasa, nafikiri ni yale ninayosema, hatua mojawapo ni kisheria. Hii ni baada ya ile *lease agreement*, moja, haitakuwa na mkataba wowote; lakini pili *TR* ambaye kwa sasa ndiye msimamizi mkuu, nafikiri chini ya Wizara husika, kwa sababu kufikia Februari sheria itakuwa imepita, naamini…

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa *AG* endelea au ulikuwa umemaliza?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa naamini kwamba kwa sababu kuna utaratibu..

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, baada ya ule Muswada, wiki ijayo unaposomwa kwa mara ya kwanza, utakuwa umeshawekwa tayari, utakuwa umeshakuwa umeshakuwa gazetted.

**SPIKA:** Kwa sasa nani anaendesha kiwanda cha *KIA*?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ni *KADCO* chini ya usimamizi wa Serikali.

**SPIKA:** *KADCO* ambaye mkataba wake umekwisha. *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, *Lease agreement* haijafikia ukomo.

**SPIKA:** Hii ndiyo Novemba unayoitaja au ni Novemba mwakani? Maana umesema mwenyewe hapa, Mwezi wa Kumi na Moja na ndiyo leo hapa tupo Tarehe 4 Mwezi wa Kumi na Moja. Ni mwezi huu au ni Mwezi wa Kumi na Moja mwakani?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, *no* ni Mwezi wa Kumi na Moja, mwaka huu.

**SPIKA:** Mwaka huu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Sasa, kwa kweli kwenye jambo hili mnalipa Bunge wakati mgumu. Kwa sababu kama kampuni hiyo ya *KADCO* ambayo umiliki asilimia 100 ni wa Serikali na iko chini ya Msajili wa Hazina, Mkataba wake umeisha bado iko *site* inafanya kazi.

Masharti yake ya uendeshaji wa kiwanja, huo mkataba ulishaisha. Uliobaki sasa hivi ni wa *lease* pekee. Sasa ule wa *lease* unawaruhusu kweli kuendesha uwanja? Mheshimiwa *AG*, hii *Lease* Agreement inawapa wao mamlaka ya kuendesha uwanja baada ya mkataba kuisha? Kwa sababu kisheria mseme hivi, tumewaongeza muda kwa sababu tunataka tubadili sheria. Ukisema mkataba umeisha bado wako pale wanafanya nini? *(Makofi)*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nafikiri tunaongea lugha moja. Kwa sababu ninaposema *TR* ndiye anayesimamia kama makampuni mengine ambayo yako chini ya Serikali, maana yake Katibu Mkuu mwenye dhamana na Waziri mwenye dhamana wana usimamizi wa moja kwa moja. Hii *transition* ninayoisema ya kuletwa sheria, maana yake lengo lake kubwa itakuwa ni kuipa ile *comprehensive mandate TAA* kuweza kuendesha *operations* za viwanja vyote nchini.

**SPIKA:** Yaani mimi nakuelewa sana. Aweze huyo *TAA* kuendesha viwanja vyote, isipokuwa *KADCO* mpaka anahitaji sheria? Sheria mpya inahitajika kwa ajili tu ya *KADCO?* Haya Mheshimiwa Waziri malizia mchango wako. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimewasikia lakini sasa Mheshimiwa Waziri alikuwa ameshasimama na mwongozo unaombwa akiwa hajasimama. Kwa hiyo, nimewaona wacha Mheshimiwa Waziri amalizie halafu nitawapa nafasi. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwa ufupi tu kama Mheshimiwa *AG* alivyosema, sisi tumeshaandika kuomba Serikali ili kwa kipindi hicho tupate angalau hicho kibali tuweze kumpa mpaka hapo sheria mpya itakapotungwa.

**MHE. CHRISTOPER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, hiyo Serikalini linaendelea.

**MHE. CHRISTOPER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** *KADCO, KADCO, KADCO!*

**MHE. CHRISTOPER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, jambo hili hapa ndani linaleta mkanganyiko mkubwa sana. Kule *site* kwa wananchi lina mkanganyiko mkubwa zaidi. Sasa hivi kuna zoezi linaendelea, kulipa fidia, Mheshimiwa Rais ametoa bilioni 11, wananchi wameelimishwa wameelewa na haikuwa kazi rahisi. Nilikuwa naenda *site* mimi kuzungumza nao, wakiwa na hasira kubwa mno, wameelewa jambo hili. Sasa, sasa hivi wanasikia tena wanapisha uwanja wao kwa mapenzi kwamba uwanja ni mali ya Serikali, hapa ukisikiliza hii sentensi maana yake ni kwamba *KADCO* sasa haijulikani ni ya nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mwongozo wako, ikiwezekana Serikali ipewe muda ndani ya wiki hii, Jumatatu au Jumanne walete tamko ili kuondoa *confusion*, kwa sababu tukiliacha hivi kule *site* litatuletea vurugu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukisikiliza maelezo ya Mheshimiwa Waziri pamoja na Mwanasheria ni dhahiri kwamba *KADCO* inaelea mahali, haina mwenyewe. Sasa ili tupate sentensi tusichanganye wananchi. Kama sisi humu ndani vinatuchanganya kule *site* itakuwaje? Mtatupa kazi kubwa na zoezi lile linaloendela kule.

Mheshimiwa Spika, naomba sana utupe Mwongozo wako lifikie mwisho, tupate sentensi ya Serikali itakayoeleweka kwa wananchi, kwamba *KADCO* ni nani?

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Ole-Sendeka.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa taarifa. Bunge hili ni Bunge lililopo kwa mujibu wa Katiba na Maazimio ya Bunge yanapaswa kuheshimiwa, kwa sababu Bunge linapofanya maazimio na sehemu ya pili Serikali ipo, kwa maana ya Waziri Mkuu, Mawaziri na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, bahati nzuri, maelezo yote yaliyotolewa na *Attorney General* ambae ninamheshimu sana, pamoja na Profesa ambaye ninamheshimu sana, kwa kweli hayana sababu yoyote (hayatoi sura nyingine) isipokuwa Serikali kupuuza kutekeleza Azimio la Bunge. Hakuna lugha nyingine ya kistaarabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine lililo kubwa zaidi, nchi hii tuna uzoefu, kuna taasisi nyingi za Serikali ambazo shughuli zake zimetoka kutoka taasisi hii kwenda taasisi nyingine, taasisi zote hizi mbili ziko chini ya *TR,* mnashindwa nini leo kuihamisha, ili kama mnataka kubinafsisha tena *TAA* au viwanja vinavyosimamiwa na *TAA,* mje muuze tu kwa bei ya jumla, kama ndiyo mmeamua kuelekea huko, kwa sababu kuna hatari, nami nataka niwaambieni…

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Sekunde 30, malizia.

**MHE. CHRISTOPER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, haya, namalizia. Jamani naomba muone hali ni mbaya sana. Tumesomesha vijana wengi, darasa alilokuweko Dkt. Tulia Ackson na alilokuwepo Prof. Mbarawa kuna wenzenu mlisoma nao, kama ninyi mmeweza kuongoza taasisi hizi kubwa, hivi kweli hamna Watanzania wanaoweza kumudu kuendesha hivyo viwanja vya ndege mpaka muwe na mawazo yote ya kukabidhi kila kitu ughaibuni? Naomba niwaambie hayawafurahishi wapiga kura wetu na haifurahishi Taifa. *KADCO* iondoke, ikabidhiwe *TAA* na viwanja vya ndege viongozwe na Watanzania wenyewe. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutulie kidogo, tutulie kidogo. Mheshimiwa *AG* hebu nisaidie, nani alikuwa anamiliki hicho kiwanja kabla *KADCO* hawajaja? Maana siyo *KADCO* waliojenga, ama ni *KADCO* wamejenga? Nani alikuwa anamiliki hicho kiwanja kabla ya *KADCO?* Waziri au nani anataka kujibu?

**SPIKA:** Waheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha *KADCO* kwanza kilikuwa Kiwanja cha Serikali, *I mean* Kiwanja cha *KIA*.

**SPIKA:** *KADCO* haina kiwanja ni kiwanja cha KIA.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika ni kiwanja cha *KIA…*

**SPIKA:** Kiwanja cha *KIA.*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha *KIA* kilikuwa Kiwanja cha Serikali, halafu wakati wa ubinafsishaji, ikaundwa kampuni ambayo kuna baadhi ya watu wa *private sector* waliingia. Mwingereza nafikiri kampuni ya Kiingereza

*MacDonald* pamoja na Kampuni ya *South Africa*. Baada ya kuona ule utaratibu uliowekwa siyo wa kuridhisha, Serikali ikaamua kuununua na wakalipa hiyo hela na ikatoa maelekezo huku nyuma kwamba kiwanja hicho kirejeshwe kwa *TAA* lakini kwa nini hakikuweza kurejeshwa kwa wakati huo wote.

Mheshimiwa Spika, sasa, *KADCO* sasa hivi ilivyo ni kampuni ya Serikali chini ya asilimia 100 na *KADCO* sasa hivi inaendeshwa na Mtanzania, haiendeshwi na watu wa nje na wafanyakazi wale wote ni Watanzania.

**SPIKA:** Sasa, nisaidie jambo jambo moja halafu tuendelee mbele Waheshimiwa Wabunge. Hii *KADCO,* maelezo yanayotoka ndiyo yanayotupa wasiwasi kama Bunge. *KADCO* asilimia 100 ni ya Serikali, kwa nini hii mijadala huwa inakuja na kwenda? *KADCO* asilimia 100 ni ya Serikali, *TAA* asilimia 100 ni ya Serikali, shida iko wapi ili Bunge tusaidie kwenye hiyo shida, tukwamue huo mkwamo ambao unatokea kati ya *KADCO* na *TAA*. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, tunakoelekea sasa hakuna mkwamo, kwa sababu kama alivyosema Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wiki hii italetwa sheria ya kusomwa mara ya kwanza ambayo itaweka mawanda yote kwa ujumla ya kuondoa *KADCO* kwenye *TAA*.

**MJUMBE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Sasa unajua hizi taarifa zimetukutia katikati kwamba na mkataba umeisha na hapa tuko Bungeni na sisi tutakuwa sehemu ya huu mchakato, tutakuwa sehemu, Serikali hebu itufafanulie huyu *KADCO* atafanyaje kazi, anaendeleaje kufanya kazi wakati mkataba haupo? Mwanasheria Mkuu wa Serikali, tufafanulie hilo tutoke hapa tukijua kwamba huo uwanja wa Watanzania uko salama pamoja na *KADCO* kuendelea kuendesha wakati mkataba haupo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nafikiri ufafanuzi wa kwanza ni kuomba subira kama ilivyo subira yavuta kheri kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, hakuna ubishi juu ya umiliki wa uwanja kwa Serikali, vilevile, hakuna ubishi juu ya uamuzi wa Serikali ku-*take over.* Pia, hakuna ubishi juu ya Azimio la Bunge hili la mwaka jana la shughuli zote za *KADCO* kuhamishiwa *TAA*. Sasa Taarifa ya Serikali kwamba, Baraza limekwishaamua na Serikali inaleta hapa Muswada, Muswada ambao kwa mujibu wa taratibu mnajua kwamba Bunge hili ndiyo litakuwa na dhamana ya kuujadili na kuupitisha.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kinachoweza kufanyika labda wiki ijayo Serikali iweze kuleta maelezo ya kuelezea hiyo *transitional arrangements* zilizosalia.

**SPIKA:** Sawa. Sasa Waheshimiwa Wabunge, nitamruhusu Mheshimiwa Mgungusi halafu kwenye hoja hii tutafanya maamuzi sasa halafu tusonge mbele. Mheshimiwa Mgungusi.

**TAARIFA**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nafikiri kwa kifupi, mimi sijaona nia ya dhati, tuseme Wizara ya Uchukuzi, kama siyo Serikali juu ya sakata hili la *KADCO* na *KIA*. Maelezo ya Mheshimiwa Waziri na *AG,* yanazungumzia mchakato ulivyokuwa mgumu kuhamisha *KADCO* kwenda *TAA* ambazo zote zinasimamiwa na *TR*. Hatukuazimia kwamba *KADCO* iende *TAA,* hoja yetu ni ule Uwanja wa *KIA* ndiyo wakwetu, Uwanja wa *KIA* uende *TAA,* hauhitaji sheria na mchakato. Kwa hiyo, mchakatao ufuatwe namna ya ku-*dissolve KADCO* au *KADCO* kampuni tanzu ya *TAA,* hilo ni jambo la kisheria la baadae. *Issu*e yetu ilikuwa siyo *KADCO* kama lilivyo, Uwanja wa *KIA* mara moja uende *TAA* ndiyo ilikuwa ajenda hata mwaka jana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la nyongeza tu, nasema nia ya dhati haipo kwa maana ya kwamba, Menejimenti ya *KADCO* wanaendelea kuongea kwamba, Azimio la mwaka jana la Bunge limetolewa lakini bado wao hawatofanya kama vile ambavyo inapaswa, kwa maana *KADCO* itaendelea ku-*run* uwanja. Kwa hiyo, kilichopo sasa hivi wanapambana huko uvunguni, wanafanya *lobbying* kwamba Azimio la Bunge lisitekelezeke. Hicho ndicho kinachoendelea *KADCO* sasa hivi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naona ulisimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, nilisimama kumpatia taarifa Mheshimiwa Mbunge, ninaemheshimu sana kwamba siyo taarifa yangu wala siyo taarifa ya Mheshimiwa Waziri iliyotolewa hapa kwamba Serikali ina mpango wa kuihamishia *KADCO, TAA*.

**WABUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutulie kidogo. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, naona umesimama.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hoja ambayo iko mezani kwetu ni hoja ya *CAG* na hoja hii ya *CAG* ni hoja ambayo inashirikisha pande zote mbili katika kufanya majadiliano. Serikali lakini ni hoja ya Bunge kwa maana ni hoja inayomilikiwa na Kamati za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kama itakupendeza, kwa kuwa bado Kanuni zinaturuhusu ambazo hazizuii mjadala huu kuendelea na kuhitimishwa kwa mujibu wa utaratibu. Kama Bunge lako itakupendeza, Mheshimiwa Waziri ametoa maelezo na Mwanasheria Mkuu amatoa maelezo na kwa kuwa tayari Serikali inaonesha kwamba ina hatua ambazo zimekwishachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kama itakupendeza basi katika Bunge, Mkutano huu Serikali tupate nafasi ya kuja kutoa kauli yetu ya Serikali kuonesha hali halisi ya mahali tulikotoka, mahali tulipofikia

na hasa katika katika kutekeleza agizo la Bunge na kutekeleza maagizo yote ambayo yalitolewa pia na Baraza la Mawaziri ili tuweze kupata uelewa mzuri wa pamoja, ikikupendeza. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA Bunge YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama hapo Mheshimiwa Waziri, pia nafikiri tulimsikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali akiomba pengine wiki ijayo wapewe muda waje watoe maelezo, lakini changamoto iliyopo ni kwamba, kauli za Serikali huwa hazijadiliwi, unasema halafu tunakuwa tumeelewa kwenye hoja hiyo.

Hoja ya msingi iliyopo mezani sasa, ni kwamba Bunge liliazimia, Serikali ikatoa majibu kuashiria kwamba hilo jambo limeshafika mahali, sehemu. Sasa leo tena imekuja na maelezo ya ziada. Kwa sababu hii Taarifa ya *CAG* ambayo inajadiliwa leo ni ya tangu Machi na hapo majibu yalishatokea, yalishatokea yalishatokea. *(Makofi)*

Februari mwakani siyo muda mrefu, lakini hoja iko pale pale. Hii *KADCO* ni ya Serikali na *TAA* ni ya Serikali, yaani *KADCO* inataka kulisimamisha Bunge? Yaani *KADCO* kama kampuni inataka kulisimamisha Bunge? Sawa, tuendelee na michango. Tutafanya uamuzi, sisi ndiyo Bunge tuko hapa na ndiyo kazi yetu kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilishamtaja Mheshimiwa Jumaa Aweso, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, Mheshimiwa Ummy Mwalimu, ajiandae.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, asiyeshukuru watu hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati ya moyo wangu nakushukuru sana Spika wangu. Moja, kwa kutuongoza vizuri lakini la pili, kwa kuaminiwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge yote Duniani. Nataka nikutie moyo, unatosha mpaka chenji inabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nilishukuru sana Bunge lako Tukufu, kwa namna nyingine ninashukuru sana Kamati zako. Moja, kwa michango yao ambayo imewasilisha, hasa juu ya taarifa za *CAG* katika Wizara zetu.

Mheshimiwa Spika, taarifa hizi kwa Wizara yetu ya Maji, imetupa tathmini na kuongeza utendaji na uwajibikaji hasa katika kwenda kuchukua hatua. Hoja ya Kamati iliyoeleza dhidi ya Wizara yetu ya Maji, imezungumza suala la udhibiti wa upotevu wa maji yaliyotibiwa, sitaki nipingane na Kamati, naomba nikubaliane na Kamati, hili tumelipokea na tunaenda kulifanyia kazi zaidi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kiwango cha upotevu wa maji kinachokubalika Kitaifa na Kimataifa, Kitaifa ni asilimia 25 na Kimataifa ni asilimia 20. Mpaka Septemba kwa maana ya mwaka huu, Wizara ya Maji eneo la upotevu wa maji kiwango tulichofikia ni asilimia 36.5. Hiki bado ni kiwango kikubwa, maana yake kuna haja ya kuendelea kupambana na suala zima la upotevu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kazi za utendaji ambazo nimefanya katika Wizara yetu ya Maji, moja, katika hili eneo la upotevu wa maji, kama Wizara ya Maji lazima tukubali kubadilika. Wakati mwingine unaweza ukakuta mwananchi kule chini ama mtaani, bomba linavuja lakini anatoa taarifa, hakuna *response* ya haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili tumeliona na sisi kama Wizara kupitia mamlaka zetu za maji, tumetengeneza *task force* ambapo inapotokea taarifa basi hili jambo lifanyike kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili, jamii ipo na viongozi wapo tu. Ukiwashirikisha utafanikiwa, usipowashirikisha utakwama.

Tunajua huko chini kuna viongozi mbalimbali wa Serikali za Mitaa na viongozi wengine, kupitia mamlaka zetu za maji, maelekezo ambayo tumeyatoa ni kuendelea kushirikiana nao.

Mheshimiwa Spika, pia eneo lingine ni suala zima la taarifa zinazotolewa na Mamlaka zetu za Maji. Kwa mfano, unaweza ukafanya ziara katika Mamlaka ya Maji, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji anakwambia hapa upotevu ni asilimia 46. Unaweza ukamhoji, hebu tupite mtaani tuone asilimia hiyo 46 inayopotea. Kwa sababu unapozungumza asilimia 46 ya maji yapotee, maana yake sisi tunategemea kuwe na mabwawa makubwa kwa ajili ya kufugia samaki, lakini ukipita hauoni, maana yake nini, moja kuna uunganishaji wa kiholela. Kwa mfano, inawezekana kuna baadhi ya viwanda ama hoteli kubwa zimeunganishwa lakini hawasomeki kama wateja ambao wanatumia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ni eneo la wizi wa maji. Tumeendelea kutengeneza uboreshaji kwa maana ya *operation* mbalimbali tunazozifanya na niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge, hili ni jukumu letu sote, tushirikiane kwa ajili ya kupambana na eneo hili.

Mheshimiwa Spika, kubwa ni kwamba, dunia imebadilika na sisi lazima twende huko. Lazima teknolojia zitumike kwa ajili ya kufanya mageuzi na mapinduzi hasa katika eneo la upotevu wa maji. Kwa hiyo, sasa hivi tunajiwekeza katika suala zima la TEHAMA ili tuwe na mitandao ambayo ita-*detect* kwa haraka sehemu ambako kunapotea maji na sisi kama Wizara ya Maji tunakwenda kudhibiti kwa haraka ili Watanzania waweze kupata maji safi na salama. Eneo lingine, …

**MHE. PHILLIPO A. MULLUGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa, taarifa, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbarawa, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mulugo.

**TAARIFA**

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, toka nimeanza kusikia…

**SPIKA:** Samahani kidogo. Mheshimiwa Aweso, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Spika, toka asubuhi hapa nimeanza kusikia *response* za Mawaziri, ndiyo Waziri pekee ambaye nimeanza kumwelewa. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Aweso.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza niendelee kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri kwa kazi kubwa ambazo wanazifanya, lakini kubwa nataka nieleze kwa eneo hili la upotevu wa maji kwamba hili ni jukumu letu sote, tuendelee kushikamana, kuhakikisha kwamba tunapigana katika hili eneo na kuhakikisha kwamba tunaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni suala zima la miundombinu chakavu. Hapa naomba nimshukuru Mheshimiwa Rais, miradi mingi ilikuwa na miundombinu chakavu, lakini kwa kipindi hiki tu kwa mwaka huu vijijini tunatekeleza miradi zaidi ya 1,546; mjini tunatekeleza miradi 2,244. Nini maana yake? Ujenzi wa miundombinu hii itakwenda kupunguza kwa kiwango kikubwa suala zima la upotevu wa maji.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nataka kuzungumza na kwa dhati ya moyo wangu naomba nimpongeze CAG kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. Moja ya maelekezo niliyopewa Waziri wa Maji, tarehe 22 Aprili, 2021 ambapo Mheshimiwa Rais alihutubia katika Bunge lako tukufu, Wizara ya Mji tulipewa maelekezo mahususi. Pamoja na kazi nyingine tulizopewa, lakini kuna kazi ile mahususi. Moja, ni juu ya kukamilisha mradi wa Same – Mwanga. Kwa hiyo, kipaumbele cha Wizara ya Maji pamoja na kazi nyingine, moja, ni Same – Mwanga; pili, ni Same – Mwanga, na tatu ni Same – Mwanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anayelala na mgonjwa ndiye anayejua mihemo ya mgonjwa. Waheshimiwa Wabunge, kaka yangu Mheshimiwa Tadayo na Mheshimiwa Mathayo, wamekuwa wasumbufu juu ya utekelezaji wa mradi huu. Kwa nini nasema nitumie nafasi hii kumshukuru *CAG*, ni kwa sababu huu ni mradi ambao ni wa muda mrefu, takribani sasa ni miaka 10. Mwaka 2021, *CAG* alifanya *special audit* kupitia taarifa yake hii, ndiyo imetuwezesha kutoka mradi asilimia 60, leo hii tuna asilimia 83.

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie, sisi kama Wizara ya Maji, hatutakuwa kikwazo kuhakikisha mradi huu unakamilika ndani ya mwezi wa Sita na wananchi wa Same – Mwanga waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, hoja ya Kamati ambayo imekuja mbele dhidi ya Wizara yetu ni kuhakikisha kwamba inaenda kufanya *audit* tena katika mradi ule. Nataka niwaambie Kamati pamoja na hoja hii, sisi hatutakuwa kikwazo, tutampa ushirikiano *CAG*, kwa sababu nia ni njema katika kuhakikisha kwamba…

**SPIKA:** Sekunde 30.

**WAZIRI WA MAJI:** …mradi huu unakamilika na Watanzania wa Same – Mwanga waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, mwisho hii Tanzania ni nchi yetu na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni Rais wetu. Pamoja na mafanikio mengi ambayo tunayapata, lakini popote kwenye mafanikio hapakosi changamoto.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Muda wake umeisha.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tuendelee kushirikiana, maoni ambayo mmeyatoa, sisi kama viongozi tutaendelea kuyachukulia hatua ili kuhakikisha Watanzania wanapata majisafi, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, atafuatiwa na Mheshimiwa Ummy Mwalimu na Mheshimiwa Profesa Ndalichako ajiandae.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa *IPU.* Jana nilipokutana nawe nilikuomba nikupe mkono na ulipokubali nilisema kwamba nina bahati ya kupewa mkono na Rais wa *IPU*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ana-*support* sekta ya michezo. Tumeshuhudia mafanikio makubwa katika Sekta hii, tume-*qualify* kwa mara nyingine kwenda *AFCON* mwakani na tumekuwa wenyeji wa *AFCON* 2027 na kabla ya hapo tutakuwa wenyeji wa *CHAN*, 2025. Haya yote ni kazi nzuri. Sisi wasaidizi wake tunahakikisha kwamba tunapambana kuiweka Sekta ya Michezo katika muktadha unaostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya michezo, tuna Chuo kimoja cha Michezo kinaitwa Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya. Chuo hiki, kwa asilimia 56.8 kipo katika Mkoa wa Mwanza na asilimia 43.2 kipo katika Mkoa wa Simiyu. Katika miaka minne iliyopita Serikali na Wizara hii na hasa watangulizi wangu wamefanya kazi nzuri ya kuhakikisha wanaboresha miundombinu ya chuo hiki. Takribani shilingi bilioni nne zimewekezwa pale katika kuboresha miundombinu ya ujenzi wa hosteli, kutatua changamoto ya maji, kujenga viwanja na ukarabati wa viwanja vya ndani, kujenga jengo la utawala pamoja madarasa. Kazi yangu ni kuendeleza kazi hiyo nzuri ambayo watangulizi wangu wameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali ni kuendelea kuwa na *center of sports excellence* katika kila Mkoa wa Tanzania. Pale *Malya* tayari ni *center of excellence* na inatumika kama *Center of Excellence for East Africa*, hatuna mpango wa kuhamisha Chuo cha *Malya.*

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, hatuna mpango wa kusema tunaondoa project yoyote *Malya*, tutaendelea na *project* katika mikoa yote. Tunawaomba wenye Mikoa hiyo watupe maeneo kama ambavyo Ilemela wamatupa eneo…

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kasalali Mageni.

**TAARIFA**

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Chuo cha *Malya,* hakina *Center of Sports Excellence* kwa sababu Serikali kupitia Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo ilisaini mkataba wa ujenzi wa kituo hicho. Kwa hiyo, hakipo na kama kingekuwepo Serikali isingesaini mkataba.

Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 22 Agosti, 2021, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akipokea timu ya *under 21* ya Taifa, naomba kwa ruhusa yako nimnukuu alisema maneno yafuatayo: "tuna mpango wa kujenga akademia ya michezo kwenye Chuo cha Michezo cha Malya, Mwanza. Pia kujenga viwanja vitatu vya kisasa vya mazoezi kwenye Mikoa ya Geita, Dar es Salaam na Dodoma, na kuja kujenga *Sports Arena* mbili Dar es Salaam na Dodoma."

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba anachokizungumza kwamba ameshakifanya, hakijafanyika. Kilichofanyika ni mpango mzuri wa Mheshimiwa Rais wa kujenga hiki kitu, na kazi nzuri ya utekelezaji iliyofanywa na Waziri, Mheshimiwa Mchengerwa na Msaidizi wake Dkt. Abbas, ambayo yeye yuko *busy* kuiharibu. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Dkt. Damas Ndumbaro, unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, siipokei hiyo taarifa. Mheshimiwa Kasalali, anapaswa kuelewa nini maana ya *Center of Excellence? Center of Excellence* ni kituo cha umahiri ambacho kinatoa huduma stahiki kwa Tanzania kwenye michezo. Kwa Afrika Mashariki *our Center of Excellence* ni *Malya*. Atofautishe na academia. Nukuu aliyoisema ya Mheshimiwa Rais inasema, 'akademia,' itajengwa akademia pale *Malya*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa akademia ni kuendele kuimarisha *Center of Excellence*. Kwa hiyo, asichanganye nukuu ya Mheshimiwa Rais ya ujenzi wa akademia…

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Damas Ndumbaro, inaonekana kuna kanuni inavunjwa. Mheshimiwa Kasalali Mageni.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu, Mheshimiwa Waziri, ameamua kulidanganya Bunge hadharani kwa sababu, kwa mujibu wa barua ambayo Wizara yake iliiandikia Halmashauri ya Ilemela, nanukuu: "Yahusu Maombi ya Kiwanja Na. 677A, Losi Busweru cha Ujenzi wa Kituo cha Ufundishaji Michezo kwa Ubora."

Mheshimiwa Spika, kwa barua ambayo *consultant* aliwaandikia Wizara kwamba, naomba niisome kidogo kwa ruhusa yako.

**SPIKA:** Sawa. Sasa ngoja kidogo…

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Spika, kwa barua hii ambayo wao walimwandikia *contractor* wakiomba kuhamisha *Center for Excellence*, kutoka Malya ambayo mkataba umesainiwa na Serikali imesaini Mkataba wa Ujenzi wa *Center for Excellence* Malya, na wao wanaomba kuhamisha *Center of*

*Excellence* ya Malya kupeleka Ilemela, halafu Waziri anasimama na kulidanganya Bunge kwamba ilishajengwa, sasa atuambie hapa, kwamba huu mkataba ambao tunao hapa ni wa Serikali au ni wa nani? Ulikuwa ni wa kujenga nini pale Malya? *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge, hoja hii alipokuwa amechangia Mheshimiwa Kasalali Mageni, aliihusisha na Taarifa ya *CAG* kwa maana ya kwamba utaratibu usipofuatwa ndiyo inapelekea zile hoja za *CAG*. Sasa, naona mjadala wetu unakoelekea tutatoka nje kabisa ya Taarifa ya *CAG*. Sasa nataka kufanya maamuzi juu ya jambo hili ili tumalize Taarifa za *CAG*, halafu kuna mambo kama mawili matatu hivi ambayo yatatuhitaji kuyafanyia kazi.

Kwa hiyo, kwa sababu lililetwa hapa Bungeni na linataka kutupeleka nje ya taarifa ambayo tunayo, kwa sababu, Mheshimiwa Kasalali, aliitumia hiyo kama mfano, siyo kwamba ipo kwenye Taarifa ya *CAG* kwamba, pengine kuna jambo liko namna Fulani; sasa, tukubaliane hivi, Mheshimiwa Waziri kuhusu hoja hii utapewa nafasi baadaye. Mheshimiwa Kasalali Mageni, kuhusu hoja hii utapewa nafasi baadaye. Tutoe nafasi kwa Mheshimiwa Waziri kutoa ufafanuzi juu ya hoja zingine.

Hoja ya kuhamisha hiyo sijui ni uwanja wa mpira ama ni *Center of Excellence* ama ni akademia, kutoka Kwimba kuelekea Ilemela tutaijadili baadaye kidogo. Tumalizie kwanza hoja ya *CAG*.

Waheshimiwa Wabunge, nadhani tumeelewana vizuri. Tumeelewana vizuri?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyo. *(Makofi)*.

**SPIKA:** Sawa. Mheshimiwa Waziri, kwa sababu utapata nafasi baadaye kidogo ya kutoa ufafanuzi kuhusu jambo hili, maana Mbunge baada ya kukupa hii taarifa nimeona linatoka kabisa nje ya Taarifa ya *CAG*. Kwa hiyo, kama unayo mengine ya kufafanua ni sawa, kama huna, basi tuliache hili, nitakupa nafasi baadaye ili tuwe na jambo hilo Mezani. Ni sawa Mheshimiwa Waziri?

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ni sawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Wabunge, tunasonga mbele. Mheshimiwa Ummy Mwalimu, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndalichako na Mheshimiwa Masauni, ajiandae.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Vile vile nakupongeza kwa kuongoza vema Bunge letu. Pili, nawapongeza sana Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati zote tatu, *PAC*, *LAAC* na *PIC* kwa taarifa zao nzuri ambazo sisi kama Sekta ya Afya kupitia Wizara ya Afya tunazipokea na mapendekezo yao yote tunayapokea na tunawaahidi kwamba tutayafanyia kazi. Kipekee nampongeza sana *CAG* kwa kufanya kazi yake ya kikatiba ya kudhibiti na kukagua fedha za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee tunataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba kila senti inayotolewa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa ajili ya kuboresha huduma za afya tutaisimamia kikamilifu. Katika kipindi cha miaka miwili tunamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sekta ya Afya tumepokea shilingi trilioni 6.7, haijapata kutokea katika historia ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, niruhusu sasa nijielekeze kwenye hoja kama tatu ambazo zimeletwa kwenye Bunge lako tukufu. Kamati ya *PAC*, *PIC* na *LAAC*, walileta hoja kuhusu *MSD*. Suala la kwanza la *MSD* ni suala la ukiukwaji wa sheria katika ununuzi wa vifaatiba kutoka kampuni ya Misri ya Alhandasya, shilingi bilioni 3.4. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, tunazingatia sheria, kanuni na taratibu. Sisi kama Serikali tumeanza kuchukua hatua za kiutawala ambapo Mtendaji Mkuu wa *MSD* tulimwondoa tarehe 12 Aprili, 2022. Hatukuishia hapo, tumeondoa Wakurugenzi sita wote wa *MSD*, Mkurugenzi wa Fedha na Mipango, Mkurugenzi wa Ununuzi, Mkurugenzi wa Utawala,

Mkurugenzi wa Usambaaji wa Huduma za Kanda, Meneja wa Sheria na Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa *MSD*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, unaweza ukaona dhamira ya dhati ya Serikali katika kuwashughulikia watu wanaotuhumiwa kutenda ubadhirifu katika fedha za Umma. Kama haitoshi…

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ummy Mwalimu, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa mchango anaoendelea nao, amekiri kwamba kulikuwa na ukiukwaji wa taratibu na waliohusika waliondolewa. Moja kati ya kilio cha Wabunge na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, ni watu kuondolewa kutoka kwenye eneo moja kwenda eneo lingine. Aliyekuwa sasa Msimamizi ambaye alikuwa Mwanajeshi, ameondolea amepelekwa Jeshini. Yuko hai, alihusika katika hiii mikataba na fedha kupotea. Tunataka sasa tujue ni hatua gani zilichukuliwa, pamoja na kumkamata yeye ili tusaidie kurudisha hichi kiasi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa, Ummy Mwalimu.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, tumeapa mbele ya Bunge lako tukufu kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, lazima tufuate Sheria na Kanuni za Kiserikali. Mheshimiwa Simbachawene, ameeleza vizuri, vyombo vyenye mamlaka ya kufanya uchunguzi wanaendelea na kazi. Kwa sababu, sheria yetu inazungumzia *presumption of innocent*, ndiyo maana tumechukua maamuzi ya kiutawala, tuache vyombo vifanye kazi yao ya taratibu nyingine za kijinai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kuwahakikishia, hatukuishia tu kwenye Wakurugenzi sita wa *MSD*, tumebadilisha Mameneja

wa Kanda wote nane wa *MSD*. Kwanza, sisi Wizara ya Afya hatukusubiri hata Taarifa ya *CAG*. Tulifanya *special audit* wenyewe, tukaleta humu na baadhi yetu sisi tulituhumiwa na baadhi ya Wabunge kwamba sisi tunawaweka pembeni baadhi yao, lakini tulikuwa tunajua tunachokifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba niseme, kila senti ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inayopelekwa kwenye Sekta ya Afya tutaisimamia. Nitume salamu kwa watendaji wote wa *MSD* na wengine katika Sekta ya Afya, hatutawavumilia. Tutachukua hatua mara moja ili kulinda fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la pili ambalo kwa sababu ya muda ni suala ya Bohari ya Dawa. Hii ni hoja ya *LAAC* kutopeleka dawa na vifaa tiba shilingi bilioni 8.6.

Mheshimiwa Spika, suala hili tayari tumeshalifanyia kazi, kwa mfano Halmashauri ya Mbinga walikuwa wanadai milioni 577 vifaa tiba wamepokea vifaa tiba vya milioni 846. Maswa walikuwa wanadai milioni 558 wameshapelekewa bidhaa za milioni 810. Pia Dar es Saalam walikuwa wanadai bilioni 2.9 wamepelekewa vifaa vyenye thamani ya bilioni 2.8.

Mheshimiwa Spika, kubwa ambalo nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, yapo mabadiliko makubwa ndani ya *MSD*. Tukiangalia thamani ya bidhaa zilizosambazwa na *MSD* mwaka wa fedha 2021/2022 wamesambaza vifaa vyenye thamani ya bilioni 315, mwaka 2023 375 kwa hiyo ongezeko la bilioni 58. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaangalia pia mapato *revenue*. Mwaka jana *quarter* ya kwanza *MSD* alipata mapato ya bilioni 77.9 *quarter* ya 2024 *MSD* imepata mapato ya bilioni 113. Hii inaonyesha maoni na ushauri wa Wabunge tumeufanyia kazi na niwaambie Waheshimiwa Wabunge tutaendelea kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna suala la *MSD* kupokea dawa ambazo zinakaribia kuisha muda limeletwa na Kamati ya *PIC* ni

kweeli mwongozo ambao unatutaka tupokee bidhaa za dawa zinatakiwa zisiwe chini ya miezi 28 au 80% lakini pia kama Wanasheria wanavyojua kwenye *general rule* lazima kuwe na *exceptions* kwa hiyo, ipo sheria inayoturuhusu.

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya bidhaa mnaweza mkazipokea chini ya wiki, chini ya *shelf life* ya wiki 24 pale ambapo bidhaa hiyo inaweza kutumika kwa ajili ya kutibu magonjwa mahususi. Kuna vitu vitendanishi vinaitwa *control*, hivyo vinazalishwa ndani ya miezi mitatu kwa hiyo miezi sita ni lazima pia uvipokee chini ya muda huo.

Mheshimiwa Spika, naenda haraka haraka suala la Njombe kwamba *MSD* alinunua mashine ya bilioni 6.3 haijafungwa. Zipo changamoto tunaendela kuzifanyia kazi lakini pia lazima tuongozwe na Taarifa za Kitaalamu. Jambo hili naomba niseme Kamati ya *PAC* tumelipokea na tutakuja kuleta ufafanuzi zaidi juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, nimalize suala la *PAC* kuhusu *NHIF*. Hili ni suala la madeni kwamba *NHIF* wanaidai Serikali bilioni 228. Waheshimiwa Wabunge tumemsikia Waziri wa Fedha katika *budget speech* hapa wamehaidi kwamba wataanza kurejesha deni hili Wizara ya Mambo ya Ndani bilioni 45, Taasisi ya Mifupa *MOI* bilioni 18.2 *NIDA* bilioni 17.3 na Hospitali ya Benjamini Mkapa bilioni 129 wenzetu Wizara ya Fedha tayari wameshalihakiki deni hili na wameahidi kulilipa ili kulinda uhai na uendelevu wa *NHIF*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kengele ya pili ilishagonga.

**WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Joyce Ndalichako atafuatiwa na Mheshimiwa Mhandisi Masauni, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba jiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja za Kamati zetu tatu ambazo zimewasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, niwapongeze sana Wajumbe wote wa Kamati hizi tatu kwa uchanbuzi wao wa makini na niseme kwamba Wizara yetu imepokea mapendekezo, maoni na ushauri ambayo yametolewa na Kamati na tutaufanyia kazi ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea na kuchangia hoja hii naomba nimpongeze kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muuungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuiongoza Nchi yetu kwa weledi, kwa kuchukua hatua mahususi za kuhakikisha kwamba analeta ustawi kwa Watanzania za kuhakikisha kwamba anatatua kero za muda mrefu katika baadhi ya maeneo ambayo yameguswa na taarifa ambazo zimewasilishwa na kamati zetu makini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo Kamati zimezungumzia ni madeni ya muda mrefu ya kwenye mifuko. Mfuko wa *PSSF* ulikuwa na deni la trilioni 4.600 ambalo lilitokana na deni la tangu mwaka 1999 ambapo Serikali ilipoanzisha mifuko iliamua kuchukua jukumu la kulipia wafanyakazi wote waliokuwa wameajiriwa kabla ya Julai 1999.

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali imechukua uamuzi huo mwaka 1999 fedha hizo zilikuwa hazijawahi kulipwa mpaka Disemba 2021chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nampongeza kwa dhati kwa kweli kwa sababu hatua hiyo imeimaarisha sana mfuko wetu wa *PSSF*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, alikuta deni la mfuko wa *PSSF* la bilioni 731 na tayari Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekwishalipa kiasi cha shilingi bilioni 500. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuta pia kuna kero kubwa ya baadhi ya waajiri kutopeleka michango ya wastaafu ambayo imesababisha Wabunge kwa vipindi tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata Kiti chako umeshakuwa ukizungumzia suala hili la madeni marefu ya waajiri kwenye mifuko ambayo yanasababisha wazee wetu ambao wamefanya kazi wa weledi kulitumikia Taifa hili wanapata usumbufu wa kupata mafao yao. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alitoa maelekezo na aliyarudia maelekezo yake hata wakati wa Mei Mosi kwamba Wizara yetu ichukue hatua mahususi za kufuatilia madeni hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelekezo hayo, lakini kama ambavyo hata Ripoti ya *CAG* kwenye Taarifa ya *PAC* imebainisha kwamba *NSSF* walikuwa na michango ya kiasi cha shilingi bilioni 408 ambazo zilikuwa bado hazijakusanywa kutoka kwa waajiri mbali mbali.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais na kwa kuzingatia kwamba hizi ni hoja za muda mrefu kwa kweli niseme kwamba *CAG* pamoja na Mheshimiwa Rais ametusaidia kufikiri nje ya *box*, ametuwezesha tumeunda Kamati Maalumu ya kufatilia fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nilijulishe Bunge lako Tukufu tangu tumepokea Ripoti ya *CAG* kutokana na kazi kubwa na nzuri ambayo imefanywa na timu mahususi ambayo tumeiunda tumefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 200.6 kati ya bilioni 408 zilizobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafurahi kwamba Bunge lako kwa kweli linazungumza kwa hisia kwa uchungu kwa sababu haya ni maisha ya watu, haya ni maisha ya wazee wetu ambao ndiyo walituwekea misingi sisi leo tunajivuna katika Taifa hili ni kwa sababu kazi kubwa ya hawa wazee wetu mbao ni wastaafu waliifanya kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa namna yoyote ile ni lamiza Serikali tutahakikisha kupata fedha zilizobaki ambazo bado hatujakusanya tutahakikisha tunazifanyia kazi…

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU**: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndalichako kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Jesca Msambatavangu.

**TAARIFA**

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa maelezo mazuri ya Mheshimiwa Waziri na *task force* aliyoiunda. Tunafahamu kwamba wamekaa kikao cha *Mock LAAC* kati ya Septemba na Oktoba ambacho kina-*clear out* zile hja zote za *CAG* kwa maelezo haya anayosema kwa *task force* waliyoiunda. Nataka kujua hiyo *task force* yake anasema imefanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Spika, mpaka tunakuja sasa hivi kwa Taarifa hii *CAG* ametuambia wapo wafanyakazi wa Jiji la Tanga walichangishana milioni 8 wakailipa *PSSSF* ili wapate mafao yao. Kwanza nataka kujua hiyo *task force* yake inajua kwamba hilo linafanyika, na wamechukua hatua gani, na je? … *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Msambatavangu Taarifa ni moja. Ahsante sana

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, naomba hiyo *task force* yake imefanya nini kwenye masuala, na wanakusanya hiyo michango kwa Sheria ipi unakwenda kuchukua mchango kwa mtumishi au mstaafu na sio kwa mwajiri.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndalichako. Ameuliza swali kwa hiyo hulazimiki kujibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, sawa lakini kwa faida ya Wabunge taarifa hii ya Kamati bahati nzuri ime-*acknowledge* haya ambayo tunayasema. Mafanikio haya yaliyopatikana tungeyaripoti kwenye kamati na Kamati imeonyesha kwamba

kulikuwa na deni la milioni 407 na ikasema kwamba wakati Kamati inafanya kazi yake jumla ya bilioni 194 zilikuwa zimekusanywa.

Mheshimiwa Spika, hatulali. Tangu kipindi cha Oktoba tulipotoka kwenye Kamati tumeshakusanya bilioni 6 nyingine. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, naomba niendelee kwenye eneo lingine.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Profesa Ndalichako kuna Taarifa nyingine kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, mimi ni Mjumbe wa *LAAC*, ni jeshi ulilonihamishia hivi karibuni nilikuwana napenda kumpa Taarifa Mheshimiwa Waziri kwamba mpaka juzi kwenye halmashauri michango ambayo haijapelekwa kwenye mfuko bilioni 260 ya watumishi wa Taifa hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Waziri Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, dada yangu Ester Bulaya anawaisha shughuli. Anachokisema ndiyo ilikuwa sehemu ambayo naendelea na mchango wangu. Ni kweli kwamba katika halmashauri zetu kumekuwa na michango ambayo haijawasilishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama navyosema tupo kazini kuhakikisha kwamba hii kero ya muda mrefu tunaifanyia kazi. Katika michango ya halmashauri tuliunda na yenyewe hiki kikosi kazi kilikuwa kinashughulikia mfuko wa *NSSF* lakini na *PSSSF* tulikuwa na

*task force* nyingine kwa sababu hawa ni watumishi wa umma ambao ilijumuisha Makatibu Wakuu wanaohusikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika TAMISEMI naomba niripoti kwenye Bunge lako kwamba tayari…

**SPIKA:** Ngoja amalizie.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, tayari tumeingia makubaliano na halmashauri 81 ambazo zina madai ya muda mrefu na halmashauri hizi 81 zimetuwezesha kuwakomboa wastaafu 1425 ambao walikuwa na madeni ya muda mrefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia kwa faida ya Watanzania na kwa sababu hili jambo limekuwa ni kero ya muda mrefu nichukue nafasi hii kumwagiza Mkurugenzi Mkuu wa *PSSSF* kuzifuatilia halmashauri ya 103 ambazo hazijaweka makubaliano ya namna gani wataleta michango yao. *(Makofi)*

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

Mheshimiwa Spika, nimuombe kaka yangu Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Mchengerwa mchapakazi mtu bingwa nitakukabidhi orodha ya hawa watu wa TAMISEMI ili waweze kuleta fedha tuweze kulipa mafao wastaafu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri umemaliza mchango wako kuna Mbunge alikuwa anataka kutoa Taarifa, itabidi, maana dakika yake ya mwisho ilikuwa imeshaisha lakini namna unavyosisitiza ni kama vile una jambo la dharura.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa mawasilisho ya Waziri. Kuna wastaafu ambao walishastaafu na wakaamua kwenda kukopa fedha kwengine ili waende walipe yale malimbikizo ambapo hawajapeleka pamoja na penati sasa wakishalipa ina maana wanalipwa fedha zao kutoka kwenye mfumo tayari unakuta hawasomeki.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nampa Taarifa kwamba hiyo *task force* aliyoiunda ihakikishe kwamba inawafatilia wale wote ambao wameshatoa hela zao wakalipa yale malimbikizo kwa hela zao zingine kwa sasa walizopata na penati ili wawatafute wahakikishe kama wanalipa zile fedha zao kihalali warudishiwe zile hela ambazo walikopa kwa…

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Waziri Ndalichako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Watanzania kwa sababu suala la wastaafu linaguza wazee wetu na wazee ni nuru ya Taifa. Kwa faida ya wazee wetu niseme kwamba utaratibu ambao upo Kisheria *control number* ya kulipa michango inapelekwa kwa mwajiri.

Mheshimiwa Spika, sasa kama kuna mwajiri ambaye anampa mtumishi ile *control number* ili akalipie tupate taarifa tutashughulikia kwa sababu utaratibu wa Kisheria upo kwa hiyo, tumepokea ushauri wake.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge kama wanafahamu waniletee tutafanyia kazi, ni hilo tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mhandisi Hamad Masauni, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe ajiandae.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Mimi sina shaka yoyote ju ya dhamira ya Waheshimiwa Wabunge katika hoja ambazo wamezizungumza na *concern* yao hususani kwenye kudhibiti fedha za umma. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba dhamira yao hiyo hiyo ndiyo dhamira ambayo Serikali yao inayo chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nithibitishe kauli yangu hiyo kwa hoja zilizoguswa kuhusu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi katika Ripoti ya *CAG* na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati. Hoja kubwa ambazo zimeguswa ni hoja mbili.

Mheshimiwa Spika, nitaomba nichukue nafasi hii kuweza kutoa ufafanuzi huo kwa utaratibu wa kujiuliza swali mwenyewe na kujijibu mwenyewe. Wakati nitakapojijibu inawezekana ikawa inatosha kuweza kutoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, swala langu la kwanza nilikuwa nataka kujiuliza ni kwamba je sasa hivi, katika kipindi hiki cha Serikali hii wizi, ubadhilifu, ufisadi, unazidi, umekuwa mkubwa zaidi kuliko wakati mwingine wowote au kinyume chake?

Mheshimiwa Spika, hoja za *CAG* ambazo zimegusa Wizara yangu mbili. Moja ni hoja ambayo inahusu mfuko wa tozo na tozo na nyingine inahusu mfuko wa kufa na kuzikana. Majawabu haya ni vizuri yakajibiwa kwa *facts and figures*. Nikichukua hayo maeneo mawili ni maeneo ambayo yamegusa tuhuma nzito na kubwa sana na yametikisa chombo chetu muhimu sana kinacholenga kulinda usalama wa raia na mali zao hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kimetikisa heshima yake, kimetikisa heshima ya Taifa ya chombo hiki kikubwa. Sio jambo dogo hizi tuhuma na shutuma, lakini tuhuma na shutuma hizi hazijatokea kipindi hiki lakini zinarekebishwa kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda tunaweza tukajiuliza kwamba kwanini tunafanikiwa maana mafanikio ni makubwa. Leo *CAG* inazungumza Ripoti kwa uwazi kama hivi, Bunge linazungumzwa

kwa uwazi na uhuru wametuongoza vizuri kwa uwazi kabisa na uhuru wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, hakuna Mbunge ambae umeacha kumpa nafsi. Haya ni mafanikio makubwa ya kujadili. Uwazi huu na mafanikio haya yana sababu zake na kila maji yanaanzia kwenye mkondo na samaki huanzia kwenye kichwa hatuwezi kuacha kumpongeza Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mkuu wa Nchi Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uwezo wake mkubwa wa uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni ishara ya uwezo mkubwa wa Kiongozi na ndiyo maana leo Taasisi zote muhimu zinafanya kazi zake nzuri kwenye Bunge hili, mihimili yote inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya mafanikio ni kwa sababu Amiri Jeshi Mkuu ameweza kutafsiri *vision* yake ya wapi anataka Taifa liende kwa kuwapa imani, kuwa-*inspire*, kuwa-*motivate* vyombo na watu wanaoitwa mamlaka sisi tusimamie. Leo hii hata mimi katika Wizara niliyopewa dhamana sisubiri kusukumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siwezi nikaona jambo lolote, doa lolote linajitokeza na tukaweza kulifumbia macho. Swali la pili je taasisi hizo mlizoziorodhesha chache TAKUKURU, Jeshi la Polisi na mengineyo na viongozi wanatimiza wajibu wao? Ama Serikali inalea wezi, serikali inalea wezi?

Mheshimiwa Spika, jambo moja ni muhimu sana Waheshimiwa Wabunge wakajua kwamba hoja hizi mbili na mimi nasema haya wazi kabisa na kama ninachokisema hiki nachozungumza hapa nitakuwa nashindwa kukitetea hakina ukweli, nasema mbele ya Bunge hili na wananchi wa jimbo langu wananisikia mimi niko tayari kuacha siasa.

Mheshimiwa Spika, nikiacha siasa maana yake Uwaziri haupo, Ubunge haupo ntarudi kwenda kushika spana. Lakini ninachokwambia ni kwamba haya ambayo tunayazungumza leo haya hayakutokana na uvumbuzi wa CAG, yametokana na

maamuzi ya Serikali ambayo tulimwandikia sisi barua kufanya ukaguzi huu wa matatizo ambayo yametokezea kipindi kirefu nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiyo ilielekeza ukaguzi huu. Nihakikishe kwamba kila hatua anayochukua ni stahiki. Nachukua fursa hii kumpongeza *CAG* kwa kazi nzuri uliyofanya, nipongeze Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge kwa kujadili vizuri Ripoti hii ya *CAG*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie, kama ambavyo tumeanza kuchukua hatua, nitazieleza hatua gani, na hatua ambazo hazijachukuliwa zitaendelea kuchukuliwa kwa kuzingatia maoni yenu.

Mheshimiwa Spika, suala lingine la tatu ambalo nataka nilizungumze, hatua gani ambazo zimeshakuliwa dhidi ya wabadhirifu hao. Kwanza nataka nieleze kitu kimoja; *CAG* anafanana kidogo na polisi, sema yule anashiriki masuala ya jinai na yule anashiriki masuala ya kifedha. Polisi anapomkamata mhalifu anafanya uchunguzi, na akimaliza anapeleka kwa *DPP, DPP*, anaangalia uzito wa ushahidi uliokusanywa kama unajitosheleza kumpeleka mtuhumiwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, *CAG* anafanya uchunguzi wa kifedha kuangalia *compliance* ya matumizi ya fedha. Sasa leo hii tukisema mtu ambaye ametajwa, tena hajatajwa waziwazi katika Ripoti ya *CAG* aende jela hiyo sio misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie, wale wote ambao wamethibitika bila shaka yoyote kuhusika wamechukuliwa hatua. Na nina orodha hapa, nina jedwali hili lina majina na hatua ambazo kila mmoja alizochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda…

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, watu ambao wamefikishwa mahakamani mpaka sasa hivi ni watu 18…

**SPIKA:** Mheshimiwa aliyesema taarifa.

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, huku taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, watu ambao wamefukuzwa kazi ni…

**SPIKA:** Mheshimiwa Masauni, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ravia.

**TAARIFA**

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Waziri; Ni kweli kachukua hatua lakini kwa askari wadogo tu, wale wakubwa bado wanaendelea kula maisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masauni, unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, siipokei kwa sababu inaonekana Mheshimiwa Mbunge, alikuwa anasinzia wakati nazungumza, hakunisikiliza.

**SPIKA:** Hapana, ngoja, Mheshimiwa Waziri, hebu mwombe radhi Mheshimiwa Mbunge na ufute hayo maneno.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimefuta hayo maneno na nimemwomba radhi... *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hizo ni tuhuma zote ya kwamba Mheshimiwa Mbunge alikuwa alisinzia. Anafuatilia mjadala ulioko hapa Bungeni. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, namwomba radhi swahiba wangu, Mheshimiwa Mbunge wa Makunduchi, tuelewane. Namwomba radhi na ninafuta, nina hakika hajakasirika kwa sababu ni rafiki yangu sana na anaelewa tunataniana mengi tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kumwomba radhi Mheshimiwa Mbunge na kufuta kauli hiyo, naomba niendelee.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masauni, ngoja, Mheshimiwa Ravia, naona bado umesiama.

**MHE. RAVIA IDARUS FAINA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimfahamishe Mheshimiwa Waziri kwamba, heshima ni kitu cha bure, lakini la pili ni kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC, ninachokiongea ninakijua kwa silimia mia. Kwa hiyo sijasinzia na ninachokiongea ninakielewa. Waliochukuliwa hatua ni wadogo na wakubwa bado wanaendelea kula maisha.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge, nadhani kwa sababu Mheshimiwa Waziri wakati amesema ile sehemu yake ya mwanzo pengine kwa sababu ya zile kelele haikuwa imesikika, lakini mimi nilimwacha aendelee na mchango kwa sababu alishasema. Ameanza kwa kusema naomba radhi, huyu ni swahiba, kwa hiyo watu hawakusikia lile neno la naomba radhi nadhani ndiyo maana watu wameendelea na hizi kelele.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ameomba radhi na amezungumza na hayo ya ziada, Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nilikuwa nimefikia kwenye takwimu za watu ambao wamechukuliwa hatua mbalimbali...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja, malizia mchango wako, kengele ya pili ilihsapigwa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika takwimu hizi za watu, kama ningesema nitaje majina ingeonekana ni wakubwa kiasi gani kwa maana tafsiri ya ukubwa ni pana sana lakini nina orodha ya watu waliofikishwa mahakamani, waliofukuzwa kazi na waliosimamishwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu ambao inasemekana walitoroka, lakini miongoni mwao hivi sasa wameshaanza kupatikana...

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** ...kuna mmoja amepatikana juzi, kwa hiyo kuna hatua nyingi ambazo zimeshachukuliwa kwa yale mambo ambayo yameshathibitika na hatua nyingine za kuweza kupata uthibitisho iliwaweze kuchukuliwa hatua zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka nizungume kwa haraka haraka…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Ni kudhibiti mifumo, ni kwamba, Je…

**SPIKA:** Mheshimiwa Masauni, muda wako umekwisha kengele ilikuwa imeshagonga nikakupa muda wa ziada. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimeshamtaja Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, atafuatiwa na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa ajiandae.

**WAZIRI WA FEDFHA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia. Awali ya yote na mimi

nipongeze Taarifa za Kamati na nimpongeze *CAG* kwa kazi kubwa ambayo ameifanya.

Mheshimiwa Spika, ninapoanza, niwaombe Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania tukubaliane yalikoanzia mafanikio haya makubwa ya leo yameanzia mpaka yamefika hapa, maana naona tulianza pamoja lakini kwenye kuvuna naona kama tunatawanyika.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii na hata Watanzania watakuwa mashahidi, imewasilishwa kwa namna tofauti kuanzia kwa *CAG* na imejadiliwa na Bunge kwa namna ya tofauti.

Mheshimiwa Spika, wengine ambao tumekuwemo humu tumeanzia mbali, tulikuwa wote humu. Kuna mambo ambayo tulikuwa tunayalalamikia na Bunge limesema kwa miaka yote. Wabunge wamelalamika miaka yote na wananchi wamelalamika miaka yote na Serikali ilikuwa inaona lakini ilikuwa haijatoa majawabu ya matatizo yale yanayojitokeza.

Mheshimiwa Spika, mambo yale yalikuwa yapi? Nianze na la kwanza; na Mbunge mmoja alisema pale na wewe ukaunga mkono; kwa sheria tulizokuwa nazo na kwa aina ya ukaguzi tuliokuwa tunaufanya ilikuwa inawezekana kuanzia bajeti inavyopita, mradi unapobuniwa, taratibu za manunuzi zinavyofanyika; taratibu zote zinafanywa lakini mradi unakuwa hauna thamani ya fedha iliyotumika. Hivyo tukasema huku ni kuiba kwa mujibu wa sheria. Lilikuwa linafanyika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa miaka yote *CAG* alikuwa anakagua *compliance*, utaratibu wa kiuhasibu tu ndio aliokuwa anakagua *CAG* kwa miaka yote.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati watakumbuka, nilipoteuliwa Waziri wa Fedha jambo la kwanza ambalo Mheshimiwa Rais alilonituma; na bajeti ikiwa imeshafungwa; Bajeti ya *CAG* inapitishwa na Kamati ya Bajeti, ilikuwa imeshafungwa, imepitishwa ya kutekeleza *compliance*. Mheshimiwa Rais akasema hapana, hatuwezi tukaendelea na utaratibu wa

kukagua *compliance*, yaani kukagua na kubariki watu wanaoiba kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Rais, akasema nenda kaiombe Kamati, ifungue bajeti ambayo ilishapitisha tumuongezee *CAG* fedha anazotaka ili aanze kukagua *real time*, akague *value for money*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilienda kuongea na Mwenyekiti wa Kamati nikamwambia hii bajeti mlishaipitisha lakini tunaomba tumwongezee *CAG* fedha. Nikaongea na *CAG* akaniambia fedha anazotaka.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, sahani…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Subiri kidogo Mheshimiwa Tabasamu. Mheshimiwa Waziri nikuombe, unapozungumza, ukigeuka nyuma maneno yale hayaingii kwenye Taarifa Rasmi za Bunge. Kwa hiyo jitahidi hapo hapo kwenye kisemeo ili tuyapate hayo maelezo kwenye Taarifa Rasmi za Bunge maana ukigeuka nyuma hatuyapati. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba wasinisemeshesemeshe maana nilishashika kasi hapa, waniache niseme ili tuelewane.

Mheshimiwa Spika, ninachosema ni nini; niliongea na *CAG,*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA:** ...nikamwambia Mheshimiwa Rais anataka aongeze fedha ukague *value for money*, thamani ya fedha, *real time audit,* ukague kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kuna taarifa.

**WAZIRI WA FEDHA:** Nikaongea na Kamati wakaongeza zaidi ya bilioni tano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nchemba, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Tabasam.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri anasema kwamba akaongeza pesa katika bajeti ya *CAG*. Bunge hili ni Bunge linaloendeshwa kwa tamaduni za Jumuiya ya Madola. Je, Jumuiya ya Madola tunatoa asilimia ngapi kuipa bajeti Ofisi ya *CAG*, aeleze umma wa Watanzania maana anapewa ela ndogo kiasi hicho wakati anatakiwa apewe asilimia kumi ya bajeti ili tukague miradi yote ya Serikali nchi nzima.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba.

**WAZIRI WA FEDHA:** *Yeah, wang'wise* huyo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo baada ya hapo tukakubaliana na Kamati tuongeze fedha ya kwa ajili ya kuanza kukagua *real time*. Wengine labda wanaweza wakasema wang'wise ni jambo baya, Wang'wise ni kaka yangu, yaani nimesema huyu ni kaka yangu, sijampa jina hata la tuzengano ni kaka yangu, *wang'wise ng'wanuyo*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tukaongeza bilioni tano kwa ajili ya kumwezesha *CAG,* aanze kufanya *real time audit,* na hiki, Mheshimiwa Rais ndiye aliyesema sitaki kuona watu wanaendelea kukagua *compliance* ambayo inawafanya watu waibe kwa utaratibu; hapo ndipo tulipoanzia. Kwa hiyo, bajeti ya mwaka ule uliotangulia ilikuwa takribani bilioni 78 tukaipeleka mpaka sasa imeshafika 97 kwa ajili ya *CAG,* na ndipo mwaka 2020/2021 akaanza na akakagua, alianza na *technical audit* nne. Mwaka uliofuata akapeleka nane na mwaka uliofuata 11.

Mheshimiwa Spika, jambo hilo limewezekana tu baada ya kuanza kukagua *value for money* halafu *real time*. Yaani mradi ukiwa unaendelea; na ndipo *CAG* anapofanya kazi yake ya

udhibiti; anaendelea kukagua. Amefanya hivyo kwenye miradi mikubwa.

Mheshimiwa Spika, jamani Afrika yetu tunaijua, ni mara chache sana nchi za kiafrika zinakuwa na Rais anayeweza kumwambia *CAG* usipepese macho kwenye taarifa. Mbona tunataka kusahau mapema? Ni marachache sana Afrika Rais anamtuma *CAG* akakague miradi mikubwa ya kimkakati tena ikiwa inaendelea. Amekagua miradi ya barabara, amekagua miradi ya kilimo na miradi yenyewe sio ya kitoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye barabara ameenda kukagua Daraja la Busisi likiwa linaendelea, kwenye umeme amekagua bwawa likiwa linaendelea. Ameenda kukagua reli ikiwa inaendelea. *Irrigation schemes* zinaendelewa kujengwa na *CAG* yuko *site* kukagua na haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais na ameweka fedha mahususi kukagua *value for money* sio vitabu...

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia.

**WAZIRI WA FEDFHA:** ... kama kweli wote tuna nia njema, Je, kuna mtu anaweza kuwa na nia njema zaidi ya aliyetoa fedha ziende kukagua….

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Nchemba, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Anatropia.

**TAARIFA**

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, nashukuru, nimpe taarifa Mheshimiwa Waziri, kaka yangu anayeongea. Itakuwa ni moja kati ya makosa makubwa kudhani kwamba Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kupewa fedha kiasi gani na kukagua ije kwa hisani. Kwanza anakagua kwa mujibu wa sheria na kuna kaguzi za aina tofauti tofauti. Ni wajibu wetu na wajibu wa Serikali kuhakikisha inamwezesha na si tu audit…

**SPIKA:** Haya, ngoja.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** ...tunayoifanya, tufanye *forensic audit* ili tuweze kuwakamata na hizo ndio ripoti zinazoweza kwenda mahakamani.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, unapokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, mimi sina hata haja ya kubishana na taarifa yake. Ninachomsisitizia ndicho na yeye anachosema. Tunachosema ni kwamba cha kwanza kilichotangulia ni *political will.*

*Hivi mbona Watanzania tunasahau mapema sana, hivi Prof. Assad alishindwa kukagua, halafu aliondokaje?* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Spika, kwa nchi za Kiafrika, *political will* ni jambo la msingi sana kufanya ukaguzi kwa uwazi, kwani jambo hili ni la kawaida?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ngoja, umeanza maneno *political will* yaliyoendelea hapo mbele, hebu yafute, halafu…

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ili nisipoteze muda nayaondoa. Nasema nilichotaka kukwambia ni kwamba, Rais ameonesha *political will* na akaongeza fedha wala sio kwa hisani, ameongeza fedha kama ambavyo katiba inasema lakini kilichotangulia ni *political will* yake, kwa sababu hajabadili katiba ili kuongeza hizo fedha. Ameonesha tu *political will* na jinsi utayari wake wa kutaka majizi kuonekana ndio hicho ninachokisisitiza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, dakika moja malizia.

**WAZIRI WA FEDHA**: Mheshimiwa Spika, jambo la pili, kwenye upande wa Mkaguzi wa ndani; Mkaguzi wa Ndani amepewa *vote* yake na Bunge lilipitisha hapa, ameitengenezea muundo

mpya ambao Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanasema hapa, kwa hiyo na yenyewe ni kwa ajili ya kudhibiti fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo mimi naomba tusitawanyike twendeni tumuunge mkono Mheshimiwa Rais, ameshaonesha nia ya kushughulikia vitu hivi tena kwa njia ya kikatiba na Waheshimiwa Wabunge, nilimsikiliza ndugu yangu Mheshimiwa Mpina…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kengele ya pili imeshagonga.

**WAZIRI WA FEDHA:** ... sisi wote tunapo kuja hapa ni Wabunge, tena mimi ni Mbunge wa jimbo anayekubalika Jimboni kwake...

**SPIKA:** Mheshimiwa ahsante sana.

**WAZIRI WA FEDHA:** ...kwa hiyo unapoongelea jambo…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba…

**WAZIRI WA FEDHA:** ...kitu ambacho hujathibitisha na hakipo kwenye taarifa ni vyema tukaheshimiana…

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba…

**WAZIRI WA FEDHA:** ...maana mimi ninapotangazwa Jimbo zima huwa linashangilia, sio kama wewe tunajua unavyoshinda… *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwigulu Nchemba…

**WAZIRI WA FEDHA:** …lazima tu…

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, Mheshimiwa Waziri ameshamaliza mchango wake.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, mwongozo.

**SPIKA:** Hapana, amemaliza mchango wake.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, haiuhusu Waziri, Waziri ameshamaliza.

**SPIKA:** Mheshimiwa… unasema?

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, haimhusu Waziri aliyekuwa anaongea ila ni mwongozo tu wa Spika.

**SPIKA:** Sawa, umeomba mwongozo, nilifikiri taarifa, karibu.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Mwongozo kwa Kanuni ya 76. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, haya ahsanteni sana, tumsikilize Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante, Kanuni ya 76, nilikuwa nataka kuona, yaani, Waheshimiwa Wabunge, tulipokuwa tunachangia toka tulipoanza, tulienda sawa lakini ilivyofika kwenye Serikali ni kama yote tuliyoyasema tulikuwa tunaisema Serikali vibaya.

Mheshimiwa Spika, nataka kujua, hivi hii michango si ni ya Wabunge na hii Kamati ya *PAC* ni ya Wabunge na michango hii ni ya Wabunge wote na sisi tumesema Waheshimiwa Mawaziri ni Wabunge? Hivi leo wanapotaka kutuona tofauti, hivi siku wakija kwenye bajeti zao wanatuonaje? Wanataka tuungane nao, tuungane na Wabunge ili kuwashambulia wao au tufanyeje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana naona kama vile, sisi tunawasema vibaya, mimi naomba utoe mwongozo, ni kwa nini tusiwe sawa, kwa nini inaonekana mambo tuliyokuwa tunazungumza ni mabaya ilhali wote tunaenda pamoja? Nani anasema kwamba Serikali imefanya vibaya kwa Rais? Maana wote tunafahamu kuwa hakuna mtu maarufu nchi hii kama Rais Samia. Waheshimiwa Wabunge wote hapa zikiletwa kura zinapigwa zote. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, ahsante sana.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Kwa nini inaonekana kwamba tukiwa tunasema ni kama vile anaguswa Mheshimiwa Rais yaani anagusa Serikali, kwa nini na huku sisi wote tuko pamoja? kwa nini tukiwa tunaongea hapa tusiende kama tunavyokwenda kwa mambo mengine? Mawaziri wengine wamechangia vizuri, kwa nini tunaanza kutuhumiana tuhuma, wakati sisi wote lengo letu ni moja? Tunataka kukamata wezi, tunataka kufukuza wezi, kwa nini tuendelee kuonekana sisi wabaya...? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Getere, umeshaeleweka. Waheshimiwa Wabunge, nilieleza kwamba Waheshimiwa Mawaziri ni sehemu ya Serikali lakini pia ni Wabunge. Kwenye hoja hii na wao wanatumia muda wao kuchangia waonavyo inafaa, waonavyo inafaa.

Waheshimiwa Wabunge, kama kuna hoja haijafafanuliwa na wenyeviti wanataka kuendelea nayo ndiyo tuko hapa tutafanya maamuzi, kwa hiyo tuwaache na wao watumie, mbona na sisi tulikuwa tunamtaja Mheshimiwa Rais wakati tunachangia. Kwa hiyo na wao wakimtaja Rais wanamtaja kwa kona waliyo ichagua. Kwa hiyo isionekane kwamba wanajitenga, hapana, sisi wote ni Wabunge na hata wao kwenye majimbo yao wanatamani haya mambo yanayojadiliwa hapa yaondoke kwenye halmashauri zao.

Kwa hiyo tulitazame kwa sura hiyo, yaani kwamba anapotajwa Rais sio kwamba anatajwa kwa sura ambayo wengine wote humu ndani wanampinga, hapana. Wengine wote humu ndani tunaungana lakini namna ya kumzungumzia,

mwingine anamzungumzia kona hii na mwingine kona nyingine, kwa hiyo tuelewane kwa sura hiyo.

Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchengerwa, watoa hoja wajiandae. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa, lakini tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kuwa na *a health discussion* inayoendelea ndani ya Bunge lako tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niseme tu kwamba, mimi ni Mbunge wa awamu ya pili, katika Ripoti za CAG ambazo nimewahi kuona zikijadiliwa *openly, transparently* na *healthy,* hii ni moja wapo ya ripoti ambayo nimeiona katika kipindi changu cha pili cha Ubunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, nataka tu nimhakikishie Mheshimiwa Bonny Kwamba, Mawaziri hatuko katika sehemu ya kulinda ubadhirifu wala hatuungi mkono uhalifu wowote unaofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la jumla, *CAG* ni jicho na ni jicho la Bunge lako kwa maana ya *oversight function.* Vile vile, ni jicho kwa sisi tuliopewa *responsibility* ya kuweza kusimamia na kuhakikisha tunachukua hatua za kulinda rasilimali za nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pale *CAG* anapokabidhi ripoti kwa Rais na inapokuja Bungeni na tunapotakiwa kwenda mbele ya Kamati, Serikali tunachukua hatua. Kwa mfano, *CAG* katika ripoti hii ya mwaka 2021/2022, amezungumzia suala la Mfuko wa Pembejeo kwamba, kuna *non-performing loans* za zaidi ya shilingi bilioni 121 ambazo hazijakusanywa.

Mheshimiwa Spika, vile vile, *CAG* ametoa *recommendation* na Kamati yako ya *PIC* imetoa *recommendation*. Moja ya *recommendation* iliyotoa ni kwamba baadhi ya madeni tuyafute.

Hata hivyo, sisi kama Serikali tunachukua hatua gani ili kuweza kusimamia rasilimali za umma?

(i) Kama Serikali tumefanya mabadiliko ya taasisi yetu ya Mfuko wa Pembejeo. Tumewaondoa viongozi waliokuwa wanasimamia taasisi zile na tumechukua *professionals* ambao wengine ni *credible*. Sasa hivi *DG* wa Mfuko wa Pembejeo ni *Formal Chief Executive Officer* wa *ECO BANK*. Tumemwomba Rais, tumemtoa *private sector* na tumemleta tumkabidhi ule Mfuko ili aweze kuu-*transform*. Mfuko ule ni muhimu kwa uchumi wetu na sekta yetu. *(Makofi)*

(ii) Mfuko wa pembejeo, wote, viongozi na wasiokuwa viongozi wali-*take advantage* na *CAG* amesema na ametoa maelekezo. Sisi katika hatua ya kufuta madeni, hatuendi kufuta madeni kwanza, tunataka ku-*recover* fedha. Toka mwezi Machi alipo-*submit report,* tumeshakusanya zaidi ya 1.4 *billion*. Pia, baadhi ya Wabunge, watumishi wa umma pamoja na viongozi wastaafu wanaodaiwa tumeshawaletea *notice*. Sasa tunakwenda kuwasajili kwenye *credit reference bureau* ili wakose uhalali wa kukopeshwa kwenye sekta yoyote ile ya nje katika uchumi mpaka waje walipe hela za umma walizokopa katika Mfuko wa Pembejeo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, wapo Wabunge wanaodaiwa?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, *yes* wapo. Vile vile, wapo hapa kwenye orodha ninayo. Pia ukiniruhusu naweza nikawataja. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Hapana, nimetaka tu hilo Wabunge wafahamu. Maana watu tunaposema *CAG* amekwenda huko kukagua akakuta madeni makubwa halafu na sisi tunadaiwa humo, tuwe wa mfano, maana sasa tusije tukawa tunawazungumzia wengine huko na sisi wenyewe hatufanyi. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, muda wako unalindwa. Endelea na mchango wako, nilitaka tu kujua hilo.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, tunakuletea rasmi *(formally)* ili wakati wa *gratuity* tuweze ku-*recover* zile hela. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo Kamati ya *PAC* na bahati nzuri Makamu Mwenyekiti wa Kamati ni aliyekuwa *Boss* wangu, ametupatia ushauri kwenye Kampuni ya *TFC*…

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Taarifa inatoka wapi? *Okay*, Mheshimiwa Bashe, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Hamis Taletale.

**TAARIFA**

**MHE. HAMISI S. TALETALE:** Mheshimiwa Spika, naomba Kaka yangu Bashe, hiyo *list* uliyoishika ungeitaja kidogo, tungejua umuhimu wa *CAG*.

**SPIKA:** Hebu hiyo orodha niletewe hapa mbele. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nataka niletewe hiyo taarifa kwa sababu na ninyi humu ndani mkichangia kuna watu mnawataja. Kwa hiyo, ngoja niletewe hiyo taarifa nione ukubwa wa hilo tatizo. Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri endelea na mchango wako.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, Taarifa ninayokukabidhi ni baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliokopa wao binafsi. Vile vile, baadhi ya Wabunge waliowadhamini wananchi wao kama *guarantor*. Pia vilevile baadhi ya viongozi wastaafu. Kwa hiyo hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo linalokabili Mfuko wa Pembejeo katika nchi yetu kwenye hili suala la kukopesha, linaikabili vile vile *Tanzania Investment Bank* na linaikabili Benki yetu ya Kilimo.

Tumeomba katika eneo la Benki ya Kilimo nao tukuletee *list* ili uweze kutusaidia na *TIB* iweze kutusaidia kupitia ofisi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ambalo nataka nichangie ni eneo la maoni ya Kamati kuhusu *TFC*. Nataka niwahakikishie Kamati, tumechukua *recommendation* za CAG kuhakikisha kwamba, Kampuni yetu ya Mbolea inanunua moja kwa moja kutoka kwenye *source* na inafanya *trading*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na hoja kwamba Serikali isifanye biashara, nataka niwaombe Waheshimiwa Wabunge, duniani kote Serikali inafanya biashara. Tunachotakiwa kujiuliza ni kwamba, taasisi za Serikali zinazofanya biashara, zinafanya biashara *efficiently and effectively?* Kama hazifanyi ni kwa nini hazifanyi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mfano *TFC,* tuliiua wenyewe *TFC*, tukaua viwanda vya kuchakata mbolea, tukavibinafsisha kwa bei holela, lakini leo tumeona umuhimu na sasa Serikali imeipatia *TFC* zaidi ya bilioni 110. Leo tunavyoongea, *TFC* inapakua zaidi ya tani 50,000 katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuingiza katika soko la mbolea ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumefanya mabadiliko kutokana na *recommendation* za Mkaguzi *(CAG)* kwamba, tufanye mabadiliko ya menejimenti. Tumefanya mabadiliko ya menejimenti, imeundwa Bodi, tumeweka *CEO* mpya, tumeweka *Commercial Director* mpya, tumepeleka *Director of Finance* mpya mwenye uwezo. Mabadiliko ya Sheria ya *Procurement Act* ambayo yamekuwa yakiifunga miguu *TFC* ku-*compete* sokoni, tumechukua hatua hizo ili *TFC* iwe *competitive* na hivi sasa tume… *(Makofi)*

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa Bashe, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kandege.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Taarifa ambayo nataka nimpe Mheshimiwa Waziri, pamoja na mchango wake mzuri juu ya sisi kuua taasisi za Serikali. Kwa mfano *TFC* ni kwamba, waliagiza mbolea lakini yakaja maelekezo wauze *below price*. Kwa hiyo, kwa vyovyote vile hasara ilianza kupatikana tangu siku ya kwanza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bashe, unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naipokea na nakiri kwamba, *TFC* na mashirika mengi ya nchi yetu yaliuawa *because of political intervention* na maamuzi ambayo ni ya kisera na *policy* ambazo hazikuwa *home-grown policies,* kwamba, *government should not trade*. Hii ndiyo ilipelekea kuua na kwa kuwa tumejifunza, naamini hatutokwenda tena siku nyingine kuichokonoa *TFC* katika nchi yetu. Sasa, *TFC* tumeipatia fedha inajenga *blending facility* Kwala. Tumeinunulia eneo na inajenga *blending facility* ili kuwa *competitive.*

Mheshimiwa Spika, la tatu, ambalo nilitaka nimalizie, mawili tu ya mwisho ili nimalizie…

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maganga.

**TAARIFA**

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Spika, mchangiaji, Mheshimiwa Waziri anachangia vizuri sana na namheshimu. Hata hivyo, kwenye taarifa iliyoko hapa mezani, tunajadili ripoti ya *CAG*. Kuna watu wametajwa majina na wewe umesema kuna majina ya Wabunge pamoja na Mawaziri ambao ni wahusika. Sasa, naomba Waziri afunguke kabisa aache kufumba macho tusije tukaua Chama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, dakika moja malizia mchango wako.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie. Pia, kama dakika moja haitatosha nitakuomba unipe hata mbili. Nataka nimalize mambo mawili ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, jana kwenye *contribution* ya Waheshimiwa Wabunge, kuna jambo lilisemwa hapa. kwamba, Ripoti ya *Financial Intelligence Unit* imeonesha upotevu wa *over two hundred trillion shillings.* Nimeamua kwenda kuichukua ile ripoti na kuisoma, kuangalia, nilishtuka sana.

Mheshimiwa Spika, mchangiaji alisema, nanukuu: "fedha hizi zinahamishwa kupita mipakani." *Technically* ukijiuliza kwa kufumba macho, unaamini kuwa kuna malori yanakatiza pale *border* na hela.

Mheshimiwa Spika, nimekwenda kuchukua ile taarifa. Sisi ni Wabunge tuna *communicate* na wananchi nje, ni hivi, *Financial Intelligence Unit Report* ambayo *summary* yake hii hapa, imesema hivi: "Taarifa za miamala ya fedha taslimu *(cash transactions)* ni 7,313, *value* ya hizo *cash transactions* siyo *value* ya hela tu, *transactions* thamani yake ukijumlisha ni *56 trillion shillings.*"

Mheshimiwa Spika, nini maana yake? *Any financial analyst* anatakiwa afanye *analysis.* Nini maana yake? Maana yake ni hivi, *our economy is dominated with cash transaction*. Nimeuza mahindi *NFRA* nalipwa cash, nabeba nakwenda foleni benki na-*deposit*. *Financial Intelligence Unit* wana-*capture* zile *data*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *Financial Intelligence Unit* wamesema, taarifa za miamala ya fedha kwa njia za kielektroniki 8,784, thamani yake ni trilioni 200. Maana yake, huko mtaani tunapeana *cash*, tunalipana kwa *M-pesa*, tunarushiana. Leo kwa taarifa za Benki Kuu, *ratio* ya *formal* na *informal* ni 60:40. Tafsiri yake bado kuna *cash* nyingi huko mikononi mwa wananchi ambazo haziko katika mfumo rasmi. Kwa hiyo, tunapoziona *cash* zinatoka kwenye

*informal* kuingia kwenye mfumo wa kibenki ni hatua nzuri kwa uchumi wowote unaokua. *(Makofi)*

**MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza taarifa zimekwishafika tatu. Pili, huu muda anaotumia Mheshimiwa Waziri ni wa kumalizia sentensi ili nimwambie muda umekwenda, kwa sababu sasa hivi ni saa nane Waheshimiwa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, anapotosha, anachokizungumza anapotosha siyo *purpose* ya *FIU*.

**SPIKA:** Omba utaratibu, kama anapotosha omba utaratibu.

Mheshimiwa Bashe.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, la mwisho, kwenye hii hoja, ninachotaka niseme kwenye hii hoja ni hivi, tusichukue taarifa kwenye *document* na kufanya *literal translation* halafu na kuzipeleka mtaani, zina-*confuse public*.

Mheshimiwa Spika, la pili, leo hapa na wewe naomba nikunukuu, umehoji kitu ambacho tunatakiwa tukijadili *as a country*. *Our governance system,* umehoji hivi, baada ya Mheshimiwa Jerry Silaa kutoa taarifa kuhusu nafasi ya Mbunge katika halmashauri kwamba, Mbunge ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha. Wewe ukasema, kama Mbunge ni sehemu ya Kamati ya Fedha katika Halmashauri inayotuhumiwa, huwezi kujadili kesi inayokuhusu.

Mheshimiwa Spika, nini maana yake? Maana yake umefika wakati wa kufanya *critical analysis* ya *role* ya Mbunge kwenye halmashauri na namna gani anamsimamia *Accounting Officer*. Waziri anapokwenda kwenye *PAC*, ambapo *PAC* inamwita Katibu Mkuu, Waziri hayupo. Nafika hapa ndani ya Bunge nahojiwa kwa kile ambacho wali-*differ* kati ya *PAC* na Waziri kwenye kikao ambacho mimi sijashiriki kama Waziri. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya, sawa.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, namalizia…

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hoja yako imeeleweka. Umekwishatoa pendekezo kwamba umefika muda wa kufanya hilo jambo, hatuwezi kuchukua muda zaidi ya hapo. Ahsante sana.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mpina, Mwongozo.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako. Waziri alipokuwa akizungumzia hapa miamala shuku ya Trilioni 280, akasema kwamba, hiyo miamala shuku ya trilioni 280 ni miamala tu ya *transaction* za kawaida za wafanyabiashara hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya miamala ya trilioni 280 tena miamala shuku. Taasisi yetu ya udhibiti na utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi, haifanyii kazi ya *transactions* za wafanyabiashara wa kawaida. Unafanyia kazi miamala wanayoishuku kwamba ina mashaka na wanaanza kuifanyia uchunguzi. Kwa hiyo, kitendo cha Waziri…

**SPIKA:** Sawa, ngoja. Ili mimi nijue aina ya mwongozo nitakaoutoa, ni sehemu ya taarifa ya CAG ama ni wewe ulikuwa unatumia mifano yako na ndiyo ile ambayo umejibiwa? Ni sehemu ya taarifa ya CAG ili nijue namna ya kujielekeza?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wako ambao nimeuomba, ni baada ya maelezo ya Waziri wa Kilimo kusema kwamba zimezungumzwa habari hapa…

**SPIKA:** Ni sawa. Sasa, mimi pia sitaki kujiingiza katika jambo ambalo kwanza sina taarifa nalo, lakini naweza kutoa Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni zetu. Ndiyo maana nakuuliza, ulipokuwa unachangia hoja hii ni sehemu ya *CAG* au hapana? Yaani hiyo taarifa ya *Financial Intelligence Unit* ni sehemu ya taarifa ya *CAG*?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, siyo sehemu ya taarifa ya *CAG*. Isipokuwa…

**SPIKA:** Sawa. Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa sababu uliruhusiwa kuchangia kwa namna ile kwa sababu ni muda wako wewe, hivyo ukaamua kutumia hiyo kama mfano. Hata hivyo sasa, Mheshimiwa Bashe anatoa ufafanuzi kwa sababu hilo jambo lilisemwa hapa ndani.

Nisingependa muda huu ambao tunataka kufanya maamuzi kwenye hoja ya CAG, tujielekeze kwenye mambo mengine. Sasa, Mwongozo wangu kuhusu hilo lililotolewa. Maadamu wewe ulichangia na Mheshimiwa Waziri naye alitumia muda wake kusema, kama kuna upotoshaji wowote, wewe tumia Kanuni zinazohusika ambazo zinahusu utaratibu ili nilisemee jambo hilo. Hili Mwongozo, Mwongozo wangu ni kwamba, Mheshimiwa Waziri ametumia haki yake ya kutoa ufafanuzi ama kutoa maelezo kwa kadri yeye alivyoona inafaa kwa sababu hili liko nje ya taarifa za *CAG*.

Waheshimiwa Wabunge, yale ambayo niliyakubali huko mwanzo ni kwa sababu ndiyo walikuwa wanachangia wale, kwa hiyo niliyapata kwa sura hiyo. Kama hili la Mheshimiwa Kasalali na hili la Mheshimiwa Ole-Shangai. Kwa hiyo, hayo mengine yanahitaji kidogo utaalamu na mimi kama Spika wenu sina utaalam na mambo ya *Financial Intelligence Unit.* Kwa kuwa sina, lazima niwe na jambo linaloniongoza ili niweze kutoa maamuzi vizuri. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nilikuwa nimekwishamtaja Mheshimiwa Mohamed Mchengerwa, watoa hoja nilisema wajiandae lakini tutaanza na Mheshimiwa Japhet Hasunga, atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia kukutana hapa siku ya leo katika kujadili hoja hizi zote mbili. Pili, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, kwa kuniamni na kuniteua katika nafasi hii kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatu, nichukue nafasi hii kukupongeza sana kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Mabunge ya Ulimwengu. Hongera sana. Pia, kwa kuwa niliwahi kuwa Mjumbe wa Mabunge haya natambua ugumu wa kupata nafasi hiyo. Kwa hiyo, nikupongeze sana pamoja na timu uliyokuwa nayo huko kwenye kampeni za ushindi.

Mheshimiwa Spika, lazima nikiri Wabunge wamefanya kazi kubwa katika misingi ya Katiba Ibara ya 61, 62 kuhusu kuisimamia Serikali. Kwa kila Kiongozi wa kuchaguliwa na kwa viongozi sisi wa kuteuliwa, Wabunge wanatutaka tufanye kazi zaidi ya kumsaidia Mheshimiwa Rais na Waheshimiwa Mawaziri kila mmoja wetu katika eneo lake ameweza kutoa majibu ya hatua ambazo tumechukua. Naomba niwathibitishie Waheshimiwa Wabunge kama Waziri ninayehusika na masuala ya Utawala, Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan iko imara sana leo kuliko jana.

Mheshimiwa Spika, hata leo tukisema tunakwenda kwenye chaguzi zetu hizo za kesho tutashinda kwa kishindo kwelikweli. Katika maeneo mengi ambako tumepita kazi kubwa imefanyika, lakini lazima nikiri Kamati ya Kudumu ya Bunge ya *LAAC* imefanya kazi kubwa na kazi nzuri sana, Mheshimiwa *CAG* amefanya kazi kubwa na kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa na ushirikiano ya karibu sana Wizara ya TAMISEMI na lazima nikiri kwamba mtu wa kwanza kuzungumza nae baada ya uteuzi wangu tukiachana na hawa wengine ni Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC,* lazima tukiri taarifa hizi zinatusaidia kuboresha utendaji kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili tuweze kufanya vizuri lugha ya kila mmoja wetu kwenda kuwajibika hakuna lugha nyingine kwenda kufanya kazi tu. Hakuna lugha nyingine na umewasikia kila Mheshimiwa Waziri akisimama hapa anazungumza ni namna gani tumewajibika tumeenda kufanya kazi katika maeneo yetu. Hakuna lugha nyepesi wasaidizi wetu na mimi nimekwisha waambia hata wasaidizi wangu Naibu Mawaziri, huu ni wakati wa kazi kama tunataka kupata ushindi wa kishindo miezi kumi ijayo katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ni lazima tufanye kazi hasa kwa kuzisoma taarifa hizi vizuri na kwenda kuzitendea haki kama ambavyo tumeshauriwa na Mwenyekiti wa Kamati pamoja na taarifa ya Mheshimiwa *CAG*. *(Makofi*)

Mheshimiwa Spika, TAMISEMI hatuna muhali, hatuna muhali hata kidogo, tunachukua hatua kama ambavyo Waheshimiwa Mawaziri wengine wamekuwa wakifanya na sisi tunachukua hatua.

Mheshimiwa Spika, yamezungumzwa hapa, taarifa ya utendaji usioridhisha kwenye baadhi ya Halmashauri tunachukua hatua, tunachukua kwelikweli na leo nitaendelea kuchukua hatua. Naomba nikuthibitishie utekelezaji wa taarifa hizi tumeendelea kutekeleza kwa kiwango cha hali ya juu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua, hata wakati fulani nilipokuwa nikiwaona Waheshimiwa Wabunge fulani wakizungumza hapa pengine wamesahau kwamba nimechukua hatua juzi tu katika maeneo yao. Mheshimiwa Kuchauka alizungumza, Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma kule Ndugu yangu amezungumza lakini Mheshimiwa Kuchauka anafahamu hatua nilizochukua juzi tu hapa takribani kama mwezi mmoja tu uliopita

tumewasimamisha kazi Watumishi ambao wameshiriki kwenye ubadhirifu wa fedha, lakini siyo kuwasimamisha tu…

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kuchauka.

**TAARIFA**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nilichozungumza hapa nataka nimpe taarifa mzungumzaji anazungumza vizuri sana, mimi kwenye mchango wangu nilisema tatizo liko TAMISEMI, katika hao Saba aliowapunguza yeye juzi alipokuja, mimi nilishapeleka taarifa zao miaka miwili iliyopita, TAMISEMI wanalindana.

**SPIKA:** Sasa hiyo taarifa, Waheshimiwa Wabunge ukisema TAMISEMI wanalindana, Mheshimiwa Mchengerwa yumo ama hayumo, maana yeye anakuambia hapa kwamba kachukua hatua na wewe unakubali kwamba kachukua hatua lakini unachojaribu kusema ni kwamba hatua zimechelewa, sasa ukitumia, sema walikuwa labda, sema walikuwa wanalindana ili ndiyo tujue hizi hatua.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, walikuwa wanalindana na ndiyo maana nikasema nimetoa taarifa miaka miwili iliyopita.

**SPIKA:** Ahsante sana, sasa kusema wanalindana maana yake ni sasa wakati hatua zimechukuliwa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, nilishawaripoti kwamba Fulani na Fulani wanatuharibia Halmashauri, hakuna kitu kilichoendelea mpaka alipokuja yeye, kwa hiyo tunaiambia Serikali kwa ujumla kwamba wanalindana.

**SPIKA:** Sawa, Mheshimiwa Kuchauka ukitumia lugha hiyo tena tutarudi kwenye Kanuni zetu hapa, ukisema walikuwa

maana yake unakiri anachosema Waziri kwamba kachukua hatua, ukisema wanalindana maana yake ni sasa na hawajafanya chochote, wewe unataka kipi kati ya hicho?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, huko nyuma walikuwa wanalindana.

**SPIKA:** Haya ahsante sana. Mheshimiwa Waziri unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, wakati tunachukua hatua kule Liwale nilichukua hatua mbele yake yeye akiwa pale pale, si kwa sababu mimi na yeye tulikuwa tumezungumza, yeye ni shahidi lakini kwa sababu ya vyanzo tulivyo navyo ndani ya Ofisi ya Rais, nilichukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua kwa Wakurugenzi wa Halmashauri kwa kuwasimamisha kazi na kutengua uteuzi wao na wengine kufikishwa Mahakamani, tumechukua hatua kwa waliokuwa Wakurugenzi wa Halmashauri ya Majiji, Jiji la Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam, Arusha na wengine wako ndani.

Mheshimiwa Spika, tumechukua hatua katika Manispaa za Singida, Iringa, Mtwara na Sumbawanga na hata aliyekuwa Mkurugenzi wa Sumbawanga akahamishiwa kwingine tumemrejesha ili akajibu kesi iliyopo Mahakamani. Kwa hiyo, zile taarifa kwamba kuna watu wanahamishwa wanapelekwa sehemu zingine katika kipindi hiki chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mtumishi yeyote popote alipo, awe amehamishwa, awe amestaafu, atakayeshiriki kwenye ubadhirifu wa fedha za umma hatutasita kumchukulia hatua, popote alipo na huo ndio ujumbe ambao tumeutuma katika maeneo ambapo tumekwisha kuchukua hatua.

Mheshimiwa Spika, pia tumechukua hatua katika Halmashauri mbalimbali kule Monduli, Muheza, Korogwe, Masasi, Kilosa, Uvinza, Buhigwe, Busega, Sengerema, Buchosa na Mvomero. Hivi tunapozungumza wataalam wangu wako

uwandani wanaendelea kufanya uchunguzi kwa taarifa ambazo tumeendelea kuzipokea kutoka TAMISEMI, kutoka kwa watoa taarifa mbalimbali, naomba nitoe taarifa kwamba TAMISEMI inaendelea na uchunguzi katika Halmashauri za Wilaya ya Kibaha ambayo imezungumzwa kwenye taarifa ya *LAAC,* tunaendelea na uchunguzi kule Kigoma, tunaendelea na uchunguzi Uvinza, tunaendelea na uchunguzi Ileje pamoja na Ifakara.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Mchengerwa kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, Wasomi wanasema "mnyonge mnyongeni haki yake mpeni". Ni kweli kwamba Mheshimiwa Mchengerwa hufuata nyayo za Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu wa sasa Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa katika kushughulikia mafisadi, natamani kama watu wote wangeungana na Mawaziri wako wengi tu waliochukua hatua, kwa kwenda kwa kasi hii ya muda mfupi uliokaa TAMISEMI tuna matumaini makubwa sana na ninahakika Waziri Mkuu amempata Msaidizi katika eneo hilo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchengerwa unaipokea taarifa hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nimepokea taarifa ya ndugu yangu na rafiki yangu. Tunaendelea kuchukua hatua hata kwa Wakuu wa Idara, naomba nitoe taarifa kwamba Wakuu wa Idara ya Vitengo vya Ununuzi na Ugavi 23 tumekwisha waondoa, Waweka Hazina 16 tumekwisha waondoa, Wakuu wa Idara ya Utawala na Rasilimali Watu Sita na Wakaguzi wa Ndani Wawili waliondolewa nafasi zao.

Mheshimiwa Spika, Waganga Wakuu 10 wa Mikoa wameondolewa nafasi zao, Waganga wa Wilaya 46 wameondolewa nafasi zao na mwingine tumemuondoa hivi karibuni kule Mbogwe, tumemuondoa hivi karibuni. Kwa hiyo

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan inachukua hatua madhubuti.

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa kuhusu….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika moja Mheshimiwa malizia.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nikiri Serikali ya Awamu ya Sita inafanya kazi kubwa sana, sana, sana na ni lazima panapotokea mafanikio makubwa ni lazima *credit* tumpe Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa na kazi nzuri anayoifanya kwenye maeneo yetu. Hatutaki tumpe taabu Mheshimiwa Rais 2024/2025, na ili tuweze kufanikiwa tusimpe taabu ni lazima tufanye kazi kwa bidii hakuna lugha nyingine! Hakuna lugha nyingine.

Mheshimiwa Spika, wale wote ambao wametajwa kwenye ripoti naomba niseme maneo yafuatayo; ole wake kiongozi yeyote mzembe na mbadhirifu, ole wake! Kiongozi yeyote mzembe kwenye Wizara yangu na asiye na nidhamu nitakaye mkuta huko na wabadhirifu, nataka niwaambie siku zao zinahesabika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia…

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri malizia mchango wako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kumuelekeza Katibu Mkuu TAMISEMI kuchukua hatua dhidi ya Mkurugenzi wa Igunga, aliyekuwa Mkurugenzi kule Kigoma Ndugu Athumani Francis Msabila, kumsimamisha kazi mara moja kwa sababu ya ushiriki wake wa fedha za mifumo akishirikiana na watendaji wa mifumo walioko TAMISEMI wawili walitajwa katika

taarifa ya ripoti. Katibu Mkuu awasimaishe kazi mara moja na taarifa hizi za ripoti ya *LAAC* pamoja na hii ya *CAG ni wakeup call* kwa kila mmoja wetu kuwajibika kwenye eneo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tutahakikisha tunawatendea haki Watanzania, Serikali inafanya kazi kubwa sana ni lazima tumtendee haki Mheshimiwa Rais, kwa sisi viongozi kufanya kazi kwa bidi, hakuna lugha nyingine ni lazima tufanya kazi kwa bidi kila mmoja wetu katika eneo lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja ya Kamati ya *LAAC* pamoja na Kamati ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na ninakuomba uridhie majibu ya kila Mbunge kwa namna yalivyotolewa TAMISEMI tumekwishaandaa majibu ya kila hoja kwa namna ilivyotolewa na tutaiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu ili tuweze kuwakabidhi Waheshimiwa Wabunge kila mmoja aweze kuipata na kuisoma, na wasisite wakati wowote pale popote kunapotokea changamoto TAMISEMI tutakuwa nanyi leo na kesho kuhakikisha kwamba tunafanya kazi kwa ajili ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya ahsanteni sana.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**SPIKA:** Hoja ya dharura? Haya, Mheshimiwa Husna Sekiboko.

## HOJA YA DHARURA

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 79 kama utaniruhusu nisiinukuu kwa ajili ya kuokoa muda.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo linazunguka kwenye mitandao ya kijamii na hata humu ndani linajadiliwa kuhusiana na

hatua zilizochukuliwa na Serikali juu ya Walimu, Wakuu wa Shule wa Shule za Tunduma, ambapo inaelezwa katika kipindi cha Tarehe Sita Oktoba kuna taasisi ilipeleka misaada kwenye shule hizo lakini taasisi hizo ziliambatana na shamrashamra za miziki, kwa hivyo, miziki iliyokuwa imepigwa kwenye shule hizo ilionekana na ilitafsiriwa kwamba ni miziki ambayo haina maadili na kwa hivyo Serikali kwa maana ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Wizara ya Elimu walichukua hatua.

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa kuomba kama itawezekana jambo hili lijadiliwe ili Serikali itoe mstari ni namna gani mambo kama haya yakitokea yatashughulikiwa hasa kwa lengo la kulinda haki na kulinda maadili ya watoto wawapo shuleni. Kwa sababu sisi wote ni mashahidi, mambo haya yameendelea kutokea katika shule zetu za Sekondari na shule za Msingi, watoto wamewekewa miziki ambayo kiukweli haina maadili, mingine inahamasisha pombe, wanasema pombe tamu, wengine wamehamasisha wanasema mimi sijui kutongoza lakini namwaga pesa na vitu vya namna hiyo ambavyo pengine vinaweza vikamong'onyoa maadili ya Mtanzania hasa kwa shule za watoto kama shule za msingi.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae, tukae Waheshimiwa Wabunge. Hoja ya Mheshimiwa Mheshimiwa Husna Sekiboko imeeleweka, nitaitolea maelezo baadae kidogo.

Nilikuwa nimeshasema kwamba tunaanza na wenye hoja sasa Wenyeviti wa Kamati, tutaanza na Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Halima James Mdee tutamalizia na Mheshimiwa Deus Sangu.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):** Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuhitimisha hoja ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuhusu ripoti za *CAG* kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2022. Aidha, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchangia hoja hii kwa ukamilifu, weledi na uzalendo wa hali ya juu, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jumla ya Waheshimiwa Wabunge takribani 78 wamechangia kwa kusema na wengine kwa kuandika na naomba kwa sababu ya muda nitasema tu mambo machache lakini kabla ya kuendelea nifanya masahihisho katika lile Azimio ambalo tulikuwa tumependekeza. Katika moja ya eneo ambalo nataka kufanya marekebisho kidogo ni lile eneo linalohusu zile fedha za *IPTL* kwenye taarifa tuliyokuwa tumesoma tulisoma bilioni 148.4 badala yake siyo bilioni tulikosea tukatumia *Tshs.* Ni Dola za Marekeni milioni 148.4. Kwa hiyo, naomba katika maeneo yote ya taarifa kuu pamoja na yale niliyoyasoma yafanyiwe marekebisho ili yasomeke hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika uchangiaji, wachangiaji wamezungumza mambo mengi sana na yote kwa kweli ni mazuri na sisi kama Kamati tumeyakubali, lakini nataka nitoe ufafanuzi katika maeneo machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza Serikali kwa hatua ilizochukua katika ufungaji wa hesabu. Hapo ukizungumzia kufunga hesabu, kuzingatia Kanuni za Kimataifa za Ufungaji wa Hesabu kuzingatia Sheria na Miongozo kwenye kufunga hesabu wako vizuri sana sasa hivi. Hali ni nzuri na ndiyo maana utakuta Hati za Ukaguzi ni nzuri na zinaonesha hali nzuri. Hati za Ukaguzi Hati zenye Mashaka zimepungua kwa kiwango kikubwa, ni kazi kubwa ambayo imefanywa na Serikali tunaitambua. Sasa kupata Hati inayoridhisha haina maana kwamba huko ndani mambo yote yako safi ni bahati mbaya hatuna neno zuri la kulitumia tunatumia "Hati Safi" hakuna neno "safi", kwa kiingereza ni *unqualified opinion* ni Hati Inayoridhisha, hakuna taasisi ambayo ni

safi 100 *percent* hakuna! kwa hiyo ni Hati Inayoridhisha, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo nilitaka kuliweka vizuri kaguzi zipo za aina nyingi, hapa tunayoiwasilisha ambayo tumeifanyia kazi kwa kiwango kikubwa ni Ukaguzi wa Masuala ya Kifedha, kuna Ukaguzi wa Masuala ya Kifedha kwa mujibu wa Katiba yetu, kuna Ukaguzi wa Ufanisi ambayo ni *Performance Audit Report,* hizo hatujazifanyia kazi nyingi bado. Kuna Ukaguzi wa Kiufundi *(Technical Audit),* kuna Ukaguzi Maalum na kuna Ukaguzi wa Kiuchunguzi au tunaita *Forensic Audit*. Sasa Waheshimiwa Wabunge naomba muelewe tofauti ya Kaguzi zote hizo.

Mheshimiwa Spika, hapa tunachokichambua kwa leo ni ukaguzi wa kifedha kuangalia kama taratibu zilizingatiwa. *CAG* anapokagua kuangalia hayo, anaangalia kama kuna upungufu na anatoa taarifa mbili; ya kwanza anatoa maoni yake ambayo yapo kwenye hati ya ukaguzi. Yale ni maoni (*expression of opinion on the financial statement)*, ndiyo hiyo ya kwanza mpaka anatoa hati.

Mheshimiwa Spika, cha pili, analeta barua inayoonesha upungufu uliopo kwenye taasisi, ambao siyo sehemu ya *financial statement,* lakini yale aliyokutana nayo, hayo yanakuwa kwenye kitu tunaita *Management Letter* na hayo ndiyo yanayotusaidia kujadili. Sisi Kamati tunapokutana, yale mazuri yote tunaya-*note,* lakini siyo sehemu ya ripoti yetu. Kwa mujibu wa Kanuni zetu, zinatuelekeza tujadili na tulete humu Bungeni maeneo yenye upungufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunayoyaleta hapa ndani ni yale maeneo yenye upungufu. Kama yana upungufu, nataka niseme, kama nilivyosema, hesabu zimefungwa vizuri, zimetayarishwa kwa kiwango kikubwa tu, na tukiangalia katika uzingatiaji wa taratibu za Kimataifa, kuna maeneo mawili tu yanaonekana yana upungufu kwenye Serikali. La kwanza liko kwenye upande wa Kanuni ya Kimataifa Kanuni 17 *(IPSAS 17)* kwenye namna ya kutambua mali za kudumu na namna za

kuzifanyia *revaluation* ili zitumike kwenye kufunga hesabu. Hilo katika taasisi nyingi kuna upungufu.

Mheshimiwa Spika, pili, ni ku-*comply* na maelekezo ya Wizara ya Fedha yaliyoagiza kila taasisi inapofunga hesabu ihakikishe mali zake zote za kudumu ziko katika mfumo wa kieletroniki wa *GAMIS*. Nataka niseme, tulipoangalia hakuna taasisi hata moja iliyoweza ku-*comply* na hiyo *100 percent,* zote zina matatizo kwenye hilo eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nizungumzie kwa kifupi sana maeneo ambayo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamechangia. Kuhusu hasara ya *TANOIL,* nashukuru baadhi ya Mawaziri wamefafanua. Tulichoambiwa sisi ni kwamba, kama nchi tunahitaji tuwe na shirika ambalo kama ikitokea *emergency* lazima liweze kufanya kazi ya Serikali. Ndiyo maana Serikali iliamua kuanzisha *TANOIL*. Hilo sisi hatuna tatizo nalo. Tatizo tulionalo, ni kwa nini ipate hasara? Hasara iliyoripotiwa mwaka ule na hasara itakayoripotiwa mwaka huo ambao wamefunga hesabu ni vitu viwili tofauti, sasa hivi nafikiri imekuwa ni kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sisi hoja yetu ni kwamba kwa nini hasara ilitokea? Wanasema hawakufuata bei zilizotangazwa na *EWURA*, waliweka *discount*. *Discount* ni kitu cha kawaida, kinaruhusiwa kibiashara, lakini unapoweka *discount,* lazima uhakikishe kwamba kweli unapata faida. Sasa hawa wamepata hasara na Serikali imekiri wamepata hasara. Kwa hiyo, hapa tunachosema ni kwamba lazima sasa tuchunguze kwa undani, hatua zichukuliwe. Hilo sidhani kama lina mjadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo limezungumziwa kwa kirefu sana na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Kilimo amelizungumzia, hili suala la madeni ya Mfuko wa Pembejeo *(AGTIF)*. Bahati nzuri ameshakupa orodha, nasi tuliiomba hiyo orodha, tuliipata, na tuli-*note* kwamba kweli wapo baadhi ya Waheshimiwa hawajalipa. Kwa hiyo, tunachosema, Bunge lifanye uamuzi, kwa sababu zile fedha zikirudishwa kwenye ule mfuko, ule mfuko utakuwa hai, utaendelea kufanya kazi ile iliyokusudiwa. Kwa hiyo, hilo hatuna matatizo nalo.

Mheshimiwa Spika, kuna madeni ambayo yapo ambayo viongozi na Serikali imetoa ufafanuzi. Sisi tunakubaliana kama Kamati, madeni ya Serikali kwenye mifuko ya hifadhi za jamii, tume-*note* hatua ambazo zimechukuliwa, wamelipa; lakini sisi *concern* yetu tunaiomba Serikali iseme italipaje hayo madeni, na kwa kipindi gani? Kwamba kila mwaka itakuwa inalipa kiasi fulani, basi kuwe na *commitment* ambayo inaonekana kabisa ambayo tunaweza kuifuatilia ili ikija mwakani, tunasema Serikali ilisema itafanya hivi, haikufanya. Kwa hiyo, hilo tunadhani kwamba itatusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, suala la riba limezungumziwa sana. Kwenye Taarifa ile ya *CAG* kubwa, suala la riba ni shilingi bilioni 418. Riba zinazotokana na ucheleweshaji wa mikataba mbalimbali kutokulipa, lakini tuliyoyafanyia kazi kwenye Kamati katika kipindi hiki, kumbuka Kamati inachukua ina *sample*, hatufanyi yote *100 percent* kwa sababu ya muda. Tuliyoyafanyia kazi ni taasisi mbili tu ndio tumezifanyia kazi, moja ni *TANROADS* ambayo tumekuta riba kwa mwaka huo pekee yake wana shilingi bilioni 36 wanadaiwa lakini *TANESCO* wanadaiwa riba na kampuni ya *Pan African Energy* shilingi bilioni 113. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ukichambua zile nyingine na hizo taasisi ambazo hatukuzichambua, ndiyo maana *CAG* anasema zinafika shilingi bilioni 418. Sasa hizo fedha *concern* yetu sisi, ni fedha nyingi. Hizo kama kweli tunge-*save* badala ya kulipa riba, zingefanya kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, japo kuna suala la madawa, wameshaeleza na Mheshimiwa Waziri nashukuru kwa maelezo uliyoyasema. Maeneo mengi kama uzingatiaji wa sheria, taratibu, nimewasikia Mawaziri walivyosema, na mmesema mambo mengi, lakini ninachotaka niseme Waheshimiwa Wabunge, kwa michango namna mlivyochangia kwa muda wa siku hizi tatu mmeitendea haki Kamati yetu na mmelitendea haki Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, michango ni mizuri na inaleta uchungu. Tunapoona Mheshimiwa Rais anapambana huku na huko

kutafuta fedha ili zitekeleze miradi, halafu nyingine haziendi kutekeleza ile miradi iliyokusudiwa, inaumiza sana. Hiyo Waheshimiwa Wabunge tume-*note concern* yenu na mmechangia vizuri sana. Tunawapongeza sana kwa hilo. Vile vile mmefanya jambo la Kikatiba. Katiba yetu inatutaka tuisimamie Serikal. Kwa hiyo, mlichokifanya leo ni kuisimamia Serikali, na maazimio mtakayoyapitisha ni ya kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, naamini maazimio yatakwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa maeneo mengine yote ambayo wameyasema yanayohusu *KADCO*, na kadhalika, kila mtu ameyasikia; yanayohusu kila taasisi, tumeyasikia. Kwa hiyo, nina imani Wabunge tutafanya uamuzi, lakini nataka nitumie muda huu kuleta kwa uchache mapendekezo ya maazimio ambayo Bunge hili sasa tunatakiwa tufikie kuamua. Mapendekezo hayo, nataka niseme mwishoni nikishamaliza kuyasema haya; nimeletewa mapendekezo na Waheshimiwa Wabunge wawili katika kuongezea maazimio ambayo tunayapendekeza kwenye Bunge. Nayo nitayatolea ufafanuzi baadaye nitakapokuwa naendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima kubwa niseme mapendekezo ya Kamati kama ambavyo tunafikiria na kama ambavyo tulipendekeza. Mabadiliko ni kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nakisi ya ukusanyaji wa mapato kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kiasi cha shilingi bilioni 887.3:-

Kwa Kuwa, Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (*CAG)* imebaini nakisi ya kiasi cha shilingi bilioni 887.3 cha mapato ambayo hayakukusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kutokana na upungufu mbalimbali ikiwa ni pamoja na usimamizi usiokuwa thabiti wa mafuta yaliyosafirishwa kwenda nje ya nchi na kisha kutumika hapa nchini na kuchelewa kusajili mapingamizi ya kikodi;

Na Kwa Kuwa, kutokukusanywa kwa mapato hayo kunasababisha upotevu wa mapato ya Serikali na pia kunapunguza uwezo wa Serikali kuwa na rasilimali za kutosha katika kutimiza majukumu yake;

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) *TRA* ihakikishe ndani ya mwaka wa fedha 2023/2024 inakamilisha usimikaji na utekelezaji wa mifumo yote muhimu ya usimamizi wa udhibiti wa kodi ili kuhakikisha mapato stahiki ya Serikali yanakusanywa kwa ukamilifu;

(b) *TRA* ihakikishe kesi zote za mapingamizi ya kodi kama zilivyoletwa na walipa kodi zinashughulikiwa kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizopo ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

(c) *TRA* ihakikishe inaweka mifumo dhabiti ya usimamizi wa kodi katika michezo ya kubahatisha na mafuta ambayo yanapitia hapa nchini kwenda nchi za nje. Katika kutekeleza azimio hili, hatua kali zichukuliwe kwa wanaokiuka sheria na umma ujulishwe ipasavyo; na

(d) *TRA* itengeneze mfumo maalum wa kusimamia makusanyo ya mizigo, yaani ile mizigo ambayo wanatakiwa kui-*consolidate (consolidators)* ili kuhakikisha mapato ya Serikali yanayokusanywa kwa mujibu wa sheria yanakusanywa. Aidha, kodi yoyote ambayo ilikuwa haijakusanywa ikusanywe kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, hilo ndilo azimio letu la kwanza, azimio la pili Waheshimiwa Wabunge kama mtaniruhusu linabaki kama lilivyo lile lilokuwa linahusu hasara ya shilingi bilioni 7.8 la *TANOIL*. Kwa sababu ya muda, kama mtaridhia kama tulivyolipendekeza awali linabaki kama lilivyo.

Mheshimiwa Spika, azimio la tatu, mapato yasiyokusanywa ya dola za Marekani 599,000 katika Wizara ya Maliasili na Utalii, linabaki kama tulivyopendekeza pale awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la nne linahusu *IPTL* kutotimiza wajibu wa kimkataba na hivyo Serikali kuwa hatarini kupatiwa madai ya dola za Marekani milioni 148.4 yanayotokana na *IPTL* kutotekeleza majuku yake. Hili azimio kama nilivyosema pale awali, *figure* tulikuwa tumeandika bilioni badala ya milioni; ni dola za Marekani milioni 148.4.

Kwa Kuwa, Taarifa ya *CAG* ilifafanua kwamba Kampuni ya *IPTL* imeshindwa kutekeleza wajibu wake wa kimtaba kwa kinga ya kisheria iliyotoa dhidi ya madai ya Serikali;

Na Kwa Kuwa, kutotekelezwa kwa kinga hiyo ya kisheria kunasababisha Serikali kuendelea kudaiwa madai mbalimbali yanayotokana na *IPTL* ikiwemo madai ya Dola za Marekani milioni 148.4.

Kwa Hiyo Basi, Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali itekeleze kwa ukamalifu masharti yaliyoambatanishwa kwenye kinga ya kisheria *(indemnity)* iliyotolewa na *IPTL* dhidi ya madai yoyote ambayo yangetokea kwa Serikali baada ya kutolewa kwa fedha hizo katika akaunti ya *Tegeta ESCROW*; na

(b) Serikali isifanye malipo mengine yoyote kwa mshauri yanayofunguliwa dhidi ya mmiliki wa *IPTL* ili kutopoteza fedha za umma kwa sababu ina kinga ya kisheria kwa suala hili.

Mheshimiwa Spika, huu ndiyo msimamo ambao tunafikiri ubaki vilevile. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge hilo azimio kama mtaridhia libaki hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tano ni upungufu katika utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Mwanga - Same hadi Korogwe. Hili nalo tunaomba libaki kama lilivyo. Hapa nimemsikia Mheshimiwa Waziri amezungumzia kwamba kulikuwa na *special audit* ilikuwa imeshafanyika. Kilichofanyika ni *technical audit,*

tunayokwenda kuifanya ni *special audit* na itaambatana na *forensic audit*, kufanya uchunguzi. Kwa hiyo, hicho ndicho kinachoenda kufanyika. Tunaomba kama nilivyopendekeza pale mwanzoni, Kamati inapendekeza bado ibaki vilevile bila mabadiliko yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la sita, manunuzi ya mita za umeme bila kukaguliwa na Wakala wa Vipimo, tunaomba hili azimio nalo libaki kama lilivyo. Eneo la saba ni Tume ya Madini kutokusanya madeni ya kiasi cha shilingi bilioni 30.7, tunaomba nalo hilo libaki kama lilivyo. Bohari Kuu ya Dawa, tunaomba libaki kama lilivyo, tulivyopendekeza pale awali. Taarifa ya Ukaguzi Maalum kuhusu uendeshaji na usimamizi wa mikataba ya maridhiano, yabaki kama tulivyopendekeza pale awali. Taarifa za matumizi ya fedha ya mkopo wa *IMF,* yabaki kama yalivyo. Kutozingatia ipasavyo kwa Kanuni za Kudumu za Utumishi wakati wa mchakato wa ajira katika Benki Kuu ya Tanzania, tunaomba azimio libaki kama tulivyopendekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla niseme, mapendekezo ya maazimio tunaomba karibu yote kama tulivyoyawasilisha pale juzi yabaki kama yalivyo, isipokuwa tumepata mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge wawili. Tumepata mapendekezo kutoka kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka na Mheshimiwa Luhaga Mpina. Sasa naomba nitoe maelezo kidogo.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya Mheshimiwa Mpina bahati mbaya yametufikia wakati karibu nasimama kuja huku, sasa hatukuweza kuifanyia kazi. Kwa hiyo, mapendekezo yake yote hatujaweza kuyatafakari na kujadiliana na Wanakamati wenzangu. Kwa hiyo, hiyo kidogo inanipa ugumu kuyaleta kama mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo ya mabadiliko ya hoja ambayo yanapendekezwa na Mheshimiwa Ole-Sendeka, anapendekeza kama ifuatavyo na Waheshimiwa Wabunge kama mtaridhia naomba niwasomee. Anasema hivi, "Kwa kuwa ukaguzi uliofanya na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*…

**SPIKA:** Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti hayo mapendekezo yameshawekwa kwenye vishikwambi. Kwa hiyo, wewe endelea na hoja yako.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC):** Mheshimiwa Spika, *okay*, nashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Waheshimiwa, Mheshimiwa Ole-Sendeka amependekeza azimio la kwanza, kwamba Serikali ihakikishe inaokoa fedha zote zilizobainishwa kwenye Taarifa ya *CAG*. Sisi kama Kamati tunaona hili ni la msingi na tunafikiri kwamba ni kitu cha msingi sana kama tunaweza tukali-*adopt* tunaweza kuliongezea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili anasema, Mawaziri, Makatibu Wakuu na Watendaji wote walioguswa na Taarifa ya *CAG* na Kamati wajitafakari kabla ya Mamlaka ya Nidhamu kuchukua hatua dhidi yao, hilo tunaliachia Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, Bunge iunde Kamati Teule kwa mujibu wa Kanuni ya 139 ya Kanuni za Kudumu na mambo mengine yanayoelekezwa kama alivyopendekeza wakati anachangia, tumeiangalia lakini tumeiachia Bunge kwamba liendelee kutafakari.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Luhaga Mpina ameleta mapendekezo mengi, hatujayapitia, lakini nimeyapata. Kwa sababu hatujayajadili na wenzagu, naomba nisiyatamke, maadamu yapo kwenye vishikwambi, basi Waheshimiwa Wabunge watazingatia wakati wanatoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo na ufafanuzi huu mdogo ambao nimeufanya, kwa heshima kubwa niwaomba Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa michango yote na kazi kubwa mliyoifanya. Sasa naomba kutoa hoja ili maazimio haya yawe ni sehemu ya Bunge letu zima.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. BAKAR HAMAD BAKAR:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Mawaziri naona kuna watu wamekaa. Waheshimiwa Wabunge huwa wanaunga mkono hoja zetu. Kwa hiyo, mnaweza na ninyi mkasimama, maana naona kuna wengine wanajiuliza kama wasimame au wasisimame? Inaruhusiwa kwa sababu na wao huwa wanaunga mkono hoja zenu, lakini kama hamjaridhika nazo basi mnakaa.

Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono na kwa utaratibu wetu napaswa niwahoji. Sasa kabla sijawahoji, kwanza ni zile hoja zote za Kamati lakini kuna hoja moja ambayo Kamati pia imeitolea mapendekezo na hawajabadilisha kulingana na wao walivyoona inafaa na ni ile hoja niliyosema nitatoa maelezo baadaye, hii hoja ya *KADCO*. Kamati yetu bado inayo mapendekezo ambayo yameletwa kwetu halafu sisi tukishahojiana hapa yatakuwa ni Maazimio ya Bunge.

Sasa hii hoja ya *KADCO* kwa sababu ilikuja mwaka jana 2022, tukaijadili hapa na Serikali ikaleta taarifa na hapa tumepata nafasi ya kuijadili, lakini pia maelezo yanayotolewa na upande wa Serikali kuhusu hoja hii hayaridhishi kwa ngazi hiyo. Hayaridhishi kwa sababu maswali tunayojiuliza ni yale ambayo tulishajiuliza na bado yanakuja yakirudi hayo hayo.

Kwenye taarifa hii ya Kamati ukurasa wa 121 wananukuu maelezo kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na huu ufafanuzi ulitolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupelekwa upande wa *TAA*, wakati wakitafuta na wenyewe Serikali namna ya kutekeleza lile Azimio la Bunge, ukurasa wa 121 wa taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge sijasimama, nimekaa, lakini tusikilizane ili tuwe tunaelewana wote kwenye haya mambo. Unasema hivi: *"The Executive Agencies Act Cap 245 establishing TAA of 1999 empowers TAA to manage, operate and develop publicly owned airports. He further opined that proposed*

*legislation should not focus on establishing a new institution for managing, operating and developing airport but continuing the TAA under the legislation."*

Ukisoma maelezo ya ziada ambayo Kamati imesema na nitaishia hapo kwenye kunukuu inasema, "kwa msingi wa nukuu hapo juu, maelezo ya aliyekuwa Katibu Mkuu Uchukuzi yanapingana na ushauri wa kisheria wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika hoja hii. Ushauri wa kisheria uliotolewa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ulibainisha kwamba *TAA* ina mamlaka kisheria ya kusimamia shughuli za viwanja vya ndege nchini hivyo kurejeshwa kwa usimamizi wa shughuli za *KIA* kwa Mamlaka hiyo kunaendana na matakwa ya kisheria na hakuzuii hatua ya Serikali ya uandaaji wa Sheria ya *TAA*." *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, taarifa hii ukiendelea kuisoma ni kwa ajili ya muda wetu inaonesha namna ambavyo baadhi ya mambo ambayo yametajwa kuwa kizuizi cha hili zoezi kukamilika ni pamoja na wale waajiriwa wa *KADCO* watahamishiwa vipi Serikalini lakini Taarifa ya Kamati hapa imeeleza mazingira ambayo Serikali imeshawahi kupata huko nyuma kuunganisha taasisi mbalimbali na zoezi halikuchukua miaka. *(Makofi)*

Sasa kwa sababu Serikali hapa ndani iliomba muda ili ikalitafakari kwa pamoja tena jambo hili halafu ituletee taarifa kabla Bunge hili halijasitishwa ama halijaahirishwa. Alisimama Mwanasheria Mkuu wa Serikali akaleta ombi hilo lakini pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu anayesimamia Sera, Uratibu na Bunge ameleta ombi hilo.

Waheshimiwa Wabunge, nafikiri kwenye hoja hii nitakapokuwa ninawahoji ili mjue mnafanya maamuzi gani; maamuzi ambayo tunayo kwenye Taarifa ya Kamati kuhusu *KADCO* yanasema, "kwa kuwa mapungufu hayo yote ambayo yametajwa wanasema;

Hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba Serikali itekeleze mapendekezo yote ya *CAG* yanayohusu Ukaguzi Maalum

uliofanyika *KADCO* kwa hoja zinazohusu utendaji na fedha kama ilivyokuwa."

Waheshimiwa Wabunge, kwa hivyo maamuzi kuhusu Azimio la Bunge ni hili ambalo liko hapa ambalo nitawahoji nalo lakini yale maombi yaliyotolewa na upande wa Serikali kuhusu kutuletea taarifa ndani ya kipindi hiki tunayakubali ili wao walete taarifa halafu hiyo taarifa itatusaidia sasa Bunge siyo kwa maana ya kufanya maamuzi mapya, kuwa katika picha kwa nini jambo hili linasumbua na kwenye Taarifa hiyo sasa tutafanya maamuzi kuhusu Taarifa hiyo na siyo kama sehemu ya Taarifa ya *CAG*.

Ninaamini nimeeleweka; tutafanya maamuzi juu ya hiyo Taarifa iliyoombwa kuletwa na Serikali lakini kwa upande wa yale ambayo tulikuwa tunazungumzia Taarifa ya *CAG* nitakayowahoji ambayo yatakuwa ndiyo Maazimio ya Bunge ni yale yaliyo kwenye Kitabu cha Kamati. Tumeelewana vizuri? *(Makofi)*

Sasa ni yale yaliyo kwenye kitabu cha Kamati pamoja na pendekezo moja kutoka kwa Mheshimiwa Ole-Sendeka lililokubaliwa na Mwenyekiti wa Kamati; sasa nitawahoji. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sawa, kwa upande wa Maazimio ya *PAC* yameshapitishwa na Bunge. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* Mheshimiwa Halima James Mdee. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, au ya kwangu inakuja baadaye?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani; naambiwa Mheshimiwa Ole-Sendeka alikuwa amesimama.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba uketi kidogo kwenye kiti kilicho karibu; Mheshimiwa Ole-Sendeka.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwamba kulikuwa na hoja mbili zilizotakiwa kuamuliwa na Bunge kwa maana moja ndiyo ilikuwa imekubaliwa na Kamati. Sasa nikasema niombe mwongozo wako niendelee kwa sasa au ni baada ya Kamati zote maana hii *issue* yangu inahusu *PAC* na Taarifa ya *PAC* ndiyo hii ilikuwa inaendelea ndiyo maana nimesimama.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Sasa wacha nitoe maelezo kidogo hapo. Kama tulivyojulishwa kuna Taarifa ya mapendekezo ambayo Mheshimiwa Ole-Sendeka alileta kwa ajili ya kufanya marekebisho au kuleta mapendekezo mapya ili yaingie kama sehemu ya Maazimio ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuleta mapendekezo haya, Kamati imekubaliana na pendekezo moja na katika mapendekezo haya mojawapo ilikuwa ni ya kuunda Kamati Teule kwa ajili ya; ametaja kwa mujibu wa Kanuni ya 139 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kuchunguza upotevu wa fedha za umma kama ulivyobainishwa na *CAG* kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita na kupendekeza mfumo sahihi utakaotumika na Bunge kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka utaratibu huu tunaotumia sasa wa kujadili hizi Taarifa za *CAG* huko nyuma hatukuwa nao. Ni utaratibu ambao tunautumia sasa kwa mara ya pili; tulitumia mwaka jana na sasa tumeutumia tena na wakati nikihitimisha ule mjadala siku ya tarehe 05 Novemba, 2022 kuna maelezo ya ziada niliyatoa na katika hayo maelezo ya ziada kwa sehemu nilieleza namna ambavyo Bunge litatumia vikao vyake vile vingine kwenye ngazi ya Kamati kufuatilia utekelezaji wa Mapendekezo ya *CAG* na Maazimio ya Bunge na nikawa nimesema pamoja na yale ambayo Bunge tunakuwa tumeletewa hapa kwenye Kamati lakini kuna yale ambayo *CAG*

Taarifa yake yanakuwa hayajaingia yote humu na tunaipa Serikali maelekezo kwamba hayo nayo mkayatazame. Na wakati huo huo nikaeleza kwamba Serikali ilete mwezi Februari kwa maana ya mwaka huu Februari ilete taarifa ya utekelezaji wa yale Maazimio ya Bunge ambacho Serikali ilileta.

Tukaanza na kitu kingine kipya baada ya Serikali kuleta utekelezaji wa yale Maazimio ya Bunge na yale Mapendekezo ya *CAG* kuingiza hapa Bungeni na tulifanya hivyo mwezi wa sita; tulifanya mwezi wa sita.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, mwezi wa tisa.

**SPIKA:** Mwezi wa tisa? Sasa sita, tisa? Mimi nasema tulifanya Juni, anayesema Septemba tuliingizia wapi maana mimi si ndiyo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mpina, Septemba wakati tunajadili nini?

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, yaani taarifa ya majumuisho ililetwa Septemba kama Sheria yetu ya Ukaguzi ilivyorekebishwa. Zamani ilikuwa *immediately* tu *CAG* akiwasilisha ripoti lakini ilipofanyiwa marekebisho sasa ikawasilishwa Septemba yale majibu ya majumuisho ya Serikali.

**SPIKA:** Sawa, majibu ya Taarifa ile iliyopita, Maazimio ya Bunge niliagiza yaletwe Februari na Serikali ilileta. Baada ya Serikali kuleta yaliletwa hapa Bungeni Juni. Tofauti tu ni kwamba kwa sababu ni jambo jipya hatukuweza kuwa na ratiba ya kuweza kujadili kuona wameweza yapi, yapi bado na yapi yanaendelea lakini yaliingizwa hapa Bungeni Juni. Jambo ambalo lilikuwa linatoa fursa kwa Kamati zetu kuanza kuyafuatilia kwa sababu tayari tumeshayaweka mezani. *(Makofi)*

Sasa mabadiliko haya katika kipindi hiki tuyape muda tuone kwa namna gani Kamati zetu zinaweza kushiriki katika zoezi la kuisimamia Serikali kuhusu yale mambo ambayo *CAG* ameyaleta. Sasa tukisema katika kipindi hiki hiki tena tuunde na Kamati Teule

tutakuwa hata sisi ule mfumo wetu mpya hatujautazama vizuri unawezaje kufanya kazi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tutoe hiyo fursa kwa sababu ndiyo tumeanza huu utaratibu mpya. Wazo ni zuri lakini tujaribu kufuatilia haya ambayo tuliagizana mwaka jana yamefanya kazi kwa sehemu gani na huko mbele tutatazama kama kuna sababu ya kuwa na Kamati maana wengine wamependekeza iwepo Kamati, wacha hii Kamati Teule, iwepo tu Kamati kwa ajili ya kufuatilia hayo. Sasa ukisema iwepo tu Kamati ndiyo kazi ya Kamati ya *PAC, LAAC* na *PIC*.

Ukisema iwepo Kamati teule maana yake unataka kutazama kipindi mahususi ambacho Mheshimiwa amekitaja kwa miaka mitatu. Kwa hiyo, nilikuwa naomba huu utaratibu mpya ambao tumeuanzisha twende nao huo tuone utatufikisha wapi halafu huko mbele *Insha Allah* Mwenyezi Mungu akituweka tutatazama kama kuna umuhimu wa bado kuwa na Kamati Teule kwa ajili ya uchunguzi huo ikiwa Kamati zetu zitakuwa hazijaweza kutufikisha mahali ambapo tunataka tuisimamie Serikali vizuri. Kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo yangu Mheshimiwa Ole-Sendeka.

Sasa nilikuwa nimeshamuita Mheshimiwa Halima James Mdee aje ahitimishe hoja ya Kamati yake.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa nafasi niliyopata ya kuweza kufanya majumuisho. Lakini vilevile nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe/Wabunge mliochangia ambao mliochangia kwa kuzungumza ni zaidi ya 78 na wengine ambao mmechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, nitajibu hoja kadhaa halafu nitakuja kwenye Maazimio. Jambo la kwanza ambalo nilikuwa nataka kulizungumza ni kuhusiana na haja ya upande wa Serikali na watendaji kuchukulia Taarifa za *CAG* kwa uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, umesema hapa mwezi Juni tulikuja hapa kupitia utekelezaji wa Serikali wa maagizo ya *CAG*. Kwa upande wetu sisi Serikali za Mitaa mpaka tunatoa taarifa hapa, kulikuwa hakuna agizo hata moja lililotekelezwa kwa ukamilifu wake. Kwa hiyo tunavyosema Serikali muwe makini tunasema muwe makini na muwe *serious* kwa sababu sisi tunakutana na maafisa masuuli kwenye vikao vya Kamati. Ni muhimu ikaeleweka kwamba majibu ambayo yataua ama kumaliza hoja za kaguzi siyo majibu ambayo Mawaziri mnatupa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majibu yatakayomaliza hoja za kaguzi ni majibu ambayo Mkaguzi atayapata kwenye vikao lakini vile vile wakaja kufanya *verification* kwamba tumesema tumekwama hapa, Serikali mnajibu hapana hatujakwama tumeenda hapo; unayetakiwa kumpa uthibitisho ni Mkaguzi wa hiyo hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mantiki hiyo maelezo waliyokuwa wanayatoa Mawaziri hapa na sisi ambao tulikuwepo kwenye vikao mpaka juzi, *mock LAAC* za mwisho kwenye *LAAC, mock LAAC* yaani vikao kati ya Ofisi ya *CAG* na upande wa Serikali vilifanyika kuanzia Oktoba 3, Oktoba 2, Septemba majibu yaliyokuja ndiyo yamepelekea Taarifa zetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi ndugu zangu; kama kweli tuna dhamira ya kusaidia hii nchi iende, hayo majibu mnayoyasema kwa sasa hayana maana mpaka *CAG* aka-*verify*. Kwa hiyo, ni muhimu mzingatie hilo Mawaziri na mimi kwenye Kamati yetu wamekuja Mawaziri wa TAMISEMI, wawili Naibu Mawaziri wanamuwakilisha Waziri wanakuja na Makatibu Wakuu. Kwa hiyo, ninashangaa Waziri anasimama hapa anasema yeye kwake anakuja anakuta hapa ni kitu kipya, hili ni jambo ambalo mnatakiwa mjue wote. Waziri aje na Katibu Mkuu wake aje; akituma mtu aje akupe mrejesho. Ndiyo tunasema hakuna *connectivity* ya kazi au utendaji kazi hakuna *connection*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana watu waliopewa dhamana ya kusimamia fedha za nchi hii hawana uchungu wa kusimamia fedha za nchi hii. Kunahitajika nguvu ya ziada, kunahitajika mkono wa chuma kusimamia watu waliopewa

dhamana ya kulinda fedha zetu; kwa nini nasema hivi? Tunataarifa hapa ya madeni kwa mfano ambayo hayakupelekwa kwenye mifuko ya hifadhi (makato).

Mheshimiwa Spika, unakuta Halmashauri ya Mpanda kwa mfano, hawakuwasilisha shilingi milioni 56.52 lakini kwa sababu mifuko yetu inavifungu vya adhabu vya faini inayotolewa kila mwezi kwa watu ambao hawapeleki michago; leo Mpanda adhabu ni shilingi milioni 514. Tuje Bunda, walitakiwa wapeleke shilingi milioni 56, hawakupeleka; faini shilingi milioni 114. Shinyanga, walitakiwa wapeleke shilingi milioni 205 hawakupeleka. *CAG* anasema eti faini imeenda mpaka shilingi bilioni 45, sisi tunajiuliza hawa watu walizembea muda gani mpaka faini zika-*accumulate to this sum? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu wamepewa dhamana. Hivi ni vitu ambavyo kama *chain* ya Serikali inafanya kazi ipasavyo, kuanzia Wakurugenzi, kuanzia Wakuu wa Mikoa, kuanzia Mawaziri wangeviona hivi vitu; huwezi kukaa usubiri *CAG* aje aone hivi vitu. Nilisikia hapa watu wakizungumza kuhusiana na *CAG* jukumu la *controllership* la *CAG* kwa mujibu wa Ibara ya 143(2)(a) ya Katiba kwa sababu kuna maeneo matatu ambayo ni majukumu ya *CAG*.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wake uko kwenye (a) kuhakikisha kwamba fedha zozote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali matumizi yake yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 136 ya Katiba hii na iwapo watatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo basi ataidhinisha hizo fedha zitolewe. Hiyo ndiyo udhibiti, *role* aliyopewa *CAG*. Sasa mnataka *CAG* akafanye kazi ambazo wanatakiwa wafanye Wakurugenzi huku ya kukimbizana hela? *Come on! (Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, hivi tunsema tumeajiri watu wa kazi gani? Ndiyo maana nikisikiaga eti imeundwa *task force,* nasema *task force* ya nini? Yaani mmeajiri watu, mnalipa watu mishahara, wamesababisha tatizo, kuenda ku-*rectify* tatizo mnaunda *task*

*force? For what? For what?* Kuna tatizo kubwa sana la mfumo ambao lazima wafanyie kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili; ni bahati mbaya natakiwa nijibu zangu tu, yaani ningekuwa nachanganya na nyingine watu hawajali. *IPTL,* hizi fedha hizi wanazoenda kulipwa ni za watu kutokujali, ni *deal* tu, kwa sababu Serikali ilienda kuweka fedha kwenye *Escrow Account*. Ule mkopo ulitakiwa ulipwe *Escrow Account* haikulipiwa. Si mfuate maneno ya mtaani wakati ana watu. Nimesema tu nachanganya; watu hawajali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *SYMBION* katika taarifa ya mwaka jana alilipwa zaidi ya milioni 300 ambazo hakutakiwa apewe, watu hawajali. Tunataka mjali. Siyo sifa kupanda VX na kuwa Waziri pekee, siyo sifa kupanda VX na kuwa Katibu Mkuu, sifa tendea haki nafasi yako.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako ya *LAAC,* nawashukuru wajumbe wangu tunafanya kazi mpaka saa sita usiku. Siku moja niliwaambia, wa TAMISEMI niliwaambia kazi inayofanywa na *LAAC basically* ni kazi iliyotakiwa ifanywe na wakurugenzi, ni kazi iliyotakiwa ifanywe na TAMISEMI. Sasa mnatuletea vitu ambavyo vimeshindikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi vitu vinauma, vinakera, vinachefua. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge mmechangia vizuri. Hivi nchi hii wakurugenzi tunawapataje? Yaani mtu ambaye mmempa dhamana ya kwenda kusimamia halmashauri kitendaji kuwa *accounting officer* kupokea mabilioni ya shilingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo kule kwenye halmashauri zinaenda *billions of money,* ukiuliza mkurugenzi amepatikanaje? "Kashindwa kura za maoni", wapambe. Maana nimegundua nchi hii yaani ukishakuwa kiongozi, yaani kabla hujawa mtu mkubwa wapambe hawapo ukishapata nafasi zenye uteuzi wapambe wanakuzunguka. Mamlaka ya uteuzi inawezekana *group* hili la wakurugenzi ninaamini linavurugwa na wapambe zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba sana, kama nchi tuangalie upya namna wakurugenzi wetu wanavyopatikana. Nilikuwa napitia kitu kinaitwa *the local government financial memorandum* ya mwaka 2009. Kuna kitu kinaitwa *responsibilities of the director*. Yaani kuna *responsibilities* hapa kama 12, ni nzito ambazo zinahitaji mtu mwenye weledi na taaluma na uzoefu wa hali ya juu katika usimamizi wa fedha, katika kusimamia watu, katika utawala na mambo mengine.

Mheshimiwa Spika, tumeshuhudia wakurugenzi tuliokutana nao huko unakuta kakurugenzi yaani katoto, *DT* ni kama baba yake. Ukiuliza umetokea wapi? "Nimetokea sekta binafsi", hasemi sekta binafsi wapi. Kwa hiyo, ukiangalia hata *wage bill,* muulize Mheshimiwa Mwigulu hapo. *Wage bill* inaongezeka kwa kiwango kikubwa kwa sababu moja kubwa, tunaokota watu nje ambao hawakuwa kwenye mfumo, tunampa nafasi ya kulipwa mshahara mnono. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, turudie utaratibu wa kila wenye vigezo vilivyowazi watu washindanishwe. Mimi nina mifano yangu hapa, mtiririko wa makusanyo ya mapato. Unakuta halmashauri kama *Kigoma DC,* nadhani, ilikadiria kukusanya shilingi milioni 700 ikakusanya shilingi milioni 688. Kigoma *DC, OC* iliyotoka Serikali Kuu; yaani hapa kuna watu wameshiba, watu wazima na akili zao, shilingi milioni 688 mwaka mzima. Yaani akili zao zote zile milioni mia 688 makusanyo ya ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukija kiasi cha *OC,* matumizi ya kawaida walichochopewa na Serikali Kuu ni shilingi bilioni 16.3. Yaani kuna watu wazima wamekaa kule chini wanalipwa mshahara. Hiyo ni *OC,* sijazungumzia miradi ya maendeleo fedha ilivyoshushwa. Sasa unajiuliza hivi kuna faida gani ya kuwa na wakurugenzi, maafisa mipango na ma-*DT* kule chini ambao hawako *creative* ku-*deal* na vyanzo vya mapato, ama kuhakikisha vilivyopo vinatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unakutana na mkurugenzi anakwambia kwamba sisi tunafanya shughuli ya kilimo. Kwa kuwa mvua hazijanyesha mapato yetu yameshuka, mkurugenzi! hivi hizi ni

akili? Kwamba ameweka pale kusubiri mvua? Sawa, si lazima uwe mbunifu, kama unasubiri mvua kuwa mbunifu na umwagiliaji. Kama huna, tafuta vyanzo vingine, tengeneza fedha itengenezwe. Tuna wakurugenzi ambao hawana uwezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba sana Serikali iweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Madeni ya wazabuni, tumeweka maazimio yetu naamini hayajabadilika, ni yale yale tu, kwa hiyo, tutayapitisha tu haraka haraka.

Mheshimiwa Spika, madeni ya wazabuni ni *crisis* nyingine, alisema Mheshimiwa Hawa Mwaifunga hapa, kwamba hii ni *sampling*. Si mkaguzi amesema bilioni nane *point* kadhaa, sisi tumekutana na halmashauri takriban 79 kwenye hii mikutano miwili. Hii juzi tumekutana na 39. Kwa fedha tu za ndani za halmashauri pekee hii taarifa ya *CAG* inazungunguka mara mbili. Si alisema shilingi bilioni nane, tunazungumza hizi halmashauri ambazo tumekutana nazo sasa hivi, na hazifiki 40; hamlipi fedha za wazabuni. Sasa tumeingia sisi kufanya kazi ya Serikali. Mnajua mlichofanya? Mkiambiwa mdawaiwa shilingi ngapi na wazabuni? shilingi kadhaa, mwaka huu mmefunga kiasi gani? Wakasema hapana tumetenga kidogo. Ndiyo *allocation* mnaenda kufanya Disemba? Ndiyo; fanyeni *reallocation,* mwaka ujao shilingi ngapi.

Mheshimiwa Spika, yaani sisi tunaweza kuwa na vikao vya Kamati kuwafanyia mambo ambayo mlitakiwa mfanye ninyi. Kwa hiyo, kila mkurugenzi aliyekuja kwenye Kamati yetu tumeshampa mpango wa kwenda kulipa wazabuni wote. Lakini najiuliza; kwa nini sisi wajumbe wako tukeshe, yaani sisi tukeshe halafu jamaa wapo hapo, haiwezekani. Natambua kazi ambayo Mchengerwa ameanza nayo, natambua, lakini tunasema hivi, kama Mheshimiwa Mchengerwa hamtatatua dudu la wakurugenzi wa hovyo wanaopatikana, wasiokuwa na uwezo; siyo wote, kuna ambao wanaweza, niseme neno baadhi, wasiokuwa na uwezo. Nakwambiaje, utaishia kutumbua. Yaani itakuwa miaka yako inaisha unatumbua, ukimaliza kutumbua huyu, unakuja unatumbua mwingine halafu fedha ya umma imepotea. Tuanze kutibu tatizo *from the core* tuangalie *source*.

Mheshimiwa Spika, sasa nashauri, yeye ni Waziri bwana, mimi sina *access* na Mheshimiwa Rais; akamshauri Mheshimiwa Rais ili aliangalie hili eneo kwa mapana na mawanda yake kwa sababu kuna *impact* kubwa sana tukiwa na wakurugenzi wazuri kule chini. Yaani *impact* kubwa ya kimapato ya kiutendaji na kiufanisi. Tufikirie nje ya *box. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni la madai ya wafanyakazi, bilioni 119. Sasa ndugu yangu Simbachawene naona hayupo; amekuja hapa katutajia *figure* zake kaondoka. Sasa hajatwambia katika *figure* zake zile Serikali Kuu ni ngapi, halmashauri ni ngapi. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Usiwe na wasiwasi Waziri Mkuu yupo.

**MHE. HALIMA J. MDEE – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA Bunge YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Waziri Mkuu yule kijana wako; amekuja ametutajia *figure* zake kaondoka, si ndiyo? Sasa mimi na timu yangu kwa taarifa ambayo mpaka tunawasilisha taarifa yetu Bungeni na kwa Spika na ambayo *Mock LAAC* zilivyokaa zimethibitisha ni kwamba kwenye halmashauri kuna bilioni 119 hazijalipwa. Hii taarifa imeeleza kila halmashauri inadai kiasi gani. *(Kicheko/Makofi))*

Mheshimiwa Spika, wanakuja watu wa Wizara tunawaambia *okay,* Wizara ya fedha ninyi si mmesema mmelipa bilioni ngapi, wanatutajia *figure* za kutisha ili kukupoteza *confidence*. Sawa basi twambie hivi, halmashuri hii mmelipa nini, halmashauri hii mmelipa nini, wanakimbia, hawana majibu. Sasa sisi tunasema hivi, mpaka sasa licha ya majibu aliyoyatoa kaka yangu Simbachawene hapo, ya kwake, ambayo hayajawa *verified,* Serikali inatakiwa ilipe madai ya watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Jesca amezungumza hapa, tulikuwa Kigoma nadhani kama siyo Kigoma ni halmashauri moja wapo. Yuko *DT…*

*(hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie. Halmashauri mojawapo, Kigoma *DT* amekaa pale anatujibu maswali amenyong'onyea. Sasa Jesca akafanya utundu kidogo, akachukua kile kitabu akaanza kuchambua baada ya kusikia watu wamejitambulisha. Kumbe yule jamaa *DT* anaidai Serikali shilingi milioni 40, yaani amekaa pale ndiye *DT* halafu ndiyo tunategemea yeye atupe majibu, kalipeni watumishi wa umma. Kujisifu kwa mbwembwe hakusaidii, mbwembwe zitajijibu zenyewe kwa matendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa sehemu ya tatu, tunaomba sasa Bunge likubali mapendekezo yale ya Kamati kama nilivyoyasoma na kama ambavyo *Hansard* imeyaingiza. Baada ya kusema hayo nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja ili mapendekezo yetu ya Kamati yaweze kupita. *(Makofi)*

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mwenyekiti…*(Makofi)*

Ahsante sana, ahsante sana, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono, na sasa nitawahoji kama Kanuni zetu zinavyotaka.

Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* kuhusu ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2022 waseme ndiyo. Wasioafiki waseme siyo. Wote wameafiki, ahsante sana. Kwa hiyo, yaliyokuwa mapendekezo ya Kamati sasa nini maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma Mheshimikwa Deus Sangu aje ahitimishe hoja ya Kamati.

**MHE. DEUS C. SANGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA (PIC):** Mheshimiwa Spika, naomba kwa moyo wangu wa dhati kwanza nitoe shukrani zangu kwa waheshimiwa Wabunge wote waliochnagia hoja ya Kamati yetu ya *PIC,* Kamati muhimu ambayo inasimamia uwekezaji wa mitaji ya umma. Nitambue michango ya Waheshimiwa Wabunge wote ambao idadi yao ni takriban Waheshimiwa Wabunge 30 michango yenu tunaithamini na kama Kamati imetupa nguvu ya kusonga mbele, tumeona kweli Waheshimiwa Wabunge mnatuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaenda kwenye kutoa ufafanuzi wa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge na hoja zangu za msisitizo kuna jambo ambalo naomba nifanye kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameweka msukumo wa pekee katika kuwekeza mtaji katika mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, hadi ninavyokuja hapa kuwasilisha ripoti ya Kamati yetu Serikali imewekeza katika mashirika ya umma mtaji wa trilioni 73.36. Na kwa miaka mitatu ongezeko lilikuwa ni shilingi trilioni 8.17. Ni uwekezaji mkubwa. Huu uwekezaji umewekwa kwenye mashiirika 304. Mashirika yameongezeka kutoka 298 yamefika mashirika 304.

Mheshimiwa Spika, taifa kuwa na *state enterprise* mashirika yake ni jambo ambalo ni muhimu sana; na mashirika haya yana maana kubwa katika ku-*drive* uchumi wa nchi wa nchi. Moja katika jambo ambalo Serikali iliamua kuanzisha hakuna shirika hata moja lilianzishwa kwa bahati mbaya. Kila shirika la umma

lililoanzishwa lilikuwa na misingi yake na lina maana kwa ajili ya kusukuma jambo fulani katika Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea swala ambalo ndilo jambo la msingi ndilo *core objective,* hasa yale mashirika yanayofanya biashara kuhakikisha kwamba yanaleta faida na kupeleka gawio kwa Serikali. Hapa katika Kamati yetu tulitumia muda mwingi kuchambua haya mshirika umma. Kati ya mashirika 66 ni mashirika 25 tu yanayofanya biashara ambayo yako chini ya sheria ya makampuni sura ya 188, ni mashirika 66 tu.

Mheshimiwa Spika, kati ya mashirika 66, ni mashirika 25, taasisi 25 tu ndizo zimeweza kupeleka gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Hapa naomba nitoe ufafanuzi. Shida ni kwamba sheria zipo lakini kuna taasisi zinakaidi kupeleka gawio kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Sasa katika hizo taasisi 25 kichekesho ni taasisi tatu tu ndizo zinachukua asilimia 93 ya fedha zile shilingi bilioni 372 zilizowekezwa kwenye Mfuko wa Serikali. Hapa nakupa *task* Mheshimiwa Waziri wa Fedha; yaani una taasisi 66 taasisi 25 hizo zilizojitoa kimasomaso, na hilo si jambo la kufanya kama ni *charity contribution,* ni jambo la kisheria, ni takwa la kisheria, ni taasisi tatu tu ndizo zimepeleka asilimia 93.

Mheshimiwa Spika, kuna *category* ya pili ni wale wanaotakiwa kupeleka mapato ghafi, mashirika, taasisi zile ziko 25, hawa nao ni taasisi chache zilizopelekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali, watu wanajifanyia wanvyotaka. Kuna *category* ya tatu ni taasisi zile zinazobaki ambazo hazijawekewa utaratibu. Hizi ni kwa hiyari, wanavyojisikia hapa napo kuna kichekesho.

Mheshimiwa Spika, taasisi hizi kuna taasisi nitawapa, na siku natoa taarifa hapa uliniambia rudia mwenyekiti sehemu hiyo. Kuna taasisi inaitwa Bodi ya Chai Tanzania. Hawa wao kwa miaka mitatu kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali walipeleka shilingi milioni mbili. Pale nilipokuwa nasoma ulidhani labda kuna *error,* milioni mbili. Maana yake ni *average* ya shilingi laki sita na nusu kila mwaka ndiyo wanapeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Huu ni utani na hauwezi kukubalika; na ndiyo maana unaona *state enterprise* nyingi zinakufa kwa sababu kuna mizaha mingi.

Mheshimiwa Spika, nataka niseme tena kwa uchungu mkubwa, yule binti ni *DG* sina maana ya kum-*offend* amekuja pale ana timu ya wataalam wafikao 20, wamekuja pale Kamati tume-*raise* maswali zaidi ya 15, 16; alifika pale aliweza kujibu maswali mawili tu. Nilimtimua nikasema wewe sasa hujui majukumu yako, nikawaambia sasa huyu timu aliyoleta hapa imetumia zaidi ya shilingi milioni 10 anapeleka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi milioni mbili ni utani kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo haya mambo yanafanyika na hapa tusiposimama madhubuti na hapa Kamati yetu mbele ya Bunge lako Tukufu nasema kwa haya mashirika ambayo kisheria yanatikiwa hayapeleki wasiwe wanakuja hata kwenye Kamati yetu maana wameshindwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo haya mambo yanafanyika na hapa tusiposimama madhubuti mbele ya Bunge lako Tukufu na hata kwenye Kamati yetu nasema, kwa haya mashirika ambayo kisheria yanatakiwa kupeleka, lakini hayapeleki wasiwe wanakuja hata kwenye Kamati yetu, maana yake wameshindwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jukumu tunapotoka hapa ndiyo kazi ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenda kufanya. Wakiacha zile fedha zibaki kule maana yake ni nini? Watu si fedha zinabaki kwao, hawajapeleka kwenye Mfuko ambao ungeenda kujenga zahanati na vituo vya afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wanaanza kugawana *honorarium*, wanaanza kugawana *bonus*, wanaanza kutafuta safari za nje, wanaanza kutafuta semina yaani wanatafuta wafanye tu *nugatory expenditure*, matumizi yasiyo ya lazima, kwa sababu hela ziko kule hamna anayejali kwenda kuzifuata. Baadaye tutakuja hapa tuunganishe mashirika, tutakuwa tunafanya biashara ya kuunganisha, tutaunganisha baadaye *state enterprises* zote zitaisha hatutakuwa na taasisi ya Serikali. Kwa hiyo, hili jambo naliongea kwa uzito wake na kwa uchungu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la gawio, *category* ya wale wanao-*fall* kwenye Sheria ya Makampuni, ile Sura 180 waka-*comply* wote. Kama hao 66 wote waliopata faida na wanatakiwa wapeleke, wakapeleke hiyo kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali na tuje tupate taarifa ndani ya Bunge hili, la sivyo tutakuwa tunafanya mchezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wale ambao wanatakiwa kutoa asilimia 15 ya mapato ghafi, *gross revenue* wanatoa asilimia 15, hao nao ziko taasisi 25. Waziri wa Fedha akafanye yeye ndiyo anamsimamia Msajili wa Hazina, akahakikishe pia mashirika hayo yanapeleka fedha kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bila kufanya hivyo tutakuwa tunacheza *dilly-dally* na haya mashirika tutaona watu tu wananenepa, wanatembelea magari mazuri, wanaishi maisha ya raha na starehe, kumbe kuna wananchi huko kwenye zahanati wamekosa dawa. Kuna wananchi huko kwenye vituo vya afya wanakufa kwa sababu hatujatimiza wajibu wa kuyasimamia haya Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala hilo la Mashirika ya Umma ambayo shilingi bilioni 272 katika uwekezaji wa trilioni 73.32 ni utani. Sawa, kuna yale yanayotoa huduma, hata haya yanayofanya biashara? Yanaweza yaka-*raise trillions of monies* zikaingia kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa hiyo hii ni *assignment* ambayo kama Kamati tumei-*pose* na tutakuwa wakali na ukali wetu watauona, Waheshimiwa Mawaziri watapata *message* kwamba kuna moto unawaka huko *PIC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naondoka kwenye suala la gawio, naingia katika suala la mikopo chechefu. Mikopo chechefu nitaanza na suala la SUMA JKT. SUMA JKT ni kampuni iliyoanzishwa, kwanza ni kampuni ya mkakati, ilikuwa kama *shock absorber*. Inapotokea taasisi nyingine zinafeli za *private* tuwe na *state enterprise* inaweza ika-*take off*. Sasa hapa kuna shida, SUMA JKT tuliamua kuiua, SUMA JKT ilipewa mradi wa matrekta na zana

nyingine za kilimo wa shilingi bilioni 61. Waliletewa, yaani hawakupewa fedha walipewa mkopo *in terms* ya vifaa.

Mheshimiwa Spika, lengo lilikuwa ni ku-*boost* sekta ya kilimo inayoajiri Watanzania zaidi ya asilimia 70. Kwa bahati mbaya pale palienda kufanyika uhuni wa ajabu. Yale matrekta yaligawiwa kama sadakalawe. Waheshimiwa Wabunge wa wakati huo na wengine wapo walichukua matrekta yale, ma-*DC,* Wakuu wa Mikoa na viongozi wengine wa Serikali waligawana. Mtu mwingine alikuwa anaenda kuchukua hadi matrekta matatu. Madhara yake ni nini? Ndani ya SUMA JKT pale kwenye kipengele tu cha mkopo wa matrekta tumezalisha shilingi bilioni 38.77 kama mkopo chechefu, haulipiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, orodha hii ipo na tumewaomba SUMA jana nilitaka nije nao hapa mimi ninge-*display* kwa majina. Kwa haraka haraka ningepiga *sampling* hapa. Naomba Bunge lako tupate orodha ile kwa rejea, kama Kamati tunayosimamia mitaji ya umma tuone ni namna gani Serikali ita-*recover* hizi fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *category* ya pili, ilikuwa ni vifaa. Kuna vifaa pale SUMA JKT vya shilingi bilioni 11, vipo pale haviuziki. Katika hiyo pesa waliyopewa ya vifaa vya shilingi bilioni 61, vifaa vya shilingi bilioni 11 haviuziki. Mkulima akienda pale vimepitwa na wakati, haviwezi kutumiwa. Madhara yake ni nini? Madhara yake ni kwamba sasa vile vifaa tunaenda sijui kupima chuma chakavu? Sijui tunavifanyaje? Yaani tunaenda ku-*sank,* tunaenda ku-*establish sank cost* ya shilingi bilioni 11, yaani shilingi bilioni 11 hivi hivi, vipo pale SUMA JKT.

Mheshimiwa Spika, *category* ya tatu, ndiyo hayo madeni mengine, wanajitahidi. Naomba jambo moja katika hili na Serikali wako hapa. Kwanza, wakapambane na mkopo wa SUMA JKT. Pili, kwenye kupambana na jambo hili kusiwe na mzaha na asionewe mtu yeyote aibu. Hata kama kwa upande huu ndugu zangu Mheshimiwa Waziri kuna watu wapo wakarudishe hizi fedha za matrekta. Kwa sababu hizi fedha ni *revolving fund* ambayo

itakuwa na-*multiply effect* ya kwenda kukopesha wakulima wengi na tuta-*boost* sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumei-*paralyze* SUMA JKT na hatujaishia hapo, tunaendelea kuiua SUMA JKT. Wametoa huduma Serikalini za kufanya ulinzi, usafi na mambo mengi wanafanya hawa SUMA JKT, wanadhulumiwa hawalipwi. Pale SUMA JKT anapompeleka mlinzi hampeleki bure, Askari yule analipwa mshahara na mnaona askari wa SUMA JKT wanavaa *uniform* safi sasa SUMA JKT hiyo hela ya kuwavalisha askari na kuwalipa mshahara anatoa wapi? Serikali na taasisi nyingi za Serikali hawalipi. Madhara yake ni nini? Madhara yake ni kwamba hii kampuni inaenda kufa na ikija hapa tutaomba sijui tu-*merge,* tufanye nini, tufanye *liquidation*, mambo kama hayo, litakuwa ni jambo la kufanya *post-mortem. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili jambo linatokana na kwamba mashirika haya yapo yote 304, hayana *instrument* ya kuyasimamia. Yupo mtu anaitwa *TR,* yaani *TR* ni mtu tu anaenda kutembea, hana *instruments*, hana meno ya kusimamia hizi taasisi, yaani ukitoa hivi tumekuja *PIC* kama Kamati sisi ndiyo angalau tuna meno ya kuya-*screw* haya mashirika. Baada ya hapo Bodi zinajiendeshea mambo. Kuna taasisi zina mambo ya ajabu, bodi fulani iliidhinisha Mkuu wa Shirika moja hivi aliidhinisha bima ya maisha ya Board Members wake na anaulizwa anasema, nimeona niwakinge na *risk Board Members* wangu, yaanio ametumia *billions of monies. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hatuwezi kufanya mambo haya, mashirika yetu yatakufa. Hapo ukiwa na bodi hivi itatokea tu *CAG* akija tutakuwa tunafanya *post-mortem*. Lazima *TR,* Sheria hii Sura 370 ya Msajili wa Hazina irekebishwe, *TR* apewe meno, asiwe mtu wa kwenda kutembelea na mtu anasema haya yako kwa *TR*. Yako kwa *TR*, sawa lakini hawezi hata kuziwajibisha Bodi, hawezi kufanya *periodic review performance*. Hata *KPI* zile tunazowapa Wakuu wa Taasisi na Wenyeviti wa Bodi, *TR* hawezi kufanya, yeye anaenda kutembea tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru Bunge lako kuanzisha hii Kamati ya *PIC*. Ni moja kati ya Kamati muhimu sana za kusimamia

hizi taasisi za umma. Naamini kama Mwenyekiti na Wajumbe wangu wa Kamati tutafanya kazi hii kwa weledi mkubwa ili kuyanusuru mashirika yetu ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeongelea deni chechefu hilo la SUMA JKT. kuna mtu anaitwa *TEMESA*, SUMA JKT anamdai *TEMESA* alichukua huduma ya ulinzi na usafi shilingi bilioni 1.11. Yaani shilingi bilioni nzima *TEMESA* wanayo ya SUMA JKT. Mwaka huu SUMA JKT ameingia kwenye *competitive tendering,* amekosa tenda ameingia *private operator*. Yule *private operator* yeye hana shida analipwa vizuri ila SUMA JKT ndiyo hatakiwi kulipwa. Tafsiri yake ni nini? Huku SUMA JKT huwezi kuchukua *ten percent* lakini *ten percent* kwa *private operator* utaipata. Sasa hiyo *logic* ndiyo hiyo hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana unaona *DAWASA* watu wametumia maji, Taasisi za Serikali zimetumia maji ya *DAWASA* ya bure ya shilingi bilioni 13. Shilingi bilioni 13 na Vyombo vya Ulinzi na Usalama tuko hapa, Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani katika eneo hili Waziri anahusika sana, akasimamie vyombo vyake vya Ulinzi na Usalama vikalipe bili ya maji waliyotumia *DAWASA*. Sisi kama Kamati hatutakubali jambo hili liendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu inayokuja kutolewa hii *DAWASA* yenyewe wanaenda ku-*collapse*, itakufa. Wanatumia huduma bure, Bunge hili tunapitisha matumizi kwa hiyo sisi tutazipitisha hizi *OC* za maji unapeleka wapi? Kwa nini wasilipe bili za maji? Hizi *OC* za ulinzi tunapitisha kwa nini hawalipi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona nitolee ufafanuzi wa jambo hili, narudi palepale kwenye mikopo chechefu. Ameongea ndugu yangu Mheshimiwa Bashe hapa *AGITF* – Mfuko wa Pembejeo wa Taifa. *AGITF* ilianzishwa tangu miaka ya 90 na lengo lilikuwa kwenda kukopesha wakulima zana za kilimo na pembejeo. Huu Mfuko ukageuka kwanza ukawa unaendeshwa na *political interest*. Waziri Bashe nikiwa Waziri wa Kilimo nitafanya ninavyojua, nitaenda kwenye sehemu yangu nitawagawia na watu ukiwapelekea kwa misingi hiyo bila kufuata *credit policy* na

mambo mengine umewapa hiyo ni kama umefanya *bonus* tu watachukua.

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana hii *AGITF* imefika na *portfolio* yake ya shilingi bilioni 26, shilingi bilioni 20 ni mikopo chechefu. Mpaka Juni 30, shilingi bilioni 20 ni mikopo chechefu, sawa na asilimia 81. Takwa la kisheria ni ku-*maintain portfolio* ibaki, tunasema *portfolio at least* ibaki asilimia tano. *AGITF* nashukuru na napongeza uamuzi aliochukua Mheshimiwa Bashe wa kuvunja *management*. Bodi mpya namwamini *CEO* mpya yule ndugu yangu *engineer* Omary kwa maana ya Mwenyekiti wa Bodi na *CEO,* amemtoa kwenye *private sector, bank* wata-*drive,* lakini wale aliowaondoa haitoshi, hela za umma zimepotea. Kachukue hatua zaidi za kinidhamu na kisheria tuwaone wengine kwenye kesi za uhujumu uchumi, tuwaone watu wanawajibika huko kinidhamu, siyo tu kuishia kuwatengua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kama ukinitengua mimi nimeshajipa tayari *gratuity* ya shilingi bilioni 20 nimeshajitangulizia mbele, nina shida gani? Wataendelea tu na maisha mengine. Kwa hiyo, Mheshimiwa Bashe katika hili mimi ni mmoja ambaye nime-*discuss* naye zaidi ya masaa matatu juu ya *AGITF*. Nimekuja na *proposal* na ndiyo maana watu walishangaa kwa nini una-*propose* baadhi ya mikopo ifutwe.

Mheshimiwa Spika, ni *principle* ya kihasibu, kuna mikopo imeishi pale zaidi ya miaka 30, yaani ilikopeshwa miaka ya 90. Ime-*accumulate* inasomeka kule kama *non-performing loans.* Zile hakuna *possibility* yoyote ya kuweza kuzi-*recover* zaidi ni ku-*write off*. Tuki-*write off* tuna *clean* vitabu, tunafanya *aging analysis* ya mikopo. Tukifanya *aging* tunaya-*cluster* yale ambayo hayawezekani, *we write off* hakuna *option,* hatuwezi kukaa nayo miaka, 100 yale yanayokusanyika tunayakusanya, ndiyo jitihada unayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, *USAID* wametusaidia *IFAD* wanatusaidia, *TaDB* wanatusaidia lakini ili uje upate *potential investor* kwenye taasisi zetu, hakuna *potential investor* atakayekuja ku-invest

kwenye taasisi yako wakati mizania ya vitabu vyako iko hatarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nani anakuja kuweka hela kwenye mikopo chechefu asilimia 86? *AGITF* hii ilikuwa *almost a dead state enterprise*. Kwa hiyo, sisi kama Kamati tunaosimamia Mitaji ya Umma tutampa Mheshimiwa Bashe *backup*, tutampa *support*. Tunaomba tu mambo haya tunayoshauri wakayafanyie kazi na *next time* wenzangu wamekuwa *popular* wanaongea mambo ya *CAG,* lakini huku kwenye Mitaji ya Umma huku tukisimamia vizuri kuna tija kubwa sana. Huku hatutaji wizi, lakini nimekuja na namba, najaribu kutoa vitu hivi, namna gani tunaweza tukaandaa taasisi zetu za umma ili kesho na kesho kutwa ziwe na tija na zisaidie kuleta mapinduzi ya kiuchumi kwenye Taifa hili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mwenyekiti malizia.

**MHE. DEUS C. SANGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA (PIC):** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa muda, nina mambo mengi, lakini kwa sababu ya muda naendelea kusisitiza yale mambo ya muhimu. Suala la *GPSA* ni jipu kubwa kwa sababu taasisi hizi zinaagiza magari yanachukua hata zaidi ya miezi 28, *CAG* kasema hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa ruhusa yako niseme jambo moja. Lengo la kuanzisha hii *bulk procurement* ya magari kwa pamoja ilikuwa ni tuwe na *volume* kubwa ili tukiagiza tupate *discount*. Sasa hivi hiyo *theory* haipo, ndiyo maana kila taasisi tulivyoinyang'anya tukampa *GPSA* tulitamani kupata unafuu, *value for money* tutaiona. Badala yake sasa imekuwa *disaster,* bei zimekuwa juu sasa tukatathmini upya jukumu hili *GPSA* bado analiweza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba kusema nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge na naomba mapendekezo yetu yote 14 tuliyoyatoa kwenye Kamati ya *PIC* yawe ni maazimio ya Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka naomba uketi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, sawa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji kuhusiana na na hoja ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya *PIC* kwa maana ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma inayohusu Taarifa ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Wote tumeafiki, kwa hivyo mapendekezo yaliyotolewa hapo yote yameafikiwa. *(Makofi)*

*(Mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwanza kabisa nitumie nafasi hii kuzishukuru sana Kamati zetu tatu kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kazi hii wameifanya kwa weledi mkubwa sana, kwa hiyo, tunawashukuru sana maana mmefanya kazi hiyo kwa niaba ya Bunge. Pia mmekuja na mapendekezo mengi ambayo

sasa ni Maazimio ya Bunge ya kuielekeza Serikali nini cha kwenda kufanya. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika kipindi hiki ambacho huwa tunajadili Taarifa ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kipindi tunachoisimamia Serikali na kwa hiyo, maazimio yanayopitishwa na Bunge ni maelekezo kwa Serikali.

Baada ya kuzishukuru Kamati zetu na viongozi wote wa Kamati hizi nitumie fursa hii kuwashukuru Wabunge wote kwa namna ambavyo mmeshiriki kwenye zoezi hili zima katika hizi siku tatu ambazo tumepata nafasi ya kujadili Taarifa za Kamati hizi tatu. Kwa hiyo, nawashukuru kwa ushiriki wenu na kila mmoja wenu kwa namna ambavyo amesoma taarifa hii na ameweza kuchangia.

Ukiacha yale ambayo ni maagizo kwa Serikali pia wamesikiliza michango yenu katika maeneo mbalimbali na kwa namna ambavyo Waheshimiwa Mawaziri walipata nafasi ya kuchangia hapa, kwa maneno waliyoyasema sina shaka kwamba wameyachukua na hayo ya ziada ambayo mmeyazungumza. *(Makofi)*

Sasa katika michango hiyo pia nitumie fursa hii kuishukuru Serikali kwa maana ya Maafisa Masuuli kwa namna ambavyo wameshiriki katika kuhakikisha Kamati zetu hizi zinafanya kazi zake vizuri kwa sababu wanahitaji kukutana nao ili waweze kukamilisha taarifa hizi. Nawashukuru pia watendaji wote wa Serikali ambao waliweza kwenda kutoa taarifa za ziada mbele ya Kamati hizi na nawashukuru Mawaziri kwa kuonesha ushirikiano ambapo Maafisa Masuuli kutoka kwenye taasisi zilizo chini yenu waliweza kufanya kazi hizi nzuri, kwa hiyo zimewawakilisha vizuri, nawapongeza nanyi pia. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia nitumie nafasi hii kumshukuru Msajili wa Hazina ambaye anafanya kazi na Kamati yetu ya *PIC* kwa kazi nzuri pamoja na changamoto ambazo zimeelezwa hapa, ametoa ushrikiano mzuri na haya yote ambayo Kamati

imeweza kusema, basi yataenda kufanyiwa kazi na Serikali. *(Makofi)*

Kwa kusema hayo kwa ujumla wake, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri mkiongozwa na Waziri Mkuu hapa Bungeni kwa ushirikiano mzuri pia ambao mmeuonesha kwenye ngazi ya Kamati zingine ukiacha hizi tatu, lakini mmeonyesha ushirikiano mkubwa, lakini hata kwenye hizi tatu yako mambo mbalimbali ambayo mmetoa ufafanuzi hapa. *(Makofi)*

Nafahamu iko changamoto kwa sababu Mawaziri mnalazimika kutoa ufafanuzi hapa katika mambo ambayo Wizara zenu huwa zinaalikwa kwenye hizo Kamati, lakini kwa namna ya utendaji kazi wake, mnajikuta kule wapo Maafisa Masuuli halafu ninyi hampo. Sasa wanatoa majibu ambayo wakati yanaletwa hapa na hizi Kamati zetu mnajikuta kwamba wakati mwingine yanakinzana na yale ambayo ninyi mnayafahamu.

Kimsingi ni kwamba sote tunapewa taarifa na hao watendaji, Waziri anakuwa amepewa na hao hao watendaji na Kamati zimepewa na hao hao watendaji, lakini nafikiri tufike mahali ambapo tunaweza kufanya kazi kwa pamoja ili Mawaziri mpate mrejesho kutoka kwa wale wanaoenda kwenye hizi Kamati, wakifahamu wazi wanawawakilisha ninyi kwa sababu humu ndani wao hawaingii, mnaingia ninyi zinapokuja hizi taarifa. Kwa hiyo, ni muhimu kujipanga kuhusu jambo hilo. *(Makofi)*

Hoja aliyoisema Mheshimiwa Bashe kuhusu utendaji huo wa jumla wa kuja kuulizwa maswali kwenye mambo ambayo anajibu mtu mwingine, naamini tukiboresha yale mawasiliano mambo yatakaa vizuri. *(Makofi)*

Pamoja na hayo iko changamoto ambayo imejitokeza nitaieleza pengine, iliombwa miongozo miwili katika kipindi hiki wakati tukijadili taarifa hizi mbili, lakini muda wetu umekwenda sana kwa hivyo hii miongozo nitaitoa siku ya Jumatatu tuvumiliane.

Sasa kuna mapendekezo mbalimbali ambayo yalitolewa wakati wa michango nataka niyaweke hayo vizuri ili isije ikaleta picha ambayo pengine haistahili. Kwanza, yalitolewa mawazo na Waheshimiwa Wabunge kwamba Taarifa ya CAG mjadala uhame kutoka mwezi Novemba kuelekea Aprili pale, yaani kwa maana kwamba taarifa ile ikipokelewa tu tuanze mjadala. Sasa limesemwa hilo likiwa limeunganishwa pamoja na lile la Waheshimiwa Wabunge wengine waliopendekeza kuhusu kuanzisha Kamati kwa ajili ya kufuatilia Maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwanza hili la mwanzo hapo la kuhusu taarifa ya CAG kupeleka mwezi Aprili. Mmesikia hapa Kamati zetu zikitoa taarifa juu ya Taasisi za Serikali zilizoenda mbele ya hizi Kamati. Haitaweza kufanyika hiyo kazi ndani ya siku moja, ndani ya mwezi mmoja. Kwa sababu hiyo, taarifa ya CAG inapotolewa, inatolewa kama taasisi ambayo imefanya kazi kwa niaba ya Bunge, lakini lazima iletwe kwetu, sisi Bunge tujiridhishe halafu tusonge nayo mbele na kuiambia Serikali nini cha kufanya. Tukifikiri kwamba tutaweza kuifanya haraka zaidi ya hii haraka tunayoifanya kwa sasa, kwanza hatutatenda haki, kwa sababu yale mapendekezo anayoyaleta CAG anayaleta kwetu kama Bunge ili sisi sasa tukishayatazama pale, tukayasikiliza ya Afisa Masuuli, tukasikiliza Serikali tutaweza kuchukua hatua stahiki, lakini tukisema tutaenda moja kwa moja tutakuwa hatutendi haki. Katika taarifa hizi za Kamati naamini mmezipitia mmeona kuna maeneo ambayo CAG alikuwa ameeleza, lakini wakati mwingine pengine kunakuwa si kutokusikilizana, lakini labda ni kutokusikilizana na upande wa taasisi za Serikali.

Wanapoenda mbele ya Kamati, basi wanaweza kupewa hiyo nafasi, CAG anasema yale kwa niaba yetu sisi, sisi tunawasikiliza upande wa Taasisi za Serikali na pale ndiyo tunaweza kufanya maamuzi kwamba maelezo tumeyasikiliza na tumeelewa hoja hii imekwisha. Maelezo tumeyasikia na kwa kweli haya maelezo tunasonga namna CAG alivyosema. Kwa hiyo, tusifike mahali tukaona kama vile kuna ucheleweshaji wa kushughulikia taarifa za CAG, ni kwa sababu ya mfumo wetu, hatuwezi kufanya haraka zaidi ya hapo tunapofanya sasa, la

sivyo tutakuwa hatutendi haki kwa wale watu ambao wanakuwa wametuhumiwa na taarifa za CAG.

Jambo lingine lililozungumzwa hapa na akasimama Mheshimiwa Mbunge mmoja, akataja na idadi kwamba Waheshimiwa Wabunge wameshafika 168 ambao wamejiandikisha kwamba wanataka sheria ibadilishwe, iletwe sheria hapa kwa ajili ya kunyonga ama kukata viungo watu ambao wamehukumiwa labda kwa ubadhirifu. Sasa mambo kama hayo wakati mwingine yanasemwa kwa sababu ni jambo ambalo kwa kweli hakuna mtu anataka uwepo ubadhirifu ndani ya nchi hii. Nia yao ni njema, lakini sasa hili jambo linalopendekezwa, kidogo tutakuwa tumetoka nje ya ule utaratibu wa kawaida. Ni kweli mmetumia mifano kwamba nchi nyingine, sasa hizo nchi nyingine ili tuweze kutoa mawazo yetu haya, lazima tujifunze na mambo mengine ya hizo nchi halafu tuone kama nchi tunataka kwenda vipi.

Waheshimiwa Wabunge, hivyo, nimeona nilifafanue hili lisije likatoa picha kwamba sasa Bunge limepitisha jambo lolote linalohusu kunyongwa ama kukatwa viungo wabadhirifu lakini Bunge kwa sheria zilizopo sasa, litaendelea kuisimamia Serikali ili iweze kuhakikisha wale ambao wanafanya ubadhirifu basi wanashughulikiwa kwa mujibu wa sheria zilizotungwa na Bunge hili kwa sasa.

Waheshimiwa Wabunge, jambo lingine lililokuwa limezungumzwa hapa nadhani nilishalieleza kwa sehemu, ni lile la uundaji wa Kamati Teule. Nimeshatoa maelezo kwamba tujaribu kwanza huu mfumo tuliouanzisha tuone utatupeleka kwa sehemu gani.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupitisha hizi taarifa zetu tatu za Kamati pamoja na Maazimio ambayo Waheshimiwa Wabunge mmeshahojiwa, kwa utaratibu ule ambao tulikuwa tumeshauanza huko nyuma, kama ilivyo ada Serikali itatuletea taarifa mwishoni mwa mwezi Februari kwamba wamefikia wapi katika haya ambayo Bunge limekubaliana siku ya leo kuiagiza Serikali.

Wakati huo huo tutajitahidi wakati wa mwezi Juni, kipindi kile cha Bajeti, Kamati zetu wakati zinaendelea kufanya kazi, basi taarifa hizi zitapewa hizo Kamati ili na zenyewe zifuatilie katika maeneo yake. Maana hizi Kamati tatu, bahati mbaya huwa hazipitishi Bajeti ya Wizara yoyote, lakini Wizara hizi zinaleta Bajeti kwenye Kamati zetu zile nyingine. Kwa hiyo, ni muhimu zile Kamati inapokuja Serikali na Bajeti yake, waulize yale ya utekelezaji wamefikia wapi, halafu muende vizuri katika ngazi ile. Huo utaratibu utalifanya Bunge zima liwe linashiriki zoezi la ufuatiliaji wa maamuzi yale tunayoyafanya kwa pamoja kwa sababu haya yote tunayoyazungumza yako kwenye Wizara mbalimbali. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa mtindo huo basi, nafikiri tutafika sehemu nzuri na kila Mwenyekiti aone hilo ni jukumu lake. Akishapitisha kule bajeti siyo unakuja humu ndani tena na wewe unaanza kulalamika, anza kufuatilia kule ili upewe majibu halisi na wananchi wanaposema sasa taarifa tumepokea mbona mnapitisha pesa nyingine, waelewe huo muktadha na wajue kwamba Kamati zetu zote zinafanya kazi kwa kushirikiana na wote nia yetu ni njema kwamba fedha ambazo Serikali inazitafuta kwa nguvu sana, na wengi wamesema hapa namna Mheshimiwa Rais anavyofanya kazi nzuri, zisipotee mahali. Anapoelekeza ziende, ziende huko na sote tunapopitisha bajeti basi tujue tunapitisha kwa muktadha huo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kulikuwa na hoja ambazo zilijitokeza ambazo ziko nje ya taarifa za CAG. Kwa namna zile hoja zilivyokuja na zinawahusu wananchi, imeniwia ngumu sana kuziacha pembeni. Kwa kuzingatia muda wetu ulivyokwenda, tunaweza tusiwe madhubutu, tusiwe *effective*. Tusiwe?

**MBUNGE FULANI:** Tija.

**SPIKA:** aaaha! Mjadala wetu usiwe na tija kwenye mambo hayo. Kwa hivyo, kama nilivyosema miongozo itatolewa Jumatatu, hoja aliyokuwa ametoa Mbunge wa Sumve, Mheshimiwa Kasalali Mageni na Mheshimiwa Waziri watapata

nafasi, lakini pia hoja aliyokuwa ameizungumza Mheshimiwa Ole Shangai na hoja ya Mheshimiwa Husna Sekiboko, zote tutashughulika nazo Jumatatu ili tuwe na tija katika mijadala yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na hayo, alisimama hapa Mheshimiwa Ole-Sendeka akisema Mwongozo. Sasa kwa sababu kwa kawaida Mwongozo hawezi kuubeba kutoka leo kwenda siku nyingine, lakini nafikiri Miongozo hapa leo ilikuwa mingi sana, kwa hivyo, tukubaliane kwamba Mheshimiwa Ole-Sendeka, kwa sababu Mwongozo anataka kujua kama jambo hilo linaruhusiwa ama haliruhusiwi, tutapata nafasi ya kujua alitaka kujua nini halafu Bunge litajulishwa kwa ajili ya kutunza pia afya zetu kidogo. Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa jambo la mwisho, kuna majina hapa nililetewa na hili nalo inabidi niliweke sawa. Kuna majina nimeletewa kutoka yale madeni ya *TANOIL* na kwamba wapo Wabunge humu ndani. Pia kuna majina nimeletewa kutoka upande wa madeni chechefu. Haya yale ambayo yanatokana na ule Mfuko wa Pembejeo.

Kwa namna ilivyosemwa inaweza ikaonekana kama vile kwa kuwa ni Waheshimiwa Wabunge ndiyo maana hawajatajwa. Wengine mbona wametajwa? Pia kwa sura iliyoletwa ni kama vile Waheshimiwa Wabunge ni wengi na mtu anaweza akajisikia vibaya kwa sura hiyo. Kwa muktadha huo, na kwa sababu hizi ni taarifa za kibiashara, na wanaohusika ni wafanyabiashara. Hiyo mikataba sijaletewa hapa ili nijue wana mikataba ya siri au ni mitakaba ambayo ni ya wazi kwa hiyo kila mtu anaruhusiwa kuiona. *(Makofi)*

Ili niweze kutaja ili watu wajue wanaposema Waheshimiwa Wabunge humu, kwa mfano kwenye hii ya pembejeo hapa ambao ni Waheshimiwa Wabunge mpaka leo, mmoja ni Mheshimiwa Mbunge mpaka leo, wengine walikuwa Wabunge kwa hiyo hawana sababu, mmoja amedhaminiwa na Mheshimiwa Mbunge. Kama anataja maana yake ni hao Waheshimiwa Wabunge wawili, Mheshimiwa Mbunge mmoja

amedhamini mwanakijiji mwenzake, na Mheshimiwa Mbunge mwingine yeye mwenyewe ndiye anayehusika.

Hii ya *TANOIL,* huku zimetajwa kampuni sasa naambiwa haya makampuni wamiliki ni Waheshimwa Wabunge. Mengine, Waheshimiwa Wabunge siyo wamiliki pekee lakini ni sehemu ya wanahisa wa hizo kampuni.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nataka kujua ili niwataje ama vipi ile mikataba ili tusije tujavunja sheria hapa ndani ambazo tumetunga wenyewe. Kwa sababu ni mikataba ya kibiashara, *TANOIL*, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, mikataba mliyoingia na hawa watu ni ya siri ama siyo ya siri? Mimi sitaki kuvunja sheria jamani. Ni mikataba ya siri ama siyo ya siri?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, mikataba ni ya siri.

**SPIKA:** Mikataba ni ya siri, haya. Mifuko ya Pembejeo, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo. Mikataba ni ya siri au siyo ya siri?

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, mikataba yote ni ya siri.

**SPIKA:** Haya. Mikataba ni ya siri. Kwa sababu hizo, inaniwia, tusikilizane Waheshimiwa. Kwa sababu hizo, inaniwia ngumu kuwataja hawa Waheshimiwa Wabunge kwa sababu nisingependa Bunge lishiriki katika kuvunja sheria.

Pamoja na hayo, hoja ya msingi kwenye hili ni kwamba wako viongozi wanaodaiwa na taasisi mbalimbali za Serikali. Hao viongozi wako ngazi tofauti, mimi nazungumzia Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Mawaziri wanaodaiwa, warejeshe hizo fedha. *(Makofi)*

Wasiporejesha, kwa sababu majina niko nayo hapa, siyataji tu kwa sababu ya kulinda zile haki zao za kibiashara. Kwa sababu majina niko nayo hapa na maombi yameshaletwa, basi wasinifikishe hapo mahali ambapo nitaanza mimi kuilipa Serikali

kwa kutumia pesa zao. Wakalipe hizo pesa ili tusifike hapo. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo sasa nawashukuru sana, leo ni siku ya Jumamosi lakini tumefanya kazi kuanzia Saa Tatu mpaka sasa na wote kwa kweli mpo hapa ndani na mkiwa na nguvu na ari kabisa. Ninawashukuru sana kwa uvumilivu wenu, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, kipekee sana namshukuru Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni nae yupo nasi tangu Saa Tatu mpaka sasa, tunakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri Mkuu, Naibu Waziri Mkuu lakini pia Waheshimiwa Mawaziri na Waheshimiwa Wabunge wote ahsanteni sana. Wakati mwingine huwa tunawasahau kidogo Makatibu hapa Mezani wakiongozwa na Katibu wa Bunge, tunawashukuru na ninyi tumekaa sote mpaka sasa. Wote kwa kweli maana kuna wengine hawako hapa ndani wako huko mitambo ndiyo maana tunaweza kuendelea kutumia, kwa hiyo tunawashukuru pia, leo ilikuwa iwe siku ya mapumziko lakini sote tumefanya kazi na naamini tumefanya kazi ambayo italisaidia Taifa letu kusonga mbele na ndiyo nia yetu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kuwashukuru, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 10.22 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 6 Novemba, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*